Iwapo utasajili ukubwa na aina ya karatasi kwenye skrini inayoonyeshwa unapopakia karatasi, kichapishi kinakujulisha ikiwa maelezo yaliyosajiliwa na mipangilio ya chapisho ni tofauti. Hii hukuzuia kupoteza karatasi na wino kwa kuhakikisha kwamba huchapishi kwenye ukubwa usiofaa wa karatasi au kuchapisha kwa rangi isiyofaa kutoka na kutumia mipangilio ambayo hailingani na aina ya katarasi.

Skrini hii haionyeshwi iwapo umelemaza **Onyesho Otom. Usanidi wa Karatasi**. Ukilemaza kipengele hiki, huwezi kuchapisha kutoka kwenye iPhone, iPad au iPod touch ukitumia AirPrint.




Iwapo ukubwa wa karatasi unaoonyeshwa ni tofauti na karatasi iliyopakiwa, teua kipengee cha kubadilisha. Iwapo mipangilio inalingana na karatasi iliyopakiwa, funga skrini.

***Kumbuka:***
*Pia unaweza kuonyesha skrini ya mipangilio ya ukubwa na aina ya karatasi kwa kuteua **Mipangilio** > **Mipangilio ya Jumla** > **Mipangilio ya Printa** > **Mipangilio Chanzo Karatasi** > **Mipangilio ya Karatasi**.*

**Maelezo Husika**

➡ "Onyesho Otom. Usanidi wa Karatasi:" kwenye ukurasa wa 265

## Orodha ya Aina za Karatasi

Ili upate matokeo mazuri ya uchapishaji, teua aina ya karatasi inayofaa karatasi hiyo.

| Jina la Midia | Aina ya Miidia | |
|---|---|---|
| | **Paneli Dhibiti** | **Kiendeshi cha Kichapishi** |
| Epson Bright White Ink Jet Paper | Karatasi tupu | Karatasi tupu |
| Epson Ultra Glossy Photo Paper | Ultra Glossy | Epson Ultra Glossy |
| Epson Premium Glossy Photo Paper<br>Epson Value Glossy Photo Paper | Haij'milika Inayongaa | Epson Premium Glossy |
| Epson Premium Semigloss Photo Paper | Haij'ilika In'gaa nusu | Epson Premium Semigloss |
| Epson Photo Paper Glossy | Glossy | Photo Paper Glossy |
| Epson Matte Paper-Heavyweight<br>Epson Double-Sided Matte Paper | Matte | Epson Matte |
| Epson Photo Quality Ink Jet Paper<br>Epson Double-sided Photo Quality Ink Jet Paper<br>Epson Photo Quality Self Adhesive Sheets | Photo Quality Ink Jet | Epson Photo Quality Ink Jet |

# Kuweka Karatasi

Unaweza kupakia karatasi au bahasha kwa kurejelea uhuishaji unaoonyeshwa kwenye skrini ya LCD ya kichapishi.

Teua ?, na kisha uteue **Jinsi ya** > **Pakia karatasi**.




Ikiwa unataka kukomesha kutazama uhuishaji, funga skrini.

**Maelezo Husika**

➡ "Mipangilio ya Ukubwa na Aina ya Karatasi" kwenye ukurasa wa 30

## Tahadhari Unapopakia Karatasi la Kichwa cha barua

- Kwa karatasi ya kichwa cha barua, teua **Letterhead** kama aina ya karatasi.
- Kwa karatasi ya kichwa cha barua, iwapo utachapisha kwenye karatasi ambayo ni ndogo kuliko mpangilio kwenye kiendeshi cha kichapishi, huenda kichapishi kikachapisha zaidi ya kingo za karatasi zinazoweza kusababisha uchafu wa wino kwenye machapisho yako na wino zaidi kuongezeka ndani ya kichapishi. Hakikisha kuwa unateua mpangilio wa ukubwa sahihi wa karatasi.
- Uchapishaji wa pande 2 na uchapishaji usio na kingo haupatikani kwa karatasi yenye mwambaa kichwa. Pia, huenda kasi ya uchapishaji ikapungua.

# Kuweka Nakala Asili

Kuweka Nakala Asili. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 34

Nakala asili ambazo Haziauniwi na ADF. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 35

# Kuweka Nakala Asili

Weka nakala asili kwenye glasi ya kitambazaji au ADF.

Unaweza kuweka nakala nyingi asili kwenye ADF.

Fuata hatua zilizo hapa chini ili kutazama uhuishaji wa kuweka nakala asili.

Teua ⓘ, na kisha uteue **Jinsi ya** > **Weka nakala asili**. Teua mbinu ya kuweka nakala asili unazotaka kutazama. Teua **Maliza** ili kufunga skirini ya uhuishaji.




### Unapotumia glasi za kitambazaji

*Tahadhari:*

*Chunga vidole vyako visikwame wakati unafunga kifuniko cha hati. La sivyo unaweza kujeruhiwa.*

***Muhimu:***

- *Unapoweka nakala kuba asili kama vile vitabu, zuia mwangaza wa nje kumulika moja kwa moja kwenye glasi ya kichanganuzi.*
- *Usitumie nguvu nyingi kupita kiasi kwenye glasi ya kichanganuzi au kifuniko cha hati. La sivyo, huenda zikaharibika.*

***Kumbuka:***

- *Ikiwa kuna taka au uchafu wowote kwenye glasi ya kichanganuzi, safu ya kutambaza inaweza kupanuka ili kuujumuisha kwa hivyo nakala asili inaweza kuonyeshwa au kupunguzwa. Ondoa uchafu wowote kwenye glasi ya kitambazaji kabla ya kutambaza.*



- *Umbali wa 1.5 mm kutoka katika kona ya glasi ya kichanganuzi hautambazwi.*
- *Nakala asili zinpowekwa kwenye ADF na kwenye glasi ya kichanganuzi, kipaumbele kinawekwa kwa nakala kwenye ADF.*
- *Ikiwa utaacha nakala asili kwenye glasi ya kichanganuzi kwa muda mrefu, zinaweza kunata kwenye sehemu ya glasi ya kichanganuzi.*

### Unapotumia ADF

> ***Muhimu:***
>
> ❏ *Usiipakie nakala asili juu ya mstari ulio chini ya alama ya pembe tatu ndani ya mwongozo wa ukingo wa ADF.*
>
> 
>
> ❏ *Usiongeze nakala za kwanza wakati wa kutambaza.*

### Maelezo Husika

➡ "Nakala asili ambazo Haziauniwi na ADF" kwenye ukurasa wa 35

## Nakala asili ambazo Haziauniwi na ADF

> ***Muhimu:***
>
> *Usiingize picha au kazi ya sana nakala asili za thamani kwenye ADF. Kuingiza vibaya kunaweza kuweka makunyanzi au kuharibu nakala asili. Tambaza nyaraka hizi kwenye kioo cha kitambazaji badala yake.*

Ili kuzuia kukwama kwa karatasi, usiweke za kwanza zifuatazo katika ADF. Kwa aina hizi, tumia kioo cha utambazaji.

❏ Nakala asili ambazo zimeraruka, kukunjwa, zenye mikunjo, zilizorota, au zilizopindika

❏ Nakala asili zenye mashimo ya mjalidi

❏ Nakala asili zilizoshikiliwa pamoja na tepu, vibanio, pini za karatasi nk.

❏ Nakala asili zilizobandikwa vibandiko au lebo

❏ Nakala asili ambazo zimekatwa bila kulingana au hazina pembe sawa

❏ Nakala asili zilizobanwa

❏ OHPs, karatasi ya kuhamisha joto, au zenye kaboni upande wa nyuma

# Kuchapisha

Kuchapisha Nyaraka. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 37

Kuchapisha kwenye Bahasha. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 64

Kuchapisha Kuarasa za Tovuti. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 65

Kuchapisha kwa kutumia Huduma ya Wingu. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 66

# Kuchapisha Nyaraka

## Kuchapisha kutoka kwenye Kompyuta — Windows

### Kuchapisha kwa kutumia Mipangilio Rahisi



***Kumbuka:***
*Utendaji unaweza kutofautiana kulingana na programu. Angalia msaada wa programu kwa maelezo.*

1. Pakia karatasi katika kichapishi.

   "Kuweka Karatasi" kwenye ukurasa wa 32

2. Fungua faili unayotaka kuchapisha.

3. Chagua **Chapisha** au **Usanidi wa Uchapishaji** katika menyu ya **Faili**.

4. Teua kichapishi chako.

5. Teua **Mapendeleo** au **Sifa** ili uende kwa dirisha la kiendeshi cha printa.



6. Badilisha mipangilio kama inavyohitajika.

   Unaweza kuona msaada wa mtandaoni kwa ufafanuzi wa vipengee vya mpangilio. Kubofya kulia kipengee huonyesha **Msaada**.

7. Bofya **OK** ili ufunge dirisha la kiendeshi cha kichapishi.

8. Bofya **Chapisha**.

### Maelezo Husika

➡ "Karatasi Inayopatikana na Uwezo" kwenye ukurasa wa 250

➡ "Orodha ya Aina za Karatasi" kwenye ukurasa wa 31

## Kuongeza Mipangilio Awali kwa Uchapishaji Rahisi

Ukiunda uwekaji wako upya mwenyewe wa mipangilio ya uchapishaji inayotumiwa mara kwa mara kwenye kiendeshi cha printa, unaweza kuchapisha kwa urahisi kwa kuchagua uwekaji upya kutoka kwa orodha.



1. Kwenye kichupo cha kiendeshi cha kichapishi cha **Kuu** au **Chaguo Zaidi**, weka kila kipengee (kama vile **Ukubwa wa Waraka** na **Aina ya Krtasi**).

2. Bofya **Uwekaji upya wa Kuongeza/Kuondoa** katika **Uwekaji Kabla Uchapishaji**.

3. Weka **Jina** na, ikihitajika, weka maoni.

4. Bofya **Hifadhi**.

   ***Kumbuka:***
   *Ili ufute uwekaji upya ulioongezwa, bofya **Uwekaji upya wa Kuongeza/Kuondoa**, chagua jina la uwekaji upya unalotaka kufuta kutoka kwa orodha, na kisha ulifute.*

5. Bofya **Chapisha**.

Wakati mwingine ukitaka kuchapisha ukitumia mipangilio sawa, chagua jina la mipangilio lililosajiliwa kutoka **Uwekaji Kabla Uchapishaji** kisha ubofye **OK**.

### Maelezo Husika

➡ "Kuweka Karatasi" kwenye ukurasa wa 32

➡ "Kuchapisha kwa kutumia Mipangilio Rahisi" kwenye ukurasa wa 37

## Kuchapisha Pande 2

Unaweza kutumia mbinu zifuatazo kuchapisha pande zote za karatasi.

❏ Uchapishaji otomatiki wa pande 2

❏ Uchapishaji mwenyewe wa pande 2
Wakati printa hii imemaliza kuchapisha upande wa kwanza, geuza karatasi ili uchapishe upande ule mwingine.



***Kumbuka:***

❏ *Kipengele hiki hakipatikani kwa uchapishaji usio na mipaka.*

❏ *Ikiwa hutatumia karatasi ambayo inafaa kwa uchapishaji wa pande 2, ubora wa uchapishaji huenda ukapungua na karatasi inaweza kukwama.*

*"Karatasi la Kuchapishwa Upande 2" kwenye ukurasa wa 252*

❏ *Kulingana na karatasi na data, wino unaweza kuvuja hadi upande huo mwingine wa karatasi.*

❏ *Huwezi kufanya mwenyewe uchapishaji wa pande 2 isipokuwa ikiwa **EPSON Status Monitor 3** imewezeshwa. Ikiwa **EPSON Status Monitor 3** imelemazwa, fikia kidirisha cha kiendesha kichapishi, bofya **Mipangilio Iliyorefushwa** kwenye kichupo cha **Utunzaji** kisha uchague **Wezesha EPSON Status Monitor 3**.*

❏ *Hata hivyo, inaweza kupatikana wakati kichapishi kinafikiwa kupitia mtandao au ni kichapishi kinachotumiwa na watu kadhaa.*

1. Kwenye kichupo cha kiendeshi cha kichapishi cha **Kuu**, teua mbinu ya **Uchapishaji wa Pande 2**.

2. Bofya **Mipangilio**, ili kuweka mipangilio inayofaa kisha ubofye **SAWA**.

3. Bofya **Uzito wa Uchapishaji**, weka mipangilio inayofaa, na kisha ubofye **SAWA**.

   Unapoweka **Uzito wa Uchapishaji**, unaweza kurekebisha uzito wa chapisho kulingana na aina ya waraka.

   ***Kumbuka:***

   ❏ *Mpangilio huu haupatikani unapoteua uchapishaji kikuli wa pande 2.*

   ❏ *Huenda uchapishaji ukawa polepole kulingana na mchanganyiko wa chaguo zilizoteuliwa za **Uzito wa Uchapishaji** katika dirisha la **Teua Aina ya Waraka** na kwa **Ubora** kwenye kichupo cha **Kuu**.*

4. Weka vipengele hivyo vingine kwenye vichupo vya **Kuu** na **Chaguo Zaidi** inavyohitajika, na kisha ubofye **SAWA**.

5. Bofya **Chapisha**.

   Kwa uchapishaji wa pande 2 wa mikono, wakati upande wa kwanza umemaliza kuchapishwa, dirisha la kidukizo linaonekana kwenye kompyuta. Fuata maagizo ya kwenye skrini.

**Maelezo Husika**

➡ "Karatasi Inayopatikana na Uwezo" kwenye ukurasa wa 250
➡ "Kuweka Karatasi" kwenye ukurasa wa 32
➡ "Kuchapisha kwa kutumia Mipangilio Rahisi" kwenye ukurasa wa 37

## Kuchapisha Kijitabu

Pia unaweza kuchapisha kijitabu ambacho kinaweza kuundwa kwa kupanga upya kurasa na kukunja chapisho.



***Kumbuka:***
- *Kipengele hiki hakipatikani na uchapishaji usio na mipaka.*
- *Ikiwa hutatumia karatasi ambayo inafaa kwa uchapishaji wa pande 2, ubora wa uchapishaji huenda ukapungua na karatasi inaweza kukwama.*

  *"Karatasi la Kuchapishwa Upande 2" kwenye ukurasa wa 252*
- *Kulingana na karatasi na data, wino unaweza kuvuja hadi upande huo mwingine wa karatasi.*
- *Huwezi kufanya mwenyewe uchapishaji wa pande 2 isipokuwa ikiwa* ***EPSON Status Monitor 3*** *imewezeshwa. Ikiwa* ***EPSON Status Monitor 3*** *imelemazwa, fikia kidirisha cha kiendesha kichapishi, bofya* ***Mipangilio Iliyorefushwa*** *kwenye kichupo cha* ***Utunzaji*** *kisha uchague* ***Wezesha EPSON Status Monitor 3****.*
- *Hata hivyo, inaweza kupatikana wakati kichapishi kinafikiwa kupitia mtandao au ni kichapishi kinachotumiwa na watu kadhaa.*

1. Kwenye kichupo cha kiendeshi cha kichapishi cha **Kuu**, teua aina ya uunganishaji wa ukingo unaotaka kutumia kutoka **Uchapishaji wa Pande 2**.

2. Bofya **Mipangilio**, teua **Kijitabu**, na kisha uteue **Kujalidi kwa Katikati** au **Kujalidi kwa Upande**.
   - Kujalidi kwa Katikati: tumia mbinu hii unapochapisha idadi kubwa ya kurasa ambazo zinaweza kupangwa na kukunjwa kwa urahisi kuwa nusu.
   - Kujalidi kwa Upande. Tumia mbinu hii unapochapisha laha moja (kurasa nne) kwa wakati mmoja, kukunja kila moja kuwa nusu kisha kuziweka pamoja kwa juzuu moja.

3. Bofya **OK**.

4. Unapochapisha data iliyo na picha na taswira nyingi, bofya **Uzito wa Uchapishaji**, na kisha uunde mipangilo inayofaa, na kisha ubofye **SAWA**.

   Unapoweka **Uzito wa Uchapishaji**, unaweza kurekebisha uzito wa chapisho kulingana na aina ya waraka.

   ***Kumbuka:***
   *Huenda uchapishaji ukawa polepole kulingana na mchanganyiko wa chaguo zilizoteuliwa za **Teua Aina ya Waraka** katika dirisha la Ma'bisho ya Uzito wa Uchapishaji na kwa **Ubora** kwenye kichupo cha **Kuu**.*

5. Weka vipengele hivyo vingine kwenye vichupo vya **Kuu** na **Chaguo Zaidi** inavyohitajika, na kisha ubofye **SAWA**.

6. Bofya **Chapisha**.

**Maelezo Husika**

➡ "Karatasi Inayopatikana na Uwezo" kwenye ukurasa wa 250
➡ "Kuweka Karatasi" kwenye ukurasa wa 32
➡ "Kuchapisha kwa kutumia Mipangilio Rahisi" kwenye ukurasa wa 37

## Kuchapisha Kurasa Kadhaa kwenye Kurasa Moja

Unaweza kuchapisha kurasa kadhaa za data kwenye laha moja ya karatasi.




***Kumbuka:***
*Kipengele hiki hakipatikani na uchapishaji usio na mipaka.*

1. Kwenye kichupo cha kiendeshi cha kichapishi cha **Kuu**, teua **2-Juu**, **4-Juu**, **6-Juu**, **8-Juu**, **9-Juu**, au **16-Juu** kama mpangilio wa **Kurasa Nyingi**.

2. Bofya **mpangilio wa muundo**, weka mipangilio inayofaa, na kisha ubofye **SAWA**.

3. Weka vipengele hivyo vingine kwenye vichupo vya **Kuu** na **Chaguo Zaidi** inavyohitajika, na kisha ubofye **SAWA**.

4. Bofya **Chapisha**.

**Maelezo Husika**

➡ "Kuweka Karatasi" kwenye ukurasa wa 32
➡ "Kuchapisha kwa kutumia Mipangilio Rahisi" kwenye ukurasa wa 37

## Kuchapisha ili Itoshee Katika Ukubwa wa Karatasi

Teua ukubwa wa karatasi uliyopakia kwenye kichapishi kama mpangilio wa Ukubwa wa Karatasi Elekea.



***Kumbuka:***
*Kipengele hiki hakipatikani na uchapishaji usio na mipaka.*

1. Kwenye kichupo cha kiendeshi cha kichapishi cha **Chaguo Zaidi**, chukua hatua zifuatazo.
   - ❏ Ukubwa wa Waraka: teua ukubwa wa karatasi uliyoweka kwenye mipangilio ya programu.
   - ❏ Karatasi ya Zao: teua ukubwa wa karatasi uliyoipakia katika kichapishi.

     **Tosheleza kwenye Ukurasa** huteuliwa kiotomatiki.

   ***Kumbuka:***
   *Bofya **Katikati** ili kuchapisha tasiwra iliyopunguzwa katikati ya karatasi.*

2. Weka vipengele hivyo vingine kwenye vichupo vya **Kuu** na **Chaguo Zaidi** inavyohitajika, na kisha ubofye **SAWA**.

3. Bofya **Chapisha**.

**Maelezo Husika**

➡ "Kuweka Karatasi" kwenye ukurasa wa 32
➡ "Kuchapisha kwa kutumia Mipangilio Rahisi" kwenye ukurasa wa 37

## Kuchapisha Hati Iliyopunguzwa au Kuongezwa ukubwa kwa Ukuzaji wowote

Unaweza kupunguza au kuongeza ukubwa wa hati na asilimia mahsusi.



***Kumbuka:***
*Kipengele hiki hakipatikani na uchapishaji usio na mipaka.*

1. Kwenye kichupo cha kiendeshi cha kichapishi **Chaguo Zaidi**, teua ukubwa wa waraka kutoka kwenye mpangilio wa **Ukubwa wa Waraka**.

2. Teua ukubwa wa karatasi unaotaka kuchapisha kutoka kwenye mpangilio wa **Karatasi ya Zao**.

3. Chagua **Punguza/Kuza Waraka**, **Kuza hadi**, na ingize asilimia.

4. Weka vipengele hivyo vingine kwenye vichupo vya **Kuu** na **Chaguo Zaidi** inavyohitajika, na kisha ubofye **SAWA**.

5. Bofya **Chapisha**.

#### Maelezo Husika

➡ "Kuweka Karatasi" kwenye ukurasa wa 32
➡ "Kuchapisha kwa kutumia Mipangilio Rahisi" kwenye ukurasa wa 37

## Kuchapisha Picha Moja kwenye Karatasi Anuwai kwa Kiuongeza Ukub wa (Kuunda Bango)

Kipengele hiki hukuruhusu kuchapisha picha moja kwenye karatasi mbalimbali. Unaweza kuunda bango kubwa kwa kuziunganisha pamoja.



1. Kwenye kichupo cha kiendeshi cha kichapishi cha **Kuu**, teua **Bango la 2x1**, **Bango la 2x2**, **Bango la 3x3**, au **Bango la 4x4** kama mpangilio wa **Kurasa Nyingi**.

2. Bofya **Mipangilio**, weka mipangilio inayofaa, na kisha ubofye **SAWA**.

   ***Kumbuka:***
   ***Chapisha Miongozo ya Kukata*** *hukuruhusu kuchapisha mwongozo wa kukata.*

3. Weka vipengele hivyo vingine kwenye vichupo vya **Kuu** na **Chaguo Zaidi** inavyohitajika, na kisha ubofye **SAWA**.

4. Bofya **Chapisha**.

**Maelezo Husika**

➡ "Kuweka Karatasi" kwenye ukurasa wa 32
➡ "Kuchapisha kwa kutumia Mipangilio Rahisi" kwenye ukurasa wa 37

### *Kutengeneza Bango Kwa Kutumia Alama Zinazolandana za Kupanga*

Huu ni mfano wa jinsi ya kutengeneza bango wakati **Bango la 2x2** iimechaguliwa, na **Alama za Mpangilio Zinazopishana** imechaguliwa katika **Chapisha Miongozo ya Kukata**.




1. Andaa Sheet 1 na Sheet 2. Kata pambizo za Sheet 1 kwenye mstari wima wa bluu kupitia katikati mwa alama za msalaba za juu na chini.



2. Weka ukingo wa Sheet 1 juu ya Sheet 2 na upange alama za msalaba, kisha uunganishe karatasi mbili pamoja kwa muda kutoka nyuma ukitumia utepe.




3. Kata karatasi zilizounganishwa mara mbili katika mstari wima wa bluu kupitia alama za kupanga (wakati huu, mstari upande wa kusho mwa alama za msalaba).



4. Unganisha karatasi pamoja kutoka nyuma ukitumia utepe.




5. Rudia hatua 1 hadi 4 uunganishe Sheet 3 na Sheet 4 pamoja ukitumia utepe.

6. Kata pambizo za Sheet 1 na Sheet 2 katika mstari mlalo wa bluu kupitia katikati mwa alama za msalaba zilizo upande wa kushoto na kulia.



7. Weka kingo ya Sheet 1 na Sheet 2 juu ya Sheet 3 na Sheet 4 na upange alamaa za msalaba, na kisha uziunganishe pamoja kwa moda kutoka nyuma.



8. Kata karatasi zilizounganishwa mara mbili katika mstari mlalo mwekundu kupitia alama za kupanga (wakati hii, mtari ulio juu mwa alama za msalaba).




9. Unganisha karatasi pamoja kutoka nyuma ukitumia utepe.



10. Kata pambizo zinazobakia katika mwingozo wa nje.




## Kuchapisha kwa Kijajuu na Kijachini

Unaweza kuchapisha maelezo kama vile jina la mtumiaji na tarehe ya kuchapisha kwenye vijajuu na vijachini.




1. Kwenye kichupo cha kiendeshi cha kichapishi cha **Chaguo Zaidi**, bofya **Vipengele vya Taswira fifi**, na kisha uteue **Kijajuu/Kijachini**.

2. **Mipangilio**, na kisha uteue vipengee unavyotaka kuchapisha na kisha ubofye OK.

   ***Kumbuka:***
   - *Ili kubainisha nambari ya ukurasa wa kwanza, teua **Nambari ya Ukurasa** kutoka kwenye nafasi unapotaka kuchapisha katika kichwa na chini kisha uteue **Nambari ya kuanzia**.*
   - *Iwapo unataka kuchapisha matini katika sehemu ya kichwa au chini, teua nafasi unayotaka kuchapisha,kisha uteue **Matini**. Andika matini unayotaka kuchapisha kwenye sehemu ya kuingiza matini.*

3. Weka vipengele hivyo vingine kwenye vichupo vya **Kuu** na **Chaguo Zaidi** inavyohitajika, na kisha ubofye **SAWA**.

4. Bofya **Chapisha**.

**Maelezo Husika**

➡ "Kuweka Karatasi" kwenye ukurasa wa 32

➡ "Kuchapisha kwa kutumia Mipangilio Rahisi" kwenye ukurasa wa 37

## Kuchapisha Taswira fifi

Unaweza kuchapisha taswira fifi kama vile "Ya siri" au ruwaza ya kutonakili kwenye machapisho yako. Iwapo utachapisha kwa ruwaza ya kutonakili, herufi zilizofichwa huonekana zinaponakiliwa ili kutofautisha nakala asili kutoka kwenye nakala.




Ruwaza ya Kizuia Nakala inapatikana chini ya masharti yafuatayo:

- Aina ya Krtasi: Karatasi tupu, Letterhead
- Isiyo na kingo: haijateluliwa
- Ubora: Wastani
- Uchapishaji wa Pande 2: Zima, Mwongozo (Kujalidi ukingo mrefu), au Mwongozo (Kujalidia ukingo mfupi)
- Usahihishaji wa Rangi: Otomatiki
- Karatasi ya Punje Fupi: haijateuliwa

***Kumbuka:***
*Unaweza pia kuongeza taswira fifi yako mwenyewe ya ruwaza ya kutonakili.*

1. Kwenye kichupo cha kiendeshi cha kichapishi cha **Chaguo Zaidi**, donoa **Vipengele vya Taswira fifi**, na kisha uteue Ruwaza ya Kizuia Nakala au Taswira fifi.

2. Bofya **Mipangilio** ili kubadilisha maelezo kama vile ukubwa, uzito, au nafasi ya ruwaza au alama.

3. Weka vipengele hivyo vingine kwenye vichupo vya **Kuu** na **Chaguo Zaidi** inavyohitajika, na kisha ubofye **SAWA**.

4. Bofya **Chapisha**.

### Maelezo Husika

➡ "Kuweka Karatasi" kwenye ukurasa wa 32
➡ "Kuchapisha kwa kutumia Mipangilio Rahisi" kwenye ukurasa wa 37

## Kuchapisha Faili Nyingi Pamoja

Laiti ya Kipangaji cha Kazi hukuruhusu kuunganisha faili nyingi zilizoundaliwa na programu tofauti na uzichapishe kama chapisho moja. Unaweza kubainisha mipangilio ya uchapishaji kwa faili zilizochanganywa, kama vile muundo wa kurasa nyingi, na uchapishaji wa pande 2.



1. Kwenye kichupo cha kiendeshi cha kichapishi cha **Kuu**, teua **Laiti ya Kipangaji cha Kazi**.

2. Bofya **Chapisha**.

   Unapoanza kuchapisha, dirisha la Laiti ya Kipangaji cha Kazi linaonyeshwa.

3. Dirisha la Laiti ya Kipangaji cha Kazi likiwa limefunguliwa, fungua faili ambayo unataka kuunganisha na faili ya sasa, na kisha urudie hatua za hapo juu.

4. Unapoteua chapisho lililoongezwa kwenye Chapisha Kipangama Lite katika kidirisha cha Laiti ya Kipangaji cha Kazi unaweza kuhariri muundo wa ukurasa.

5. Bofya **Chapisha** kutoka kwenye menyu ya **Faili** ili kuanza kuchapisha.

   ***Kumbuka:***
   *Iwapo utafunga dirisha la Laiti ya Kipangaji cha Kazi kabla ya kuongeza data yote ya uchapishaji kwenye Chapisha Kipangama, kazi ya uchapishaji unayoishughulikia sasa inakatishwa. Bofya **Hifadhi** kutoka kwenye menyu ya **Faili** ili kuhifadhi kazi ya sasa. Kiendelezi cha faili zilizohifadhiwa ni "ecl".*

   *Ili kufungua Mradi wa Kuchapisha, bofya **Laiti ya Kipangaji cha Kazi** kwenye kichupo cha kiendesha kichapishi cha **Utunzaji** ili kufungua kidirisha cha Job Arranger Lite. Kisha, chagua **Fungua** katika menyu ya **Faili** ili uchague faili hiyo.*

### Maelezo Husika

➡ "Kuweka Karatasi" kwenye ukurasa wa 32
➡ "Kuchapisha kwa kutumia Mipangilio Rahisi" kwenye ukurasa wa 37

## Kuchapisha kwa Kutumia Kipengele cha Uchapishaji Uliosawazishwa

Unaweza kuboresha uonekanaji wa matini na picha kwenye machapisho.



Chapisho Lote la Rangi kinapatikana tu mipangilio ifuatayo inapoteuliwa.

- ❏ Aina ya Krtasi: Karatasi tupu, Letterhead
- ❏ Ubora: **Wastani** au ubora wa juu
- ❏ Rangi: **Rangi**
- ❏ Programu-tumizi: Microsoft® Office 2007 au toleo la baadaye
- ❏ Ukubwa wa Matini: alama 96 au kidogo

1. Kwenye kichupo cha kiendeshi cha kichapishi cha **Chaguo Zaidi**, bofya **Chaguo za Taswira** kwenye mpangilio wa **Usahihishaji wa Rangi**.

2. Teua chaguo kutoka kwenye mpangilio wa **Chapisho Lote la Rangi**.

3. **Chaguo za Uboreshaji** ili uunde mipangilio zaidi.

4. Weka vipengele hivyo vingine kwenye vichupo vya **Kuu** na **Chaguo Zaidi** inavyohitajika, na kisha ubofye **SAWA**.

5. Bofya **Chapisha**.

   ***Kumbuka:***
   - ❏ *Baadhi ya vibambo vinaweza kubadilishwa kwa ruwaza, kama vile "+"uonekana kama "±".*
   - ❏ *Ruwaza na mistari ya chini maalum ya programu-tumizi inaweza kubadilisha maudhui yaliyochapishwa kwa kutumia mipangilio hii.*
   - ❏ *Ubora wa chapisho unaweza kupungua kwenye picha na taswira nyingine unapotumia mipangilio ya Chapisho Lote la Rangi.*
   - ❏ *Kasi ya uchapishaji inapungua unapotumia mipangilio ya Chapisho Lote la Rangi.*

### Maelezo Husika

➡ "Kuweka Karatasi" kwenye ukurasa wa 32

➡ "Kuchapisha kwa kutumia Mipangilio Rahisi" kwenye ukurasa wa 37

## Kurekebisha Rangi ya Uchapishaji

Unaweza kurekebisha rangi zinazotumiwa katika uchapishaji. Marekebisho haya hayatumiwi kwenye data ya kwanza.



**Ubora Picha** hutoa picha nzuri zaidi na rangi dhahiri zaidi kwa kurekebisha ulinganuaji, ukifishwaji, na uangavu wa data ya kwanza ya picha kiotomatiki.

***Kumbuka:***
***Ubora Picha*** *hurekebisha rangi kwa kuchanganua eneo la kipengele. Kwa hivyo, ikiwa umebadilisha eneo la kipengele kwa kupunguza, kukuza, kupogoa, au kuzungusha picha hiyo, rangi inaweza kubadilika bila kutarajiwa. Kuteua mipangilio isiyompaka pia hubadilisha eneo la mada na kusababisha kubadilika kwa rangi. Ikiwa picha iko nje ya mwimo, toni inaweza kuwa sio ya kiasili. Ikiwa rangi imebadilishwa au imekuwa sio ya asili, chapisha kwa modi nyingine mbali na* ***Ubora Picha****.*

1. Kwenye kichupo cha kiendeshi cha kichapishi cha **Chaguo Zaidi**, teua mbinu ya ubadilishaji wa rangi kutoka kwenye mpangilio wa **Usahihishaji wa Rangi**.
   - ❏ Otomatiki: mpangilio huu hurekebisha toni kiotomatiki ili kulingana na aina ya karatasi na mipangilio ya ubora wa uchapishaji.
   - ❏ Kaida: bofya **Iliyoboreshwa**, unaweza kuweka mipangilio yako binafsi.
2. Weka vipengele hivyo vingine kwenye vichupo vya **Kuu** na **Chaguo Zaidi** inavyohitajika, na kisha ubofye **SAWA**.
3. Bofya **Chapisha**.

#### Maelezo Husika

➡ "Kuweka Karatasi" kwenye ukurasa wa 32
➡ "Kuchapisha kwa kutumia Mipangilio Rahisi" kwenye ukurasa wa 37

## Kuchapisha Kusisitiza Mistari Nyembamba

Unaweza kukoleza mistari nyembemba ambayo ni nyembemba zaidi kuchapisha.



1. Kwenye kichupo cha kiendeshi cha kichapishi cha **Chaguo Zaidi**, bofya **Chaguo za Taswira** kwenye mpangilio wa **Usahihishaji wa Rangi**.
2. Teua **Sisitiza Mistari Miebamba**.

3. Weka vipengele hivyo vingine kwenye vichupo vya **Kuu** na **Chaguo Zaidi** inavyohitajika, na kisha ubofye **SAWA**.

4. Bofya **Chapisha**.

#### Maelezo Husika

➡ "Kuweka Karatasi" kwenye ukurasa wa 32

➡ "Kuchapisha kwa kutumia Mipangilio Rahisi" kwenye ukurasa wa 37

## Kuchapisha Misimbo ya Mwambaa Wazi

Unaweza kuchapisha msimbo wa mwambaa vizuri zaidi na kuurahisisha kutambazwa. Wezesha tu kipengele hiki iwapo msimbo wa mwamba uliouchapisha hauwezi kutambazwa.




Unaweza kutumia kipengele hiki chini ya hali zifuatazo.

❏ Aina ya Krtasi: Karatasi tupu, Letterhead, au Bahasha

❏ Ubora: **Wastani**

1. Kwenye kichupo cha kiendeshi cha kichapishi cha **Utunzaji**, bofya **Mipangilio Iliyorefushwa**, na kisha uteue **Modi ya Msimbo upau**.

2. Weka vipengele hivyo vingine kwenye vichupo vya **Kuu** na **Chaguo Zaidi** inavyohitajika, na kisha ubofye **SAWA**.

3. Bofya **Chapisha**.

   ***Kumbuka:***
   *Huenda upunguzaji usiwezekane kulingana na hali.*

#### Maelezo Husika

➡ "Kuweka Karatasi" kwenye ukurasa wa 32

➡ "Kuchapisha kwa kutumia Mipangilio Rahisi" kwenye ukurasa wa 37

# Kuchapisha kutoka kwenye Kompyuta — Mac OS

## Kuchapisha kwa kutumia Mipangilio Rahisi



***Kumbuka:***
*Utendaji na skrini zinaweza kutofautiana kulingana na programu. Angalia msaada wa programu kwa maelezo.*

1. Pakia karatasi katika kichapishi.

   "Kuweka Karatasi" kwenye ukurasa wa 32

2. Fungua faili unayotaka kuchapisha.

3. Chagua **Chapisha** kutoka kwa menyu ya **Faili** au amri nyingine ili ufikie mawasiliano ya uchapishaji.

   Inapohitajika, bofya **Onyesha Maelezo** au ▼ ili uongeze dirisha la uchapishaji.

4. Teua kichapishi chako.

5. Teua **Mipangilio ya Kuchapisha** kutoka kwa menyu ibukizi.




6. Badilisha mipangilio kama inavyohitajika.

7. Bofya **Chapisha**.

#### Maelezo Husika

➡ “Karatasi Inayopatikana na Uwezo” kwenye ukurasa wa 250

➡ “Orodha ya Aina za Karatasi” kwenye ukurasa wa 31

## Kuongeza Mipangilio Awali kwa Uchapishaji Rahisi

Ukiunda uwekaji wako upya mwenyewe wa mipangilio ya uchapishaji inayotumiwa mara kwa mara kwenye kiendeshi cha printa, unaweza kuchapisha kwa urahisi kwa kuchagua uwekaji upya kutoka kwa orodha.



1. Weka kila kipengee kama vile **Mipangilio ya Kuchapisha** na **Mpangilio** (**Ukbwa wa Krtasi**, **Media Type** na mengineyo).

2. Bofya **Mipangilio awali** ili uhifadhi mipangilio ya sasa kama mipangilio awali.

3. Bofya **OK**.

   ***Kumbuka:***
   *Ili kufuta uwekaji upya ulioongezwa, bofya **Uwekaji upya** > **Onyesha Uwekaji Upya**, teua jina la uwekaji upya unalotaka kufuta kutoka kwa orodha, na kisha ulifute.*

4. Bofya **Chapisha**.

Wakati mwingine ukitaka kuchapisha ukitumia mipangilio sawa, chagua jina la mipangilio awali lililosajiliwa kutoka **Mipangilio awali**.

#### Maelezo Husika

➡ “Kuweka Karatasi” kwenye ukurasa wa 32

➡ “Kuchapisha kwa kutumia Mipangilio Rahisi” kwenye ukurasa wa 56

## Kuchapisha Pande 2

Unaweza kuchapisha katika pande zote za karatasi.



***Kumbuka:***

- *Kipengele hiki hakipatikani na uchapishaji usio na mipaka.*
- *Ikiwa hutatumia karatasi ambayo inafaa kwa uchapishaji wa pande 2, ubora wa uchapishaji huenda ukapungua na karatasi inaweza kukwama.*

  *"Karatasi la Kuchapishwa Upande 2" kwenye ukurasa wa 252*
- *Kulingana na karatasi na data, wino unaweza kuvuja hadi upande huo mwingine wa karatasi.*

1. Teua **Two-sided Printing Settings** kutoka kwa menyu ibukizi.
2. Teua zinazofungana kwenye **Two-sided Printing**.
3. Teua aina ya asili kwenye **Document Type**.

   ***Kumbuka:***
   - *Huenda uchapishaji ukapungua kasi kulingana na mpangilio wa* ***Document Type****.*
   - *Iwapo unachapisha data yenye uzito wa juu kama vile picha au grafu, teua* ***Text & Photos*** *au* ***Text & Graphics*** *kama mpangilio wa* ***Document Type****. Ikiwa kuchakaa kutatokea au picha ivuje wino upande wa nyuma, rekebisha uzito wa chapa na muda wa wino kukauka kwa kubofya alama ya kishale kando ya* ***Adjustments****.*
4. Weka vipengele hivyo vingine inavyohitajika.
5. Bofya **Chapisha**.

### Maelezo Husika

➡ "Karatasi Inayopatikana na Uwezo" kwenye ukurasa wa 250
➡ "Kuweka Karatasi" kwenye ukurasa wa 32
➡ "Kuchapisha kwa kutumia Mipangilio Rahisi" kwenye ukurasa wa 56

## Kuchapisha Kurasa Kadhaa kwenye Kurasa Moja

Unaweza kuchapisha kurasa kadhaa za data kwenye laha moja ya karatasi.



1. Chagua **Mpangilio** katika menyu ya kidukizo.

2. Weka idadi ya kurasa katika **Kurasa kwa Ukurasa**, **Mwelekeo wa Mpangilio** (mpangilio wa ukurasa), na **Mpaka**.

3. Weka vipengele hivyo vingine inavyohitajika.

4. Bofya **Chapisha**.

**Maelezo Husika**

➡ "Kuweka Karatasi" kwenye ukurasa wa 32

➡ "Kuchapisha kwa kutumia Mipangilio Rahisi" kwenye ukurasa wa 56

## Kuchapisha ili Itoshee Katika Ukubwa wa Karatasi

Teua ukubwa wa karatasi uliyopakia kwenye kichapishi kama mpangilio wa Ukubwa wa Karatasi Elekea.



1. Chagua ukubwa wa karatasi unayoweka katika programu kama mpangilio wa **Ukbwa wa Krtasi**.

2. Chagua **Ushughulikiaji wa Karatasi** kutoka kwa menyu ya kidukizo.

3. Chagua **Skeli ili itoshee katika ukubwa wa karatasi**.

4. Teua ukubwa wa karatasi uliyopakia kwenye kichapishi kama mpangilio wa **Ukubwa wa Karatasi Elekea**.

5. Weka vipengele hivyo vingine inavyohitajika.

6. Bofya **Chapisha**.

**Maelezo Husika**

➡ "Kuweka Karatasi" kwenye ukurasa wa 32

➡ "Kuchapisha kwa kutumia Mipangilio Rahisi" kwenye ukurasa wa 56

## Kuchapisha Hati Iliyopunguzwa au Kuongezwa ukubwa kwa Ukuzaji wowote

Unaweza kupunguza au kuongeza ukubwa wa hati na asilimia mahsusi.



1. Chagua **Chapisha** kutoka kwa menyu ya **Faili** au amri nyingine ili ufikie mawasiliano ya uchapishaji.

2. Teua **Mpangilio wa Ukurasa** kwenye menyu ya **Faili** ya programu.

3. Teua **Kichapishi**, **Ukubwa wa Karatasi**, weka asilimia kwenye **Mizani** kisha ubofye **OK**.

   ***Kumbuka:***
   *Teua ukubwa wa karatasi ulioweka kwenye programu kuwa mpangilio wako wa **Ukubwa wa Karatasi**.*

4. Weka vipengele hivyo vingine inavyohitajika.

5. Bofya **Chapisha**.

**Maelezo Husika**

➡ "Kuweka Karatasi" kwenye ukurasa wa 32

➡ "Kuchapisha kwa kutumia Mipangilio Rahisi" kwenye ukurasa wa 56

### Kurekebisha Rangi ya Uchapishaji

Unaweza kurekebisha rangi zinazotumiwa katika uchapishaji. Marekebisho haya hayatumiwi kwenye data ya kwanza.



**Ubora Picha** hutoa picha nzuri zaidi na rangi dhahiri zaidi kwa kurekebisha ulinganuaji, ukifishwaji, na uangavu wa data ya kwanza ya picha kiotomatiki.

***Kumbuka:***
*__Ubora Picha__ hurekebisha rangi kwa kuchanganua eneo la kipengele. Kwa hivyo, ikiwa umebadilisha eneo la kipengele kwa kupunguza, kukuza, kupogoa, au kuzungusha picha hiyo, rangi inaweza kubadilika bila kutarajiwa. Kuteua mipangilio isiyompaka pia hubadilisha eneo la mada na kusababisha kubadilika kwa rangi. Ikiwa picha iko nje ya mwimo, toni inaweza kuwa sio ya kiasili. Ikiwa rangi imebadilishwa au imekuwa sio ya asili, chapisha kwa modi nyingine mbali na __Ubora Picha__.*

1. Chagua **Kulinganisha Rangi** katika menyu ya kidukizo, na kisha uchague **EPSON Color Controls**.

2. Teua **Color Options** kutoka kwenye menyu ibukizi, na kisha uteue moja ya chaguo zinazopatikana.

3. Bofya mshale kando ya **Mipangilio Iliyoboreshwa** na uweke mipangilio inayofaa.

4. Weka vipengele hivyo vingine inavyohitajika.

5. Bofya **Chapisha**.

#### Maelezo Husika

➡ "Kuweka Karatasi" kwenye ukurasa wa 32
➡ "Kuchapisha kwa kutumia Mipangilio Rahisi" kwenye ukurasa wa 56

## Kuchapisha Nyaraka kutoka Vifaa Maizi (iOS)

Unaweza kuchapisha nyaraka kutoka vifaa maizi kama vile simu mahiri au kompyuta kibao.



### Kuchapisha Nyaraka Ukitumia Epson Smart Panel

***Kumbuka:***
*Uendeshaji unaweza kutofautiana kulingana na kifaa.*

1. Sanidi kichapishi chako kwa uchapishi wa pasi waya.

2. Ikiwa Epson Smart Panel haijasakinishwa, isakinishe.

   "Programu ya Kuendesha Kichapishi Rahisi kutoka kwenye Kifaa maizi (Epson Smart Panel)" kwenye ukurasa wa 258

3. Unganisha kifaa chako maizi kupitia kipanga njia pasiwaya.

4. Anzisha Epson Smart Panel.

5. Teua menyu ya kutambaza waraka kwenye skrini ya nyumbani.

6. Teua waraka unaotaka kuchapisha.

7. Anza kuchapisha.

## Kuchapisha Nyaraka Ukitumia AirPrint

AirPrint huwezesha uchapishaji pasiwaya wa papo hapo kutoka kwenye iPhone, iPad, iPod ya mguso, na Mac bila kuhitajika kusakinisha viendeshi au kupakua programu.

Works with Apple AirPrint

***Kumbuka:***
*Iwapo ulilemaza ujumbe wa usanidi wa karatasi kwenye paneli dhibiti ya kichapishi chako, huwezi kutumia AirPrint. Tazama kiungo kilicho hapa chini ili kuwezesha ujumbe, iwapo inahitajika.*

1. Sanidi kichapishi chako kwa uchapishi wa pasi waya. Tazama kiungo cha hapa chini.

   http://epson.sn

2. Unganisha kifa chako cha Apple kwenye mtandao sawa wa pasi waya ambao kichapishi chako kinatumia.

3. Chapisha kutoka kwa kifaa chako hadi kwa printa.

   ***Kumbuka:***
   *Kwa maelezo, tazama ukurasa wa AirPrint kwenye tovuti ya Apple.*

### Maelezo Husika

➡ "Hakiwezi Kuchapisha Ingawa Muunganisho Umewekwa (iOS)" kwenye ukurasa wa 160

# Kuchapisha Nyaraka kutoka Vifaa Maizi (Android)

Unaweza kuchapisha nyaraka kutoka vifaa maizi kama vile simu mahiri au kompyuta kibao.



## Kuchapisha Nyaraka Ukitumia Epson Smart Panel

***Kumbuka:***
*Uendeshaji unaweza kutofautiana kulingana na kifaa.*

1. Sanidi kichapishi chako kwa uchapishi wa pasi waya.
2. Ikiwa Epson Smart Panel haijasakinishwa, isakinishe.

   "Programu ya Kuendesha Kichapishi Rahisi kutoka kwenye Kifaa maizi (Epson Smart Panel)" kwenye ukurasa wa 258
3. Unganisha kifaa chako maizi kupitia kipanga njia pasiwaya.
4. Anzisha Epson Smart Panel.
5. Teua menyu ya kutambaza waraka kwenye skrini ya nyumbani.
6. Teua waraka unaotaka kuchapisha.
7. Anza kuchapisha.

## Kuchapisha Nyaraka kwa kutumia Epson Print Enabler

Unaweza kuchapisha hati, barua pepe, picha au kurasa za wavuti pasiwaya moja kwa moja kutoka katika simu au kompyuta yako kibao Android (Android v 4.4 au jipya zaidi). Kwa kudonoa mara chache tu, kifaa chako cha Android kinaweza kugundua kichapishi cha Epson ambacho kimeunganishwa kwenye mtandao sawa pasiwaya.

***Kumbuka:***
*Uendeshaji unaweza kutofautiana kulingana na kifaa.*

1. Sanidi kichapishi chako kwa uchapishi wa pasi waya. Tazama kiungo cha hapa chini.

   http://epson.sn
2. Sakinisha programu-jalizi ya Kiwezeshaji cha Kichapishi cha Epson kutoka kwa Google Play.
3. Unganisha kifa chako cha Android kwenye mtandao sawa wa pasi waya ambao kichapishi chako kinatumia.
4. Nenda katika **Mipangilio** kwenye kifaa cha Android, teua **Kuchapisha** kisha wezesha Epson Print Enabler.
5. Kutoka katika programu ya Android kama vile Chrome, donoa aikoni ya menyu na uchapishe kilicho kwenye skrini.

   ***Kumbuka:***
   *Iwapo hutaona kichapishi chako, donoa **Vichapishi Vyote** na uteue kichapishi chako.*

## Kuchapisha Ukitumia Mopria Print Service

Mopria Print Service huwezesha uchapishaji wa papo hapo wa pasi waya kutoka kwenye simu maizi au kompyuta ndogo za Android.

1. Sakinisha Mopria Print Service kutoka Google Play.

2. Pakia karatasi katika kichapishi.

3. Sanidi kichapishi chako kwa uchapishi wa pasi waya. Tazama kiungo cha hapa chini.

   http://epson.sn

4. Unganisha kifa chako cha Android kwenye mtandao sawa wa pasi waya ambao kichapishi chako kinatumia.

5. Chapisha kutoka kwa kifaa chako hadi kwa printa.

   ***Kumbuka:***
   *Kwa maelezo zaidi, fikia tovuti ya Mopria Web katika https://mopria.org.*

**Maelezo Husika**

➡ “Kuweka Karatasi” kwenye ukurasa wa 32

# Kuchapisha kwenye Bahasha

## Kuchapisha Bahasha kutoka kwa Kompyuta (Windows)

1. Pakia bahasha kwenye kichapishi.

   “Kuweka Karatasi” kwenye ukurasa wa 32

2. Fungua faili unayotaka kuchapisha.

3. Fikia dirisha la kiendeshi cha kichapishi.

4. Teua ukubwa wa bahasha kutoka **Ukubwa wa Waraka** kwenye kichupo cha **Kuu** kisha uteue **Bahasha** kutoka **Aina ya Krtasi**.

5. Weka vipengele hivyo vingine kwenye vichupo vya **Kuu** na **Chaguo Zaidi** inavyohitajika, na kisha ubofye **SAWA**.

6. Bofya **Chapisha**.

### Kuchapisha Bahasha kutoka kwa Kompyuta (Mac OS)

1. Pakia bahasha kwenye kichapishi.

   "Kuweka Karatasi" kwenye ukurasa wa 32

2. Fungua faili unayotaka kuchapisha.

3. Chagua **Chapisha** kutoka kwa menyu ya **Faili** au amri nyingine ili ufikie mawasiliano ya uchapishaji.

4. Teua ukubwa kama mpangilio wa **Ukbwa wa Krtasi**.

5. Teua **Mipangilio ya Kuchapisha** kutoka kwa menyu ibukizi.

6. Teua **Bahasha** kama mpangilio wa **Media Type**.

7. Weka vipengele hivyo vingine inavyohitajika.

8. Bofya **Chapisha**.

# Kuchapisha Kuarasa za Tovuti

### Kuchapisha Kurasa za Tovuti kutoka Kompyuta

Epson Photo+ hukuruhusu kuonyesha kurasa za wavuti, kupogoa eneo lililobainishwa na kisha kuhairir na kuzichapisha. Angalia msaada wa programu kwa maelezo.

### Kuchapisha Kurasa za Tovuti kutoka kwa Vifaa Maizi

***Kumbuka:***
*Uendeshaji unaweza kutofautiana kulingana na kifaa.*

1. Sanidi kichapishi chako kwa uchapishi wa pasi waya.

2. Ikiwa Epson Smart Panel haijasakinishwa, isakinishe.

   "Programu ya Kuendesha Kichapishi Rahisi kutoka kwenye Kifaa maizi (Epson Smart Panel)" kwenye ukurasa wa 258

3. Unganisha kifaa chako maizi kwenye mtandao pasiwaya kilipounganishwa kichapishi chako.

4. Fungua ukurasa wa tovuti unaotaka kuchapisha kwenye programu ya kivinjari chako cha wavuti.

5. Donoa **Shiriki** kutoka katika menyu ya programu ya kivinjari chako cha wavuti.

6. Teua **Smart Panel**.

7. Donoa **Chapisha**.

# Kuchapisha kwa kutumia Huduma ya Wingu

Kwa kutumia huduma ya Epson Connect inayopatikana mtandaoni, unaweza kuchapisha kutoka kwa simu yako mahiri, kijilaptopu, au laptopu, wakati wowote na kutoka mahali popote. Ili kutumia huduma hii, unahitaji kusajili mtumiaji na kichapishi kwenye Epson Connect.



Vipengele vinavyopatikana kwenye Wavuti ni kama vifuatavyo.

- Email Print

  Unapotuma barua pepe iliyo na viambatisho kama vile nyaraka au picha kwenye anwani ya barua pepe iliyopangiwa kichapishi, unaweza kuchapisha barua pepe na viambatisho kutoka maeneo ya mbali kama vile nyumbani kwako au kichapishi cha ofisini.

- Epson iPrint

  Programu hii ni ya iOS na Android, na hukuruhusu kuchapisha na kutambaza kutoka katika smartphone au kompyuta kibao. Unaweza kuchapisha nyaraka, picha na tovuti kwa kuzituma moja kwa moja kwenye kichapishi kilicho kwenye LAN pasiwaya.

- Remote Print Driver

  Hiki ni kiendeshi kilichoshirikiwa kinachoauniwa na Kiendeshi cha Kuchapisha Mbali. Unapochapisha ukitumia kichapishi ukiwa mbali, unaweza kuchapisha kwa kubadilisha kichapishi kwenye kidirisha cha kawaida cha programu.

Angalia kitovu cha tovuti cha Epson Connect kwa maelezo kuhusu jinsi ya kuweka mipangilio na kuchapisha.

https://www.epsonconnect.com/

http://www.epsonconnect.eu (Ulaya peke yake)

## Inasajili kwenye Huduma ya Muunganisho wa Epson kutoka kwa Paneli Dhibiti

Fuata hatua zilizo hapa chini ili kusajili kichapishi.

1. Teua **Mipangilio** kwenye paneli dhibiti.

2. Teua **Mipangilio ya Jumla** > **Mipangilio ya Huduma ya Wavuti** > **Hdma za Kuunginsha Epson** > **Batilisha usajili** ili kuchapisha laha la usajili.

3. Fuata maagizo kwenye laha la usajili ili kusajili kichapishi.

# Kunakili

Mbinu Zinazopatikana za Kunakili. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 69

Chaguo Msingi za Menyu kwa Kunakjili. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .73

Chaguo Mahiri za Menyu kwa Kunakili. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 74

# Mbinu Zinazopatikana za Kunakili

Weka nakala asili kwenye glasi ya kitambazaji au ADF, na kisha uteue menyu ya **Nakili** kwenye skrini ya nyumbani.

## Kunakili Nakala Asili

Unaweza kunakili nakala asili za ukubwa thabiti au ukubwa maalum kwa rangi au rangi moja.



1. Pakia karatasi katika kichapishi.

   "Kuweka Karatasi" kwenye ukurasa wa 32

2. Weka nakala za kwanza.

   Iwapo unataka kunakili nakala asili nyingi, weka nakala zote asili kwenye ADF.

   "Kuweka Nakala Asili" kwenye ukurasa wa 34

3. Teua **Nakili** kwenye skrini ya nyumbani.

4. Teua kichupo cha **Nakili**, na kisha uteue **Nyeusi na Nyeupe** au **Rangi**.




5. Donoa ◇.

## Kunakili kwenye Pande 2

Nakili nakala nyingi asili kwenye pande zote mbili za karatasi.



1. Weka nakala zote asili zikiwa zinaangalia juu katika ADF.

   "Kuweka Nakala Asili" kwenye ukurasa wa 34

   > ***Muhimu:***
   > *Iwapo unataka kunakili nakala asili ambazo haziauniwi na ADF, tumia glasi ya kitambazaji.*
   >
   > *"Nakala asili ambazo Haziauniwi na ADF" kwenye ukurasa wa 35*

   ***Kumbuka:***
   *Pia unaweza kuweka nakala asili kwenye glasi ya kitambazaji.*

   *"Kuweka Nakala Asili" kwenye ukurasa wa 34*

2. Teua **Nakili** kwenye skrini ya nyumbani.

3. Teua kichupo cha **Nakili**, na kisha uteue (**Pande 2**) > **1>Pande 2**.

4. Bainisha mwelekeo asili na mkao wa kubana, na kisha uteue **Sawa**.

5. Donoa ◇.

## Kunakili kwa Kupanua au Kupunguza

Unaweza kunakili nakala asili kwa upanuzi uliobainishwa.



1. Weka nakala za kwanza.

   Iwapo unataka kutambaza nakala asili nyingi, weka nakala zote asili kwenye ADF.

   "Kuweka Nakala Asili" kwenye ukurasa wa 34

2. Teua **Nakili** kwenye skrini ya nyumbani.

3. Teua kichupo cha **Mipangilio Mahiri**, na kisha uteue **Kuza**.

4. Bainisha kiwango cha kupanua au kupunguza, na kisha uteue **Sawa**.

5. Donoa ◇ kwenye kichupo cha **Nakili**.

## Kunakili Nakala asili Anuwai kwenye Laha Moja

Unaweza kunakili nakala asili anuwai kwenye laha moja la karatasi.




1. Weka nakala zote asili zikiwa zinaangalia juu katika ADF.

   “Kuweka Nakala Asili” kwenye ukurasa wa 34

   Ziweke katika mwelekeo ulioonyeshwa kwenye mfano.

   ❏ Nakala asili za Taswira

   

   ❏ Nakala asili la Mandhari

   


> **_Muhimu:_**
>
> *Iwapo unataka kunakili nakala asili ambazo haziauniwi na ADF, tumia glasi ya kitambazaji.*
>
> *“Nakala asili ambazo Haziauniwi na ADF” kwenye ukurasa wa 35*

**_Kumbuka:_**
*Pia unaweza kuweka nakala asili kwenye glasi ya kitambazaji.*

*“Kuweka Nakala Asili” kwenye ukurasa wa 34*

2. Teua **Nakili** kwenye skrini ya nyumbani.

3. Teua kichupo cha **Mipangilio Mahiri**, na kisha uteue **Kurasa Nyingi** > **2-juu**.

4. Bainisha mpangilio wa muundo na mwelekeo, na kisha uteue **Sawa**.

5. Donoa ◇ kwenye kichupo cha **Nakili**.

## Kunakili Nakala Asili Kwa Kutumia Ubora Unaofaa

Unaweza kunakili anakala asili bila vivuli na mashimo yaliyotobolewa.



1. Weka nakala za kwanza.

   Iwapo unataka kunakili nakala asili nyingi, weka nakala zote asili kwenye ADF.

   "Kuweka Nakala Asili" kwenye ukurasa wa 34

2. Teua **Nakili** kwenye skrini ya nyumbani.

3. Teua kichupo cha **Mipangilio Mahiri**, teua **Ondoa Kivuli** au **Ondoa Mashimo ya Panchi**, na kisha uwezeshe mpangilio.

4. Donoa ◇ kwenye kichupo cha **Nakili**.

## Kunakili kadi ya Kitambulisho

Hutambaza pande zote mbili za kadi ya utambulisho na hunakili upande mmoja wa karatasi.



1. Weka nakala asili kwenye glasi ya kitambazaji.

   "Kuweka Nakala Asili" kwenye ukurasa wa 34

2. Teua **Nakili** kwenye skrini ya nyumbani.

3. Teua kichupo cha **Mipangilio Mahiri**, na kisha uwezeshe **Nakala ya Kadi ya ID**.

4. Donoa ◇ kwenye kichupo cha **Nakili**.

## Kunakili Bila Pambizo

Hunakili bila pambizo kwenye kingo. Taswira imekuzwa kidogo ili kuondoa pambizo kutoka kwenye kingo za karatasi.




1. Weka nakala asili kwenye glasi ya kitambazaji.

   "Kuweka Nakala Asili" kwenye ukurasa wa 34

2. Teua **Nakili** kwenye skrini ya nyumbani.

3. Teua kichupo cha **Mipangilio Mahiri**, na kisha uwezeshe **Nakala Isiyo na mipaka**.

4. Bainisha **Upanuzi**.

5. Donoa ◇ kwenye kichupo cha **Nakili**.

# Chaguo Msingi za Menyu kwa Kunakjili

***Kumbuka:***
*Huenda vipengee visipatikane kulingana na mipangilio mingine uliyofanya.*

Nyeusi na Nyeupe:

Hunakili nakala asili katika rangi nyeusi na nyeupe (rangi moja).

Rangi:

Hunakili nakala asili katika rangi.

(Pande 2):

Teua muundo wa pande 2.

❏ 1→Upande 1

Hunakili upande mmoja wa hati halisi kwenye karatasi ya upande moja.

❏ 1>Pande 2

Hunakili hati halisi zenye pande mbele kwenye pande mbili za karatasi moja. Teua mwelekeo wa nakala asili na eneo la kuunganisha karatasi.

(Uzito):

Ongeza kiwango cha uzito wakati matokeo ya kunakili yamefifia. Punguza kiwango cha uzito wino unapomwagika.

# Chaguo Mahiri za Menyu kwa Kunakili

***Kumbuka:***
*Huenda vipengee visipatikane kulingana na mipangilio mingine uliyofanya.*

Mipangilio ya K'si:

Teua ukubwa wa karatasi na aina ya karatasi uliyopakia.

Kuza:

Husanidi mgao wa ukuzaji wa upanuaji au upunguzaji. Iwapo unataka kupunguza au kuongeza ukubwa wa nakala asili kwa asilimia maalum, teua thamani, na kisha uingize asiliamia ndani ya kiwango cha 25 hadi 400%.

- Saizi Halisi

  Hunakili kwa ukuzaji wa 100%.

- A4→A5 na nyingine

  Hukuza au kupunguza nakala asili kiotomatiki ili kutoshea kwenye ukubwa wa karatasi bainifu.

- Tosheza Ukrs Oto

  Hutambua eneo la kuchapisha na kukuza kiotomatiki au kupunguza nakala asili ili itoshee kwenye ukubwa wa karatasi uliyoteua. Wakati kuna pambizo nyeupe kwenye nakala asili, pambizo hizo nyeupe kutoka kwenye alama ya kona ya kioo cha kitambazaji zinatambuliwa kama eneo la kutambaza, lakini pambizo katika upande mkabala zinaweza kupunwa.




Saizi ya Hati:

Chagua ukubwa wa nakala yako ya kwanza. Unaponakili nakala asili za ukubwa usio wastani, teua ukubwa unaokaribiana na nakala yako asili.

Kurasa Nyingi:

Teua muundo wa nakala.

- ❏ Ukurasa Mmoja

  Hunakili hati halisi zenye pande mbili kwenye karatasi moja.
- ❏ 2-juu

  Hunakili hati halisi zenye pande mbili kwenye karatasi moja yenye mpangilio wa 2-up. Teua mpangilio wa muundo na mwelekeo wa nakala yako asili.

### Ubora:

Teua ubora wa nakili. Kuteua **Juu** hutoa uchapishaji wa hali ya juu zaidi, lakini kasi ya uchapishaji huenda ikawa ya chini.

### Mwelekeo wa Hati:

Teua mwelekeo wa nakala yako asili.

### Ondoa Kivuli:

Huondoa vivuli vinavyoonekana kwenye nakala unaponakili karatasi nzito au vinavyotokea katikati ya nakala unaponakili kijitabu.

### Ondoa Mashimo ya Panchi:

Huondoa mashino ya kufunga wakati wa kunakili.

### Nakala ya Kadi ya ID:

Hutambaza pande zote mbili za kadi ya utambulisho na hunakili upande mmoja wa karatasi.

### Nakala Isiyo na mipaka:

Hunakili bila pambizo kwenye kingo. Taswira imekuzwa kidogo ili kuondoa pambizo kutoka kwenye kingo za karatasi. Teua kiwango cha kubadilisha ukubwa kwenye mpangilio wa **Upanuzi**.

### Ondoa Mipangilio Yote:

Rejesha mipangilio ya nakala kuwa chaguomsingi.

# Utambazaji


Maelezo Msingi kuhusu Utambazaji. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .77

Kutambaza Nakala Asili kwenye Kompyuta. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 80

Kutambaza Nakala Asiili kwenye Wingu. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .81

Kutambaza kwa Kutumia WSD. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 83

Kutambaza Nakala Asili kwenye Kifaa Maizi. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .85

Utambazaji wa Kina. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 85

# Maelezo Msingi kuhusu Utambazaji

## Je, “Utambazaji” ni nini?

“Utambazaji” ni mchakato wa kubadilisha taarifa zinazoonekana za data kwenye karatasi (kama vile nyaraka, mibano ya gazeti, picha, ufafanuzi ulioandikwa kwa mikono na kadhalika) kuwa data ya taswira ya kidijitali.

Unaweza kuhifadhi data iliyotambaza kuwa taswira ya kidijitali kama vile JPEG au PDF.

Kisha unaweza kuchapisha taswira, kuituma kupitia barua pepe na kadhalika.



## Matumizi ya Utambazaji

Unaweza kutumia utambazaji kwa njia mbalimbali ili kufanya maisha kuwa rahisi zaidi.

- ❏ Kwa kutambaza waraka wa karatasi na kuigueza kuwa data ya kidjitali, unaweza kuisoma kwenye kompyuta ai kifaa maizi.
- ❏ Kwa kutambaza tiketi au mabngo kuwa data ya kidijitali, unaweza kutupa nakala asili na kupunguza mrundiko.
- ❏ Kwa kutambaza nyaraka muhimu, unaweza kuweka nakala rudufu kwenye huduma ya wingu au midia nyingine ya uhifadhi, uzipate endapo zitapotea.
- ❏ Unaweza kutuma picha au nayaraka zilizotambazwa kwa marafiki kupitaia barua pepe.
- ❏ Kwa kutambaza ufafanuzi uliochorwa kwa mikono na kadhalika, unaweza kuushiriki kwenye mitandao ya kijamii katika ubora wa juu zaidi kuliko kupiga tu picha kwenye kifaa chako maizi.
- ❏ Kwa kutambaza kurasa zako unazopenda kutoka magazeti au jarida, unaweza kuzihifadhi na kisha kutupa nakala asili.

## Mbinu Zinazopatikana za Utambazaji

Unaweza kutumia mbinu zozote kati ya zifuatazo kutambaza ukitumia kichapishi hiki.

### Utambazaji kwa Kompyuta

   Tazama msaada wa kiendeshi cha PC-FAX kwa ufafanuzi kwenye kila kipengee cha mpangilio.

   Bofya ? upande wa chini kushoto wa dirisha ili kufungua msaada wa kiendeshi cha PC-FAX.

6. Teua menyu ya Recipient Settings, na kisha ubainishe mpokeaji.

   ❏ Kubanisha mpokeaji (jina, faksi, nambari, nakadhalika) moja kwa moja:

   Bofya kipengee cha **Add**, ingiza maelezo yanayofaa, na kisha ubofye . Mpokeaji anaongezwa kwenye Recipient List iliyoonyeshwa sehemu ya juu ya dirisha.

   Iwapo umeteua “Enter fax number twice” kwenye mipangilio ya kiendeshi cha PC-FAX, unahitaji kuingiza nambari hiyo tena unapobofya .

   Iwapo laini ya muunganisho wa faksi yako inahitaji msimbo wa kiambishi awali, ingiza External Access Prefix.

   ***Kumbuka:***
   *Iwapo Aina ya Laini ya kichapishi chako imewekwa kwa **PBX** na msimbo wa ufikiaj umewekwa kwa # (hashi) badala ya kuingiza msimbo halisi wa kiambishi awali, ingiza # (hashi). Kwa maelezo, angalia Aina ya Laini kwenye Mipangilio Msingi kutoka kwenye kiungo cha maelezo Husiani hapa chini.*

   ❏ Kuteua mpokeaji (jina, faksi, nambari, nakadhalika) kutoka kwenye kitabu cha simu:

   Iwapo mpokeaji amehifadhiwa kwenye kitabu cha anwani, bofya . Teua mpokeaji kutoka kwenye orodha, na kisha ubofye **Add** > **OK**.

   Iwapo laini ya muunganisho wa faksi yako inahitaji msimbo wa kiambishi awali, ingiza External Access Prefix.

   ***Kumbuka:***
   *Iwapo Aina ya Laini ya kichapishi chako imewekwa kwa **PBX** na msimbo wa ufikiaj umewekwa kwa # (hashi) badala ya kuingiza msimbo halisi wa kiambishi awali, ingiza # (hashi). Kwa maelezo, angalia Aina ya Laini kwenye Mipangilio Msingi kutoka kwenye kiungo cha maelezo Husiani hapa chini.*

7. Angalia mipangilio ya mpokeaji, na kisha ubofye **Fax**.

   Inaanza kutuma.

   Hakikisha jina pamoja na nambari ya faksi ya mpokeaji ni sahihi kabla ya usambazaji.

   ***Kumbuka:***
   ❏ *Iwapo utabofya ikoni ya kichapishi kwenye Dock, skrini ya kukagua hali ya usambazaji inaonyeshwa. Ili kusitisha kutuma, bofya data, na kisha ubofye **Delete**.*

   ❏ *Iwapo kosa litatokea wakati wa usambazaji, ujumbe wa **Sending failed** unaonyeshwa. Angalia rekodi za usambazaji kwenye skrini ya **Fax Transmission Record**.*

   ❏ *Huenda nyaraka zilizo na ukubwa uliochanganywa wa karatasi zisitumwe sahihi.*

**Maelezo Husika**

➡ “Mipangilio Msingi” kwenye ukurasa wa 269

# Kupokea Faksi kwenye Kompyuta

Faksi zinaweza kupokewa kwa kichapishi na kuhifadhiwa kwenye umbizo la PDF kwenye kompyuta iliyounganishwa kwenye kichapishi. Tumia FAX Utility (programu tumizi) ili kuunda mipangilio.

Kwa maelezo kuhusu jinsi ya kuendesha FAX Utility, tazama Basic Operations kwenye msaada wa FAX Utility (yanayoonyeshwa kwenye dirisha kuu). Iwapo skrini ya ingizo la nywila itaonyeshwa kwenye skrini ya kompyuta unapounda mipangilio, ingiza nywila. Iwapo hujui nywila, wasiliana na msimamizi wako.

***Kumbuka:***

- *Angalia iwapo FAX Utility na kiendeshi cha PC-FAX kimesakinishwa na mipangilio ya FAX Utility imewekwa kabla ya kutumia kipengele hiki.*

  *"Programu-tumizi kwa Usanidi wa Operesheni za Faksi na Kutuma Faksi (FAX Utility)" kwenye ukurasa wa 259*

  *"Programu-tumizi ya Kutuma Faksi (Kiendeshi cha PC-FAX)" kwenye ukurasa wa 260*

- *Iwapo Matumizi ya FAX haijasakinishwa, sakinisha FAX Utility kwa kutumia EPSON Software Updater (programu tumizi kwa kusasisha programu).*

***Muhimu:***

- *Ili kupokea faksi kwenye kompyuta, lazima **Hali ya Kupokea** kwenye paneli dhibiti ya kichapishi iwekwe kwa **Otomatiki**. Wasiliana na msimamizi wako kwa maelezo kuhusu hali ya mipangilio ya kichapishi. Ili kuunda mipangilio kwenye paneli ya udhibiti ya kichapishi, teua **Mipangilio** > **Mipangilio ya Jumla** > **Mipangilio ya Faksi** > **Mipangilio Msingi** > **Hali ya Kupokea**.*
- *Kompyuta iliyowekwa kupokea faksi inafaa kuwashwa kila mara. Nyaraka zilizopokewa zinahifadhiwa kwa muda kwenye kumbukumbu ya kichapishi kabla ya nyaraka zilizohifadhiwa kwenye kompyuta. Ukizima kompyuta, huenda kumbukumbu ya kichapishi ikajaa kwa kuwa haiwezi kutuma nyaraka kwenye kompyuta.*
- *Idadi ya nyaraka ambazo zimehifadhiwa kwa muda katika kumbukumbu ya kichapishi huonyeshwa kwenye kwenye paneli dhibiti ya kichapishi.*
- *Ili kusoma faksi zilizopokewa, unahitaji kusakinisha kionyeshaji cha PDF kama vile Adobe Reader kwenye kompyuta.*

**Maelezo Husika**

➡ "Kupokea Faksi kwenye Kompyuta" kwenye ukurasa wa 107

## Kuangalia Faksi Mpya (Windows)

Kwa kusanidi kompyuta ili kuhifadhi faksi zilizopokewa na kichapishi, unaweza kuangalia hali ya uchakataji ya faksi zilizopokewa, na iwapo kuna faksi zozote mpya au la kwa kutumia ikoni ya fakdsi kwenye mwambaa wa kazi wa Windows. Kwa kusanidi kompyuta ya kuonyesha taarifa wakati faksi mpya zinapokewa, skrini ya taarifa hutokea karibu na trei ya mfumo wa Windows, na unaweza kuangalia faksi mpya.

***Kumbuka:***

- *Data ya faksi iliyopokewa iliyohifadhiwa kwenye kompyuta inaondolewa kutoka kwenye kumbukumbu ya kichapishi.*
- *Unahitaji Adobe Reader ili kutazama faksi zilizopokewa ambazo zilihifadhiwa kama faili za PDF.*

### Kutumia Ikoni ya Faksi kwenye Mwambaa wa Kazi wa (Windows)

Unaweza kuangalia faksi mpya na hali ya operesheni kwa kutumia ikoni ya faksi iliyoonyeshwa kwenye mwambaa wa kazi wa Windows.

1. Angalia ikoni.
   - : kukaa ange.
   - : kuangalia faksi mpya.
   - : kuleta faksi mpya kumekamilika.

2. Bofya kulia kwenye ikoni, na kisha ubofye **View Receiving Fax Record**.

   Skrini ya **Receiving Fax Record** inaonyeshwa.

3. Angalia tarehe na mtumaji kwenye orodha, na kisha ufungue faili ya PDF.

   ***Kumbuka:***
   - *Faksi zilizopokewa zinabadilishwa jina kiotomatiki kwa kutumia umbizo lifuatalo la utoaji majina.*

     *YYYYMMDDHHMMSS_xxxxxxxxxx_nnnnn (Mwaka/Mwezi/Siku/Saa/Dakika/Sekunde_nambari ya mtumaji)*
   - *Pia unaweza kufungua kabrasha la faksi iliyopokewa moja kwa moja unapobofya ikoni ya kulia. Kwa maelezo, tazama* ***Optional Settings*** *kwenye msaada wa FAX Utility (yanayoonyeshwa kwenye dirisha kuu).*

Wakati ikoni ya faski huonyesha kuwa inakaa ange, unaweza kuangalia faksi mpya papo hapo kwa kuteua **Check new faxes now**.

### Kutumia Dirisha la Taarifa (Windows)

Unapoweka ili kukuarifu kuwepo kwa faksi mpya, dirisha la taarifa linaonyeshwa karibu na mwambaa wa kazi kwa kila faksi.

1. Angalia skrini ya taarifa inayoonyeshwa kwenye skrini yako ya kompyuta.

   ***Kumbuka:***
   *Skrini ya taarifa hutoweka iwapo hakuna operesheni inayotekelezwa kwa kipindi fulani cha muda. Unaweza kubadilisha mipangilio ya taarifa kama vile muda wa onyesho.*

2. Bofya mahali popote kwenye skrini ya taarifa, isipokuwa kwa kitufe cha .

   Skrini ya **Receiving Fax Record** inaonyeshwa.

3. Angalia tarehe na mtumaji kwenye orodha, na kisha ufungue faili ya PDF.

   ***Kumbuka:***
   - *Faksi zilizopokewa zinabadilishwa jina kiotomatiki kwa kutumia umbizo lifuatalo la utoaji majina.*

     *YYYYMMDDHHMMSS_xxxxxxxxxx_nnnnn (Mwaka/Mwezi/Siku/Saa/Dakika/Sekunde_nambari ya mtumaji)*
   - *Pia unaweza kufungua kabrasha la faksi iliyopokewa moja kwa moja unapobofya ikoni ya kulia. Kwa maelezo, tazama* ***Optional Settings*** *kwenye msaada wa FAX Utility (yanayoonyeshwa kwenye dirisha kuu).*

## Kuangalia Faksi Mpya (Mac OS)

Unaweza kuangalia faksi mpya kwa kutumia mbinu zifuatazo. Hii inapatikana tu kwenye kompyuta zilizowekwa kwa **"Save" (save faxes on this computer)**.

- Fungua kabrasha ya faksi iliyopokewa (imebainishwa kwenye **Received Fax Output Settings.**)
- Fungua Fax Receive Monitor na ubofye **Check new faxes now**.
- Taarifa ambayo faksi mpya zimepokewa

  Teua **Notify me of new faxes via a dock icon** kwenye **Fax Receive Monitor** > **Preferences** katika Matumizi ya FAKSI, ikoni ya monita ya kupokea faksi kwenye Egesho huruka ili kukuarifu kuwa faksi mpya zimefika.

## Fungua Kabrasha la Faski Iliyopokerwa kutoka kwenye Kifuatiliaji cha Faksi Iliyopokewa (Mac OS)

Unaweza kufungua kabrasha la kuhifadhi kutoka kwenye kompyuta iliyobainishwa ili kupokea faksi unapoteua **"Save" (save faxes on this computer)**.

1. Bofya ikoni ya ufuatiliaji wa faksi iliyopokewa kwenye Dock ili kufungua **Fax Receive Monitor**.

2. Teua kichapishi na ubofye **Open folder**, au bofya mara mbili jina la kichapishi.

3. Angalia tarehe na mtumaji kwenye jina la faili, na kisha ufungue faili ya PDF.

   ***Kumbuka:***
   *Faksi zilizopokewa zinabadilishwa jina kiotomatiki kwa kutumia umbizo lifuatalo la utoaji majina.*

   *YYYYMMDDHHMMSS_xxxxxxxxxx_nnnnn (Mwaka/Mwezi/Siku/Saa/Dakika/Sekunde_nambari ya mtumaji)*

   *Maelezo yaliyotumwa kutoka kwa mtumaji yanaonyeshwa kama nambari ya mtumaji. Huendanambari hii isionyeshwe kulingana na mtumaji.*

# Kukatisha Kipengele Kinachohifadhi Faksi Zinazoingia kwenye Kompyuta

Unaweza kukatisha kuhifadhi faksi kwenye kompyuta kwa kutumia FAX Utility.

Kwa maelezo, tazama Basic Operations kwenye msaada wa FAX Utility (yanayoonyeshwa kwenye dirisha kuu).

***Kumbuka:***
- *Iwapo kuna faksi zozote ambazo zimehifadhiwa kwenye kompyuta, huwezi kukatisha kipengele kinachohifadhi faksi kwenye kompyuta.*
- *Pia unaweza kubadilisha mipangilio kwenye kichapishi. Wasiliana na msimamizi wako kwa maelezo kwenye mipangiio ya ukatishaji ili kuhifadhi faksi kwenye kompyuta.*

### Maelezo Husika

➡ "Kufanya Mpangilo wa Hifadhi kwenye Kompyuta Kutopokea Faksi" kwenye ukurasa wa 306

# Kukarabati Kichapishi


Kuangalia Hali ya Vitumika. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 112

Kusafisha Kijia cha Karatasi kwa Matatizo ya Kuingiza Karatasi. . . . . . . . . . . . . . . . 112

Kuboresha Ubora wa Uchapishaji, Kunakili, Kutambaza, na Faksi. . . . . . . . . . . . . . 115

Kusafisha Kichapishi. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 126

Kusafisha Wino Uliomwagika. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 127

Kukagua Idadi Kamili ya Kurasa Zilizoingizwa Kwenye Kichapishi. . . . . . . . . . . . . .127

Kuhifadhi Nishati. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 128

Kusakinisha au Kuondoa Programu Kando. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .128

Kusafirisha na Kuhifadhi Kichapishi. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .134

# Kuangalia Hali ya Vitumika

Unaweza kuangalia takriban ya maisha ya huduma ya kikasha cha matengenezo kutoka kwenye paneli dhibiti ya kichapishi. Teua  kwenye skrini ya nyumbani.

Ili uhakikishe wino unaobakia, angalia viwango vya wino katika matangi yote ya printa.

**Muhimu:**

*Kuendelea kutumia printa kwa muda mrefu wakati kiwango cha wino kiko chini ya laini ya chini kunaweza kuharibu printa.*



***Kumbuka:***
*Pia unaweza kuangalia makadirio ya viwango vya wino na makadirio ya maisha ya huduma ya kisanduku cha matengenezo kutoka kwenye kiwambo cha hali kwewnye kiendeshi cha kichapishi.*

- *Windows*

  *Bofya **EPSON Status Monitor 3** kwenye kichupo cha **Utunzaji**.*

  *Ikiwa **EPSON Status Monitor 3** imelemazwa, bofya **Mipangilio Iliyorefushwa** kwenye kichupo cha **Utunzaji**, na kisha uteue **Wezesha EPSON Status Monitor 3**.*

- *Mac OS*

  *Apple menyu > **Mapendeleo ya Mfumo** > **Vichapishaji na Vitambazaji** (au **Chapisha na Utambaze**, **Chapisha na Utume Faksi**) > Epson(XXXX) > **Chaguo na Usambazaji** > **Matumizi** > **Fungua Matumizi ya Kichapishaji** > **EPSON Status Monitor***

**Maelezo Husika**

➡ "Kujaza Matangi ya Wino Upya" kwenye ukurasa wa 198

➡ "Kubadilisha Kisanduku cha Ukarabati" kwenye ukurasa wa 204

# Kusafisha Kijia cha Karatasi kwa Matatizo ya Kuingiza Karatasi

Wakati karatasi halijaingizwa kutoka kwenye mkanda wa karatasi sahihi, safisha rola iliyo ndani.

1. Zima kichapishi kwa kubonyeza kitufe cha ⏻.

2. Chomoa waya ya nishati, na kisha ukate muunganisho wa waya ya nishati.

3. Funga kifuniko cha waraka iwako kiko wazi.

4. Fungua kitengo cha kitambazaji kwa mikono miwili hadi kijifunge.



5. Hakikisha kuwa kifuniko cha tanki la wino kimefungwa salama.



> **Muhimu:**
> *Iwapo kifuniko cha tanki la wino hakijafungwa salama, wino unaweza kuvuja.*

6. Funga kitengo cha kitambazaji.



***Kumbuka:***
*Kitengo cha kitambazaji kimeundwa ili kufunga taratibu na kukataa kidogo kama kuzuia vidole vyako kukamatwa. Endelea kufunga hata ikiwa unahisi inakataa kidogo.*

7. Telezesha nje mkanda wa karatasi, na kisha uondoe karatasi.



8. Simamisha kichapishi kwa upande wake huku tanki la wino la kichapishi likiwa upande wa chini.



> **Tahadhari:**
> *Chunga mkono au vidole vyako visikwame unaposimamisha kichapishi. La sivyo unaweza kujeruhiwa.*

> **Muhimu:**
> *Usiruhusu kichapishi kisimame kwa muda mrefu.*

9. Ingiza kitambaa laini nyevunyevu, kisugue vizuri, na kisha upanguse rola unapoizungusha kwa kitambaa.



10. Rudisha kichapishi katika eneo lake la kawaida, na kisha uchomeke kaseti ya karatasi.

11. Unganisha waya ya nishati.

# Kuboresha Ubora wa Uchapishaji, Kunakili, Kutambaza, na Faksi

## Kukagua na Kusafisha Kichwa cha Kuchapisha

Ikiwa nozeli zimeziba, uchapishaji unakuwa fifu, mistati inaonekana, au rangi zisizotarajiwa zinaonekana. Ikiwa nozeli zimeziba sana, karatasi tupu itachapishwa. Wakati ubora wa chapisho umepungua, kwanza tumia kipengele cha kukagua nozeli na ukague kama nozeli zimeziba. Ikiwa nozeli zimeziba, safisha kichwa cha kuchapisha.

> **Muhimu:**
> - *Usifungue kitengo cha kitambazo au kuzima printa wakati wa usafishaji wa kichwa. Ikiwa usafisha wa kichwa haujakamilika, huenda usiweze kuchapisha.*
> - *Kusafisha kichwa hutumia wino mwingi na unapaswa kufanywa ikiwa ni muhimu tu.*
> - *Wakati wino ni kidogo, huenda usiweze kusafisha kichwa cha kuchapisha.*
> - *Ikiwa ubora wa chapisho haujaimarika baada ya kurudia kuangalia nozeli na kusafisha kichwa mara 3, subiri kwa angalau saa 12 bila kuchapisha kisha uangalie nozeli tena na urudie usafishaji wa kichwa ikiwa ni muhimu. Tunapendekeza uzime kichapishi kwa kutumia kitufe cha ⏻. Ikiwa ubora wa uchapishaji bado haujaimarika, endesha Usafishaji wa Nishati.*
> - *Ili kuzuia kichwa cha kuchapisha kisikaue, usichomoe printa wakati nishati imewashwa.*

1. Teua **Matengenezo** kwenye paneli dhibiti ya kichapishi.

2. Teua **Ukgz Nozeli ya Kichwa Chapa**.

3. Fuata maelekezo yaliyo kwenye skrini ili kupakia karatasi na kuchapisha ruwaza ya kukagua nozeli.

4. Angalia ruwaza iliyochapishwa ili kuona iwapo nozeli za kichwa cha kuchapisha zimezibika.




- A:

  Mistari yote imechapishwa. Teua . Hakuna hatua za ziada zinazohitajika.

- B au karibu na B

  Baaadhi ya nozeli zimeziba. Teua , na kisha ufuate maagizo kwenye skrini ili kusafisha kichwa cha chapisho.

  Usafishaji unapokamilika, ruwaza ya ukaguaji nozeli inachapishwa kiotomatiki.

- C au karibu na C

  Iiwa laini nyingi hazipo au hazijachapishwa, hii inaonyesha kwamba nozeli nyingi zimeziba. Teua  ili kutoka kwenye kipengele cha kukagua nozeli, na kisha uendeshe Usafishaji wa Nishati. Kwa maelezo, tazama “Maelezo husiani” hapa chini.

5. Rudia usafishaji na uchapishaji hadi mistari yote ichapishwe kabisa.

***Muhimu:***

*Ikiwa ubora wa chapisho haujaimarika baada ya kurudia kuangalia nozeli na kusafisha kichwa mara 3, subiri kwa angalau saa 12 bila kuchapisha kisha uangalie nozeli tena na urudie usafishaji wa kichwa ikiwa ni muhimu.*

*Tunapendekeza uzime kichapishi kwa kutumia kitufe cha . Ikiwa ubora wa uchapishaji bado haujaimarika, endesha Usafishaji wa Nishati.*

***Kumbuka:***

*Unaweza kuangalia na kusafisha kichwa cha kuchapisha kutoka kwenye kiendeshi cha kichapishi.*

- *Windows*

  *Bofya **Ukaguzi wa Nozeli ya Kichwa cha Kuchapisha** kwenye kichupo cha **Utunzaji**.*

- *Mac OS*

  *Apple menyu > **Mapendeleo ya Mfumo** > **Vichapishaji na Vitambazaji** (au **Chapisha na Utambaze**, **Chapisha na Utume Faksi**) > Epson(XXXX) > **Chaguo na Usambazaji** > **Matumizi** > **Fungua Matumizi ya Kichapishaji** > **Ukaguzi wa Nozeli ya Kichwa cha Kuchapisha***

**Maelezo Husika**

➡ "Kuendesha Usafishaji wa Nishati" kwenye ukurasa wa 117

## Kuendesha Usafishaji wa Nishati

Huduma ya **Usafishaji wa Nishati** hukuwezesha kubadilisha wino wote ulio ndani ya tubu za wino. Katika hali zifuatazo, unaweza kuihitaji kutumia kipengele hiki ili kuboresha ubora wa chapisho.

- ❏ Ulichapisha au kutekeleza usafishaji wa kichwa wakati viwango vya wino vilikuwa chini ili kuonekana kwenye madirisha ya tanki za wino.
- ❏ Ulipofanya ukaguaji nozeli na usafishaji wa kichwa mara 3 na kisha ukasubiri angalau saa 12 bila kuchapisha, lakini bado ubora wa chapisho haukuimarika.

Kabla ya kuendesha kipengele hiki, soma maagizo yafuatayo.

> ***Muhimu:***
>
> *Hakikisha kuwa kuna wino wa kutosha kwenye tanki za wino.*
>
> *Hakikisha kuwa tanki zote zina angalau theluthi moja ya wino.Viwango vya chini vya wino wakati wa Usafishaji wa Nishati vinaweza kuharibu bidhaa.*

> ***Muhimu:***
>
> *Kipindi cha saa 12 kinahitajika kati ya kila Usafishaji wa Nishati.*
>
> *Kwa kawida, Usafishaji wa Nishati moja inafaa kutatua suala la ubora wa kuchapisha ndani ya saa 12.Kwa hivyo, ili kuzuia matumizi yasiyofaa ya wino, unafaa kusubiri hadi saa 12 kabla ujaribu tena.*

> ***Muhimu:***
>
> *Kubadilisha kisanduku cha matengenezo kunaweza kuhitajika.*
>
> *Wino utawekwa kwenye kisanduku cha matengenezo.Iwapo kitajaa, lazima utayarishe na kusakinisha kisanduku cha matengenezo ili kuendelea kuchapisha.*

***Kumbuka:***
*Wakati viwango vya wino au nafasi huru kwenye kisanduku cha matengenezo vinatosha Usafishaji wa Nishati, huwezi kuendesha kipengele hiki.Hata katika hali hii, viwango na nafasi huru ya kuchapisha inaweza kusalia.*

1. Teua **Matengenezo** kwenye paneli dhibiti ya kichapishi.

2. Teua **Usafishaji wa Nishati**.

3. Fuata maagizo yaliyo kwenye skrini ili kuendesha kipengele cha Usafishaji wa Nishati.

   ***Kumbuka:***
   *Iwapo huwezi kuendesha kipengele hiki, tatua matatizo yanayoonyeshwa kwenye skrini. Pili, fuata utaratibu kutoka hatua ya 1 ili kuendesha kipengele hiki tena.*

4. Baada ya kuendesha kipengele hiki, endesha ukaguaji nozeli ili kuhakikisha nozeli hazijaziba.

   Kwa maelezo kuhusu jinsi ya kuendesha ukaguzi wa nozeli, tazama maelezo husiani hapa chini.

> ***Muhimu:***
>
> *Ikiwa ubora wa chapisho haujaimarika baada ya kuendesha Usafishaji wa Nishati, subiri kwa angalau saa 12 bila kuchapisha kisha uchapishe ruwaza ya uangaliaji nozeli tena. Endesha Usafishaji Kichwa cha Chapa au Usafishaji wa Nishati tena kwa kutegemea ruwaza iliyochapishwa. Ikiwa ubora bado hajuaimarika, wasiliana na timu ya usaidizi ya Epson.*

***Kumbuka:***
*Pia unaweza kuendesha usafishaji wa nishati kutoka kwenye kiendeshi cha kichapishi.*

- *Windows*

  *Bofya **Usafishaji wa Nishati** kwenye kichupo cha **Utunzaji**.*

- *Mac OS*

  *Apple menyu > **Mapendeleo ya Mfumo** > **Vichapishaji na Vitambazaji** (au **Chapisha na Utambaze**, **Chapisha na Utume Faksi**) > Epson(XXXX) > **Chaguo na Usambazaji** > **Matumizi** > **Fungua Matumizi ya Kichapishaji** > **Usafishaji wa Nishati***

**Maelezo Husika**

➡ "Kukagua na Kusafisha Kichwa cha Kuchapisha" kwenye ukurasa wa 115

## Kuzuia kuziba kwa nozeli

Kila mara tumia kitufe cha nishati unapowasha na kuzima kichapishi.

Hakikisha kuwa taa ya nishati imezimwa kabla utenganisahe kamba ya nishati.

Wino wenyewe unaweza kukauka iwapo haujafunikwa. Kama tu kuweka kifuniko kwenye kalamu ya wino au kalamu ya mafuta ili kuizuia kukauka, hakikisha kichwa cha kuchapisha kimefunikwa vilivyo ili kuzuia wino kukauka.

Wakati kamba ya nishati imechomolewa au tatizo la nishati litokee wakati kichapishi kinaendeshwa, kichwa cha kuchapisha huenda kisifunikwe vilivyo. Iwapo kichwa cha kuchapisha kinasalia vivyo hivyo, kitakauka huku kikisababisha kuzibika kwa nozeli (sehemu za kutoa wino).

Katika hali hizi, washa na uzime kichapishi tena haraka iwezekanavyo ili kufunika kichwa cha kuchapisha.

## Kulinganisha Kichwa cha Kuchapisha

Ukiona kutolingana kwa mistari wima au picha zenye ukungu, linganisha kichwa cha kuchapisha.

1. Teua **Matengenezo** kwenye paneli dhibiti ya kichapishi.
2. Teua **Ulainishaji Kichwa**.
3. Teua mojawapo ya menyu za kupangilia.
   - Mistari wima itaonekana kutopangiliwa vizuri au iwapo machapisho yako hayaonekani vizuri: teua **Ulainishaji Wima**.
   - Mstari wa mlalo hutokea katika viwango vya mara kwa mara: teua **Upangiliaji Kimlalo**.
4. Fuata maelekezo yaliyo kwenye skrini ili kupakia na kuchapisha ruwaza ya mpangilio.

## Kusafisha Kijia cha Karatasi na Umwagikaji wa Wino

Wakati uchapishaji una uchafu au kuchakaa, safisha kibiringizaji kiicho ndani.

1. Teua **Matengenezo** kwenye paneli dhibiti ya kichapishi.

2. Teua **Usfshaji Mwongzo wa Krtasi**.

3. Fuata maelekezo yaliyo kwenye skrini ili kupakia karatasi na kusafisha njia ya karatasi.

4. Rudia utaratibu huu hadi karatasi iwache kuchafuliwa na wino.

5. Wakati tatizo haliwezi kuondolewa baada ya kusafisha njia ya karatasi, sehemu iliyo ndani ya kichapishi ambayo imeonyeshwa kwenye kielelezo inalainishwa. Zima kichapishi, na kisha upanguse wino kwa kutumia pamba.



**Muhimu:**

- *Usitumie karatasi ya shashi kusafisha ndani ya kichapishi. Nozeli za kichwa cha kushapisha zinaweza kuzibwa na nyuzi za pamba.*
- *Usiguze kebo nyeupe bapa, sehemu angavu, na tyubu za wino zilizo ndani ya kichapishi. Ukifanya hivyo unaweza kusababisha hitalifu.*



## Kusafisha Glasi ya Kichanganuzi

Wakati nakala au taswira zilizotambazwa ni chafu au zimachakaa, safisha glasi ya kichanganuzi.

> ***Tahadhari:***
> *Chunga usijibane mkono au vidole wakati unafungua au kufunga kifuniko cha hati. La sivyo unaweza kujeruhiwa.*

> ***Muhimu:***
> *Usiwahi kutumia pombe au thina kusafisha printa. Kemikali hizi zinaweza kuharibu printa.*

1. Fungua kifuniko cha hati.



2. Tumia kitambaa laini, safi na kikavu kusafisha glasi ya kichanganuzi.

> ***Muhimu:***
> - *Iwapo eneo la kioo limekwamiliwa na grisi au nyenzo nyingine ngumu kuondoa, tumia kiasi kidogo cha kisafishaji kioo na kitambaa laini kuiondoa. Pangusa unyevu wote unaobakia.*
> - *Usibonyeze glasi kwa nguvu.*
> - *Kuwa makini usikwaruze au kuharibu glasi. Glasi iliyoharibika inaweza kupunguza ubora wa utambazaji.*

## Kusafisha ADF

Wakati picha zilizonakiliwa au kutambazwa kutoka kwa ADF zimechafuka au za kwanza haziingii katka ADF ipasavyo, safisha ADF.

> ***Muhimu:***
> *Usiwahi kutumia pombe au thina kusafisha printa. Kemikali hizi zinaweza kuharibu printa.*

1. Fungua jalada la ADF.



2. Tumia kitambaa safi kilicho na maji kusafisha rola na ndani ya ADF.



> ***Muhimu:***
> *Kutumia kitambaa kilichokauka kunawea kuharibu eneo la rola. Tumia ADF baada ya rola kukauka.*

3. Funga jalada la ADF, na kisha fungua kifuniko cha waraka.



4. Safisha sehemu ambayo imeonyeshwa katika kielelezo.



> **Muhimu:**
>
> - *Iwapo eneo la kioo limekwamiliwa na grisi au nyenzo nyingine ngumu kuondoa, tumia kiasi kidogo cha kisafishaji kioo na kitambaa laini kuiondoa. Pangusa unyevu wote unaobakia.*
> - *Usibonyeze glasi kwa nguvu.*
> - *Kuwa makini usikwaruze au kuharibu glasi. Glasi iliyoharibika inaweza kupunguza ubora wa utambazaji.*

5. Iwapo tatizo haliwezi kuondolewa, zima kichapishi kwa kubonyeza kitufe cha ⏻, fungua jalada la ADF, na kisha uinue trei ingizo ya ADF.



6. Safisha sehemu ambayo imeonyeshwa katika kielelezo.



## Kusafisha Filamu Angavu

Wakati chapisho halijaboreshwa baadaya kulinganisha kichwa cha kuchapisha au kusafisha njia ya karatasi, filamu angavu iliyo ndani ya kichapishi inachafuka.

Vipengee vinavyohitajika:

❏ Pamba (nyingi)

❏ Maji yaliyo na sabuni kidfogo (matone 2 hadi 3 kwenye kikumbe 1/4 cha maji ya mfereji)

❏ Mwangaza wa kuangalia uchafu

> ***Muhimu:***
> *Usitumie kioevu chochote cha kusafisha kando na maji yaliyo na matone kiasi ya sabuni.*

1. Zima kichapishi kwa kubonyeza kitufe cha ⏻.

2. Funga kifuniko cha waraka iwako kiko wazi.

3. Fungua kitengo cha kitambazaji kwa mikono miwili hadi kijifunge.



4. Angalia iwapo utepe nzito imechafuka. Ni rahisi kuona uchafu iwapo unatumia mwangaza.

   Iwapo kuna uchafu (kama vile alama za vidoile au grisi) kwenye filamu angavu (A), nenda kwenye hatua inayofduata.




A: filamu angavu

B: reli

> **Muhimu:**
>
> *Tahadhari usiguse reli (B). Vinginevyo, huenda usiweze kuchapisha. Usipanguse grisi kwenye reli, kwa sababu inahitajika kwa operesheni.*

5. Weka maji kwenye pamba pamoja na matone kiasi ya sababu ili maji yasiwe mengi zaidi, na kisha pangusa sehemu iliyochafuka.



> **Muhimu:**
>
> *Pangusa uchafu polepole. Iwapo utafinyilia zaidi pamba kwenye filamu, springi za filamu zinaweza kuondolewa katika nafasi yake na kichapishi kinaweza kuharibika.*

6. Tumia pamba kavu ili kupangusa filamu.

> **Muhimu:**
>
> *Usiache nyuzi zozote kwenye filamu.*

***Kumbuka:***
*Ili kuzuia kuenea kwa uchafu, badilisha pamba kila mara kwa nyingine mpya.*

7. Rudia hatua ya 5 na 6 hadi filamu iwe safi.

8. Hakikisha kuwa filamu haina ucxhafu.

9. Funga kitengo cha kitambazaji.



***Kumbuka:***
*Kitengo cha kitambazaji kimeundwa ili kufunga taratibu na kukataa kidogo kama kuzuia vidole vyako kukamatwa. Endelea kufunga hata ikiwa unahisi inakataa kidogo.*

# Kusafisha Kichapishi

Iwapo vijenzi na kesi ni chafu au ina vumbi, zima kichapishi na uvisafishe kwa kutumia kitambaa safi laini ambacho kimeloweshwa kwa maji. Iwapo huwezi kuondoa uchafu, jaribu kuongeza kiwango kidogo cha sabuni kwa kitambaa chenye unyevu.



**Muhimu:**

- *Kuwa makini ili usimwage maji ndani ya mtambo wa kichapishi au viambajengo vyake vya kielektroniki. La sivyo, kichapishi kinaweza kuharikibika.*
- *Usitumia pombe au kiyeyusha rangi kusafisha vijenzi na kifuniko. Kemikali hizi zinaweza kuziharibu.*
- *Usiguse sehemu zinazoonyeshwa kwenye mfano. Ukifanya hivyo unaweza kusababisha hitalifu.*



# Kusafisha Wino Uliomwagika

Iwapo wino umemwagika, usafishe kwa njia zifuatazo.

- Iwapo wino utamwagika katika eneo lililo karibu na tangi, pangusa kwa kutumia kitambaa safi laini au pamba.
- Iwapo wino utamwagika kwenye dawati au sakafuni, upanguse mara moja. Wino unapokauka, itakuwa vigumu kuuondoa. Ili kuzuia ueneaji wa wino, weka kitambaa kwenye wino, na kisha uupanguse kwa kitambaa cha unyenunyevu.
- Iwapo wino utajipaka kwenye mikono yako, nawa kwa maji na sabuni.

# Kukagua Idadi Kamili ya Kurasa Zilizoingizwa Kwenye Kichapishi

Unaweza kukagua idadi kamili ya kurasa zilizoingizwa kwenye printa. Maelezo yanachapishwa pamoja na ruwaza ya ukaguzi wa nozeli.

1. Teua **Matengenezo** kwenye paneli dhibiti ya kichapishi.

2. Teua **Ukgz Nozeli ya Kichwa Chapa**.

3. Fuata maelekezo yaliyo kwenye skrini ili kupakia karatasi na kuchapisha ruwaza ya kukagua nozeli.

***Kumbuka:***
*Pia unaweza kukagua idadi kamili ya kurasa zilizoingizwa kwenye kichapishi.*

- *Windows*

  *Bofya **Maelezo ya Printa na Chaguo** kwenye kichupo cha **Utunzaji**.*
- *Mac OS*

  *Apple menyu > **Mapendeleo ya Mfumo** > **Vichapishaji na Vitambazaji** (au **Chapisha na Utambaze**, **Chapisha na Utume Faksi**) > Epson(XXXX) > **Chaguo na Usambazaji** > **Matumizi** > **Fungua Matumizi ya Kichapishaji** > **Printer and Option Information***

# Kuhifadhi Nishati

Kichapishi kinaingia katika modi ya kulala au kujizima kiotomatiki ikiwa hakuna kazi zinafanywa kwa muda uliwekwa. Unaweza kurekebisha muda kabla ya udhibiti wa nishati kutekelezwa. Ongezeko lolote litaathiri ufanisi wa nishati ya bidhaa. Tafadhali zingatia mazingira kabla ya kufanya mabadiliko yoyote.

## Kuhifadhi Nishati — Paneli Dhibiti

1. Teua **Mipangilio** kwenye skrini ya nyumbani.

2. Teua **Mipangilio ya Jumla** > **Mipangilio Msingi**.

3. Fanya moja kati ya zifuatazo.

   ***Kumbuka:***
   *Huenda bidhaa yako ina kipengele cha **Mip'ilio ya Kuzima** au **Kipima Saa ya Kuzima** kulingana na eneo la ununuzi.*

   - Chagua **Kipima saa cha Kulala** au **Mip'ilio ya Kuzima** > **Zima Ikiwa Haitumiki** au **Zima ikiwa Imetenganishwa**, na kisha uweze mipangilio.
   - Chagua **Kipima saa cha Kulala** au **Kipima Saa ya Kuzima**, na kisha uweke mipangilio.

# Kusakinisha au Kuondoa Programu Kando

Unganisha kompyuta yako kwenye mtandao na usakinishe toleo jipya la programu kutoka kwenye tovuti. Ingia kwenye kompyuta yako kama msimamizi. Ingiza nywila ya msimamizi iwapo kompyuta itakuitisha.

## Kusakinisha Programu Kando

***Kumbuka:***
*Wakati unasakinisha upya programu, unahitaji kuisakinusha kwanza.*

1. Hakikisha kuwa kichapishi na kompyuta zinapatikana kwa mawasiliano, na kompyuta imeunganishwa kwenye Intaneti.

2. Anzisha EPSON Software Updater.

   Picha ya skrini ni mfano kwenye Windows.




3. Kwa Windows, teua kichapishi chako, kisha ubofye ili utafute programu za hivi punde zinazopatikana.

4. Teua vipengee unavyotaka kusakinisha au kusasisha, na kisha ubofye kitufe cha kusakinisha.

> ***Muhimu:***
>
> *Usizime au kuchomoa kichapishi hadi usasishaji ukamilike. Kufanya hivyo kunaweza kusababisha kichapishi kutofanya kazi.*

***Kumbuka:***

- *Unaweza kupakua programu-tumizi za sasa kutoka kwenye tovuti ya Epson.*

  *http://www.epson.com*

- *Iwapo unatumia mifumo ya uendeshaji ya Windows Server, huwezi kutumia Epson Software Updater. Pakua programu za hivi majuzi kutoka kwenye tovuti ya Epson.*

**Maelezo Husika**

➡ "Programu ya Kusasisha Programu na Vifaa Dhibiti (Epson Software Updater)" kwenye ukurasa wa 263

➡ "Sakinusha Programu" kwenye ukurasa wa 131

## Kuangalia ikiwa kiendeshi halali cha kichapishi cha Epson kimesakinishwa — Windows

Unaweza kuangalia iwapo kiendeshi halali cha kichapishi cha Epson kimesakinishwa kwenye kompyuta yako kwa kutumia mojawapo ya mbinu zifuatazo.

Teua **Paneli Dhibiti** > **Tazama vifaa na vichapishi** (**Vichapishi**, **Vichapishi na Faksi**), na kisha ufuate yafuatayo ili kufungua dirisha la sifa za seva ya kuchapisha.

- ❏ Windows Windows 10/Windows 8.1/Windows 8/Windows 7/Windows Server 2019/Windows Server 2016/ Windows Server 2012 R2/Windows Server 2012/Windows Server 2008 R2

  Bofya ikoni ya kichapishi, na kisha ubofye **Sifa za seva ya uchapishaji** katika upande wa juu wa dirisha.
- ❏ Windows Vista/Windows Server 2008

  Bofya kulia kwenye kabrasha la **Vichapishi**, na kisha ubofye **Endesha kama msimamizi** > **Sifa za Seva**.
- ❏ Windows XP/Windows Server 2003 R2/Windows Server 2003

  Kutoka kwenye menyu ya **Faili**, teua **Sifa za Seva**.

Bofya kichupo cha **Kiendeshi**. Iwapo jina la kichapishi chako litaonyeshwa kwenye orodha, kiendeshi halali cha Epson kimesakinishwa kwenye kompyuta yako.




### Maelezo Husika

➡ “Kusakinisha Programu Kando” kwenye ukurasa wa 128

## Kukagua ikiwa kiendeshi halali cha kichapishi cha Epson kimesakinishwa — Mac OS

Unaweza kuangalia iwapo kiendeshi halali cha kichapishi cha Epson kimesakinishwa kwenye kompyuta yako kwa kutumia mojawapo ya mbinu zifuatazo.

Teua **Mapendeleo ya Mfumo** kwenye menyu ya Apple > **Vichapishaji na Vitambazaji** (au **Chapisha na Utambaze**, **Chapisha na Utume Faksi**), kisha uteue kichapishaji. Bofya **Chaguo Vifaa**, na iwapo kichupo cha

**Chaguo** na kichupo cha **Huduma** vitaonyeshwa kwenye dirisha, kiendeshi halali cha kichapoishi cha Epson kimesakinishwa kwenye kompyuta yako.computer.




**Maelezo Husika**

➡ "Kusakinisha Programu Kando" kwenye ukurasa wa 128

## Kuongeza Kichapishi (kwa Mac OS tu)

1. Teua **Mapendeleo ya Mfumo** kutoka kwenye menyu ya Apple > **Vichapishi na Vitambazaji** (au **Chapisho na Tambazo**, **Chapisho na Faksi**).

2. Bofya +, na kisha uteue **Ongeza Kichapishi na Kitambazaji Kingine**.

3. Teua kichapishi chako, na kisha uteue kichapishi chako kutoka kwenye **Matumizi**.

4. Bofya **Ongeza**.

   ***Kumbuka:***
   *Iwapo kichapishi hakijaorodheshwa, thibitisha kuwa kimeunganishwa sahihi kwenye kompyuta na kuwa kichapishi kimewashwa.*

## Sakinusha Programu

Ingia kwenye kompyuta yako kama msimamizi. Ingiza nywila ya msimamizi iwapo kompyuta itakuitisha.

### Kusakinusha Programu — Windows

1. Bonyeza kitufe cha ⏻ ili uzime kichapishi.

2. Toka kwa programu-tumizi zote zinazoendeshwa.

3. Fungua **Paneli Dhibiti**:
   - Windows 10/Windows Server 2019/Windows Server 2016

     Bofya kitufe cha kuwasha, na kisha uteue **Mfumo wa Windows** > **Paneli Dhibiti**.
   - Windows 8.1/Windows 8/Windows Server 2012 R2/Windows Server 2012

     Teua **Eneo kazi** > **Mipangilio** > **Paneli Dhibiti**.
   - Windows 7/Windows Vista/Windows XP/Windows Server 2008 R2/Windows Server 2008/Windows Server 2003 R2/Windows Server 2003

     Bofya kitufe cha kuwasha na uteue **Paneli Dhibiti**.

4. Fungua **Sakinusha programu** (au **Ongeza au Ondoa Programu**):
   - Windows 10/Windows 8.1/Windows 8/Windows 7/Windows Vista/Windows Server 2019/Windows Server 2016/Windows Server 2012 R2/Windows Server 2012/Windows Server 2008 R2/Windows Server 2008

     Chagua **Sakinusha programu** katika **Programu**.
   - Windows XP/Windows Server 2003 R2/Windows Server 2003

     Bofya **Ongeza au Ondoa Programu**.

5. Teua programu unayotaka kusakinusha.

   Huwezi kusakinusha kiendeshi cha kichapishi iwapo kuna kazi zozote za kuchapisha. Futa au subiri kuchapisha kazi kabla ya kusakinusha.

6. Sakinusha programu:
   - Windows 10/Windows 8.1/Windows 8/Windows 7/Windows Vista/Windows Server 2019/Windows Server 2016/Windows Server 2012 R2/Windows Server 2012/Windows Server 2008 R2/Windows Server 2008

     Bofya **Sakinusha/Badilisha** au **Sakinusha**.
   - Windows XP/Windows Server 2003 R2/Windows Server 2003

     Bofya **Badilisha/Ondoa** au **Ondoa**.

   ***Kumbuka:***
   *Ikiwa dirisha la **Udhibiti wa Akaunti ya Mtumiaji** linaonekana, bofya **Endelea**.*

7. Fuata maagizo ya kwenye skrini.

## Kusakinusha Programu — Mac OS

1. Pakua Uninstaller ukitumia EPSON Software Updater.

   Ukishapakua Uninstaller, huhitaji kuipakua tena kila wakati unasakinusha programu.

2. Bonyeza kitufe cha ⏻ ili uzime kichapishi.

3. Ili usakinishe kiendeshi cha printa au kiendeshi cha PC-FAX, chagua **Mapendeleo ya Mfumo** katika Apple menyu > **Printa & Vitambazo** (au **Chapisha & Tambaza**, **Chapisha & Tuma Faksi**), na kisha uondoe printa kutoka kwa orodha ya printa zilizowezeshwa.

4. Toka kwa programu-tumizi zote zinazoendeshwa.

5. Teua **Nenda** > **Programu** > **Epson Software** > **Uninstaller**.

6. Chagua programu unayotaka kusakinusha, na kisha ubofye **Uninstall**.

> ***Muhimu:***
> *Uninstaller huondoa viendeshi vyote vya printa za jeti ya wino za Epson kutoka kwa kompyuta. Ukitumia printa nyingi za jeti ya wino za Epson na unataka kufuta baadhi ya viendeshi peke yake, futa zote kwanza, na kisha usakinishe kiendeshi cha printa unachotaka tena.*

***Kumbuka:***
*Ikiwa huwezi kupata programu unayotaka kusakinusha katika orodha ya programu, huwezi kusakinusha ukitumia Uninstaller. Katika hali hii, chagua **Nenda** > **Programu** > **Epson Software**, chagua programu unayotaka kusakinusha, na kisha uikokote kwenye ikoni ya taka.*

#### Maelezo Husika

➡ "Programu ya Kusasisha Programu na Vifaa Dhibiti (Epson Software Updater)" kwenye ukurasa wa 263

## Kusasisha Programu na Ngome

Unaweza kutatua matatizo fulani na kuboresha au kuongeza dhima kwa kusasisha programu na ngome. Hakikisha unatumia toleo lipya la programu na ngome.

1. Hakikisha kwamba printa na kompyuta zimeunganishwa, na kompyuta imeunganishwa kwenye wavuti.

2. Anzisha EPSON Software Updater, na usasishe programu au ngome.

> ***Muhimu:***
> *Usizime au kuchomoa kichapishi hadi kisasisho kikamilike; vinginevyo, huenda kichapishi kisifanye kazi vilivyo.*

***Kumbuka:***
*Ikiwa huwezi kupata programu unayotaka kusasisha katika orodha, huwezi kusasisha ukitumia EPSON Software Updater. Tafuta metoleo mapya ya programu kutoka kwa tovuti yako ya Epson.*

*http://www.epson.com*

#### Maelezo Husika

➡ "Programu ya Kusasisha Programu na Vifaa Dhibiti (Epson Software Updater)" kwenye ukurasa wa 263

### Kusasisha Programu Dhibiti ya Kichapishi kwa Kutumia paneli Dhibiti

Iwapo kichapishi kimeunganishwa kwenye Mtandao, unaweza kusasisha programu dhibiti ya kichapishi kwa kutumia paneli dhibiti. Pia unaweza kuweka kichapishi katika ukaguzi wa kila mara kwa visasisho vya programu dhibiti na kukuarifu iwapo kuna vyovyote vinavyopatikana.

#### Maelezo Husika

➡ "Sasisho la Pro." kwenye ukurasa wa 277

# Kusafirisha na Kuhifadhi Kichapishi

Wakati unahitaji kuhifadhi kichapishi au kukihamisha au kwa ukarabati, fuata hatua zilizo hapa chini za kupakia kichapishi.

1. Zima kichapishi kwa kubonyeza kitufe cha ⏻.
2. Hakikisha taa ya nishati imezima, na kisha uchomoe waya ya nishati.

> ***Muhimu:***
> *Chomoa waya ya nishati wakati taa ya nishati imezimwa. La sivyo, kichwa cha kuchapisha hakitarudi kwenye mkao wake na wino utakauka, na huenda isiweze kuchapisha.*

3. Tenganisha kebo zote kama vile waya ya nishati na kebo ya USB.
4. Ondoa karatasi zote kutoka kwa kichapishi.
5. Hakikisha hakuna nakala za kwanza kwenye kichapishi.
6. Funga kifuniko cha waraka iwako kiko wazi.
7. Fungua kitengo cha kitambazaji kwa mikono miwili hadi kijifunge.



> ***Tahadhari:***
> *Chunga mkono au vidole vyako visikwame wakati unafungua au kufunga kitengo cha kitambazaji. La sivyo unaweza kujeruhiwa.*

8. Funga kichwa cha kuchapisha kwenye kesi ukitumia utepe.



9. Hakikisha umesakinisha kifuniko kilicho kwenye tangi la wino vizuri.



10. Funga kifuniko cha tanki la wino kwa usalama.



11. Funga kitengo cha kitambazaji.



***Kumbuka:***
*Kitengo cha kitambazaji kimeundwa ili kufunga taratibu na kukataa kidogo kama kuzuia vidole vyako kukamatwa. Endelea kufunga hata ikiwa unahisi inakataa kidogo.*

12. Andaa kupakua kichapishi kama inavyoonyeshwa hapa chini.



13. Weka kichapishi kwenye mkoba wa plastiki na uufunge.

14. Fuga printa kwenye sanduku lake kwa kutumia vifaa vya kukinga.



**!** ***Muhimu:***

- *Unapohifadhi kichapishi au kukisafirisha, weka kichapishi kwenye mkoba wa plastiki na uufunge. Epuka kuinamisha kichapishi, usikiweke wima, au kuigeuza upande wa chini kuangalia juu; la sivyo wino utavuja.*



- *Wakati wa kuhifadhi au kusafirisha chupa ya wino, usiinamishe chupa na usiigongeshe au kuiweka mahali penye mabadiliko ya hali joto.La sivyo, wino unaweza kuvuja hata kama kifuniko kilicho kwenye chupa ya wino kimekazwa vizuri.Hakikisha umeweka chupa ya wino ikiwa imesimama wakati unakaza kifuniko, na utahadhari ili uzuie wino usivuje wakati unasafirisha chupa, kwa mfano, kuweka chupa kwenye mkoba.*
- *Usiweke chupa za wino zilizofunguliwa ndani ya sanduku pamoja na printa.*



Wakati unatumia printa wakati mwingine, hakikisha unatoa utepe unaoshikilia kichwa cha kuchapisha. Ikiwa ubora wa uchapishaji utapungua wakati ujao utakaochapisha, safisha na ulinganishe kichwa cha kuchapisha.

**Maelezo Husika**

➡ "Kukagua na Kusafisha Kichwa cha Kuchapisha" kwenye ukurasa wa 115
➡ "Kulinganisha Kichwa cha Kuchapisha" kwenye ukurasa wa 118

# Kutatua Matatizo

Kichapishi Hakifanyi Kazi Inavyotarajiwa. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .139

Ujumbe unaonyeshwa kwenye Skrini ya LCD. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 190

Karatasi Zinakwama. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 192

Ni Wakati wa Kujaza tena Wino. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 197

Ni wakati wa Kubadilisha Kikasha cha Matengenezo. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .204

Ubora wa Kuchapisha, Kunakili na Kutambaza ni Duni. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .205

Haiwezi Kutatua Tatizo. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 226

# Kichapishi Hakifanyi Kazi Inavyotarajiwa

## Kichapishi Hakiwaki wala Kuzima

### Haiwaki

Sababu zifuatazo zinaweza kuzingatiwa.

#### Waya ya nishati haijaunganishwa ipasavyo kwenye lango la stima.

**Suluhisho**

Hakikisha kwamba waya ya nishati imeingizwa vizuri.

#### Kitufe cha ⏻ kwa muda mrefu ipasavyo.

**Suluhisho**

Shikilia kitufe cha ⏻ chini kwa muda mrefu zaidi kidogo.

### Haizimi

#### Kitufe cha ⏻ kwa muda mrefu ipasavyo.

**Suluhisho**

Shikilia kitufe cha ⏻ chini kwa muda mrefu zaidi kidogo. Ikiwa bado huwezi kuzima printa, chomoa waya ya nishati. Ili kuzuia kicha cha kuchapisha kizikauke, washa na uzime printa kwa kubonyeza kitufe cha ⏻.

### Nishati Huzima Kiotomatiki

#### Kipengele cha Mip'ilio ya Kuzima au Kipima Saa ya Kuzima kimewashwa.

**Suluhisho**

- Chagua **Mipangilio** > **Mipangilio ya Jumla** > **Mipangilio Msingi** > **Mip'ilio ya Kuzima**, na kisha ulemaze **Zima Ikiwa Haitumiki** na mipangilio ya **Zima ikiwa Imetenganishwa**.
- Teua **Mipangilio** > **Mipangilio ya Jumla** > **Mipangilio Msingi**, na kisha ulemaze Mpangilio wa **Kipima Saa ya Kuzima**.

***Kumbuka:***
*Huenda bidhaa yako ina kipengele cha **Mip'ilio ya Kuzima** au **Kipima Saa ya Kuzima** kulingana na eneo la ununuzi.*

# Karatasi Haitoi Mlisho Ipasavyo

## Hakuna Karatasi

Sababu zifuatazo zinaweza kuzingatiwa.

### Eneo la usakinishaji halifai.

**Suluhisho**

Weka printa kwenye eneo tambarare na uitumie katika hali ya mazingira iliyopendekezwa.

➡ "Sifa za Kimazingira" kwenye ukurasa wa 285

### Karatasi isiyokubaliwa inatumika.

**Suluhisho**

Tumia karatasi inayokubaliwa na hiki kichapishi.

➡ "Karatasi Inayopatikana na Uwezo" kwenye ukurasa wa 250
➡ "Aina Zisizopatikana za Karatasi" kwenye ukurasa wa 253

### Ushughulikiaji wa karatasi si sahihi.

**Suluhisho**

Fuata maagizo ya kushughilikia karatasi.

➡ "Tahadhari za Kushughulikia Karatasi" kwenye ukurasa wa 30

### Laha nyingi zimepakiwa kwenye kichapishi.

**Suluhisho**

Usiweke zaidi ya upeo wa idadi ya karatasi uliotajwa kwa karatasi.

➡ "Karatasi Inayopatikana na Uwezo" kwenye ukurasa wa 250

### Mipangilio ya karatasi kwenye kichapishi si sahihi.

**Suluhisho**

Hakikisha mipangilio ya ukubwa wa karatasi na aina ya karatasi inalingana na ukubwa halisi wa karatasi na aina ya karatasi iliyopakiwa kwenye kichapishi.

➡ "Mipangilio ya Ukubwa na Aina ya Karatasi" kwenye ukurasa wa 30

### Karatasi huteleza endapo vumbi ya karatasi inanata kwenye rola.

**Suluhisho**

Safisha rola.

➡ "Kusafisha Kijia cha Karatasi kwa Matatizo ya Kuingiza Karatasi" kwenye ukurasa wa 112

## Karatasi Huingia kama Imeinama

Sababu zifuatazo zinaweza kuzingatiwa.

### Eneo la usakinishaji halifai.

**Suluhisho**

Weka printa kwenye eneo tambarare na uitumie katika hali ya mazingira iliyopendekezwa.

➡ “Sifa za Kimazingira” kwenye ukurasa wa 285

### Karatasi isiyokubaliwa inatumika.

**Suluhisho**

Tumia karatasi inayokubaliwa na hiki kichapishi.

➡ “Karatasi Inayopatikana na Uwezo” kwenye ukurasa wa 250
➡ “Aina Zisizopatikana za Karatasi” kwenye ukurasa wa 253

### Ushughulikiaji wa karatasi si sahihi.

**Suluhisho**

Fuata maagizo ya kushughilikia karatasi.

➡ “Tahadhari za Kushughulikia Karatasi” kwenye ukurasa wa 30

### Karatasi imepakiwa visivyo.

**Suluhisho**

Weka karatasi ikiwa inaangalia upande unaofaa, na telezesha mwongozo wa kingo kando ya kingo ya karatasi.

➡ “Kuweka Karatasi” kwenye ukurasa wa 32

### Laha nyingi zimepakiwa kwenye kichapishi.

**Suluhisho**

Usiweke zaidi ya upeo wa idadi ya karatasi uliotajwa kwa karatasi.

➡ “Karatasi Inayopatikana na Uwezo” kwenye ukurasa wa 250

### Mipangilio ya karatasi kwenye kichapishi si sahihi.

**Suluhisho**

Hakikisha mipangilio ya ukubwa wa karatasi na aina ya karatasi inalingana na ukubwa halisi wa karatasi na aina ya karatasi iliyopakiwa kwenye kichapishi.

➡ “Mipangilio ya Ukubwa na Aina ya Karatasi” kwenye ukurasa wa 30

### Karatasi huteleza endapo vumbi ya karatasi inanata kwenye rola.

**Suluhisho**

Safisha rola.

➡ "Kusafisha Kijia cha Karatasi kwa Matatizo ya Kuingiza Karatasi" kwenye ukurasa wa 112

## Karatasi Kadhaa Kuwekwa Moja baada ya Nyingine

Sababu zifuatazo zinaweza kuzingatiwa.

### Eneo la usakinishaji halifai.

**Suluhisho**

Weka printa kwenye eneo tambarare na uitumie katika hali ya mazingira iliyopendekezwa.

➡ "Sifa za Kimazingira" kwenye ukurasa wa 285

### Karatasi isiyokubaliwa inatumika.

**Suluhisho**

Tumia karatasi inayokubaliwa na hiki kichapishi.

➡ "Karatasi Inayopatikana na Uwezo" kwenye ukurasa wa 250
➡ "Aina Zisizopatikana za Karatasi" kwenye ukurasa wa 253

### Ushughulikiaji wa karatasi si sahihi.

**Suluhisho**

Fuata maagizo ya kushughilikia karatasi.

➡ "Tahadhari za Kushughulikia Karatasi" kwenye ukurasa wa 30

### Karatasi ina unyevunyevu au ni chafu.

**Suluhisho**

Pakia karatasi mpya.

### Umeme wa mgusano unasababisha laha za karatasi kushikana.

**Suluhisho**

Pepeta karatasi kabla ya kupakia. Ikiwa karatasi haitalishwa, pakia karatasi moja baada ya nyingine.

### Laha nyingi zimepakiwa kwenye kichapishi.

**Suluhisho**

Usiweke zaidi ya upeo wa idadi ya karatasi uliotajwa kwa karatasi.

➡ "Karatasi Inayopatikana na Uwezo" kwenye ukurasa wa 250

### Mipangilio ya karatasi kwenye kichapishi si sahihi.

**Suluhisho**

Hakikisha mipangilio ya ukubwa wa karatasi na aina ya karatasi inalingana na ukubwa halisi wa karatasi na aina ya karatasi iliyopakiwa kwenye kichapishi.

➡ "Mipangilio ya Ukubwa na Aina ya Karatasi" kwenye ukurasa wa 30

### Karatasi huteleza endapo vumbi ya karatasi inanata kwenye rola.

**Suluhisho**

Safisha rola.

➡ "Kusafisha Kijia cha Karatasi kwa Matatizo ya Kuingiza Karatasi" kwenye ukurasa wa 112

### Laha nyingi za karatasi hulishwa kwa wakati mmoja watika wa uchapishaji wa pande 2 mwenyewe.

**Suluhisho**

Ondoa karatasi yoyote ambayo imepakiwa kwenye chanzo cha karatasi kabla ya kupakia karatasi tena.

## Karatasi Inatolewa Wakati wa Uchapishaji

### Letterhead haijateuliewa kama aina ya karatasi.

**Suluhisho**

Unapopakia karatasi ya kichwa cha barua (karatasi ambayo maelezo kama vile jina la mtumaji au jina la shirika yanachapishwa awali kwenye kijajuu), teua **Letterhead** kama mpangilio wa aina ya karatasi.

## Nakala Asili Haiingii kwenye ADF

Sababu zifuatazo zinaweza kuzingatiwa.

### Nakala asili ambazo haziauniwi na ADF zinatumika.

**Suluhisho**

Tumia nakala za kwanza zinazokubaliwa na ADF.

➡ "Vipimo vya ADF" kwenye ukurasa wa 279

### Nakala asili zimepakiwa visivyo.

**Suluhisho**

Pakia nakala za kwanza zikiwa zinaangalia upande unaofaa, na utelezeshe mwongozo wa kingo ya ADF dhidi ya kingo ya nakala asili.

#### Laha nyingi zimepakiwa kwenye ADF.

**Suluhisho**

Usipakie nakala asili juu ya mstari unaoonyeshwa na alama ya pembetatu kwenye ADF.



#### Nakala halisi huteleza endapo vumbi ya karatasi inanata kwenye rola.

**Suluhisho**

Safisha ndani ya ADF.

➡ "Kusafisha ADF" kwenye ukurasa wa 120

#### Nakala Nakala asili hazitambuliwi.

**Suluhisho**

Kwenye skrini ya kunakili, kutambaza, au kutuma faksi, hakikisha kuwa ikoni ya ADF imewashwa. Ikiwa imezima, weka nakala asili tena.

# Haiwezi Kuchapisha

## Haiwezi Kuchapisho kutoka kwenye Windows

Hakikisha kwamba kompyuta na kichapishi vimeunganishwa ipasavyo.

Sababu na suluhu la tatizo hutofautiana kwa kutegemea iwapo vimeunganishwa au la.

### *Kuangalia Hali Ya Muunganisho*

Tumia Epson Printer Connection Checker kuangalia hali ya muunganisho ya kompyuta na kichapishi. Unaweza kutatua tatizo kwa kutegemea matokeo ya uangaliaji.

1. Donoa aikoni ya **Epson Printer Connection Checker** mara mbili kwenye eneo-kazi.

   Epson Printer Connection Checker huanza.

   Iwapo hakuna aikoni kwenye eneo-kazi, fuata mbinu zilizo hapa chini ili kuwasha Epson Printer Connection Checker.

   ❏ Windows 10

   Bofya kitufe cha kuwasha, na kisha uteue **Epson Software** > **Epson Printer Connection Checker**.

   ❏ Windows 8.1/Windows 8

   Andika jina la programu katika sehemu ya utafutaji, na kisha uchague ikoni inayoonekana.

- ❏ Windows 7

  Bofya kitufe cha kuwasha kisha uteue **Programu Zote** > **Epson Software** > **Epson Printer Connection Checker**.

2. Fuata maelekezo yaliyo kwenye skrini ili kuangalia.

   ***Kumbuka:***
   *Iwapo jina la kichapishi halionyeshwi, sakinisha kiendeshi halali cha kichapishi cha Epson.*

   *"Kuangalia ikiwa kiendeshi halali cha kichapishi cha Epson kimesakinishwa — Windows" kwenye ukurasa wa 129*

Ikiwa umetambua tatizo, fuata suluhu inayoonyeshwa kwenye skrini.

Ikiwa huwezi kutatua tatizo, angallia yafuatayo kulingana na hali yako.

- ❏ Kichapishi hakijatambulika kupitia muunganisho wa mtandao

  "Haiwezi kuunganishwa kwenye Mtandao" kwenye ukurasa wa 145

- ❏ Kichapishi hakijatambulika kwa kutumia muunganisho wa USB

  "Kichapishi Hakiwezi Kuunganishwa kupitia USB (Windows)" kwenye ukurasa wa 148

- ❏ Kichapishi kimetambulika lakini hakiwezi kuchapisha.

  "Hakiwezi Kuchapisha Ingawa Muunganisho Umewekwa (Windows)" kwenye ukurasa wa 148

## Haiwezi kuunganishwa kwenye Mtandao

Huenda tatizo likawa mojawapo ya yafuatayo.

### Tatizo fulani limetokea kwenye kifaa cha mtandao kwa muunganisho wa Wi-Fi.

**Suluhisho**

Ikiwa mfumo wako wa simu unahitaji msimbo wa ufikiaji wa nje ili kufikia laini ya nje, sajili msimbo wa ufikiaji kwenye printa, na uingize # (hashi) mwanzoni mwa nambari ya faksi wakati wa kutuma.

### maelMaelezo ya kijajuu kwa faksi zinazoondoka hayajasajiliwa.

**Suluhisho**

Teua **Mipangilio** > **Mipangilio ya Jumla** > **Mipangilio ya Faksi** > **Mipangilio Msingi** > **Kijajuu** na usanidi maelezo ya kijajuu. Baadhi ya mashine za faksi hukataa faksi zinazoingia ambazo hazina taarifa ya kichwa kiotomatiki.

### KiKitambulisho chako cha mpigaji simu kimezuiwa.

**Suluhisho**

Wasiliana na kampuni ya simu yako ili kufungua Kitambulisho chako cha mpigaji simu. Baadhi ya simu na mashine za faksi hukataa simu zisizo na jina kiotomatiki.

### NaNambari ya faksi ya mpokeaji sio sahihi.

**Suluhisho**

Hakikisha kuwa nambari ya mpokeaji iliyosajiliwa kwenye orodha yako ya waasiliani au kuwa uliyoingiza moja kwa moja kwa kutumia kidayo ni sahihi. Au, angalia na mpokeaji ili kuhakikisha kuwa nambari ya faksi ni sahihi.

### MashMashine ya faksi ya mpokeaji hayapotayari kupokea faksi.

**Suluhisho**

Muulize mpokeaji kama mashine ya faksi ya mpokeaji yapo tayari kupokea faksi.

### DataData inayotumwa ni kubwa sana.

**Suluhisho**

Unaweza kutuma faksi kwa ukubewa mdogo wa data ukitumia mojawapo ya mbinu zifuatazo.

- ❏ Unapotuma faksi kwenye rangi moja, wezesha **Tuma Moja kwa Moja** kwenye **Faksi** > **Mipangilio ya Faksi** > **Mipangilio ya Kutuma Faksi**.

  "Kutuma Kurasa Nyingi za Hati Yenye Rangi Moja (Tuma Moja kwa Moja)" kwenye ukurasa wa 93

- ❏ Kutumia simu iliyounganishwa

  "Kudayo Kutuma Faksi kutoka kwa Huduma ya Simu ya Nje" kwenye ukurasa wa 93

❏ Kutenganisha nakala asili

## Haiwezi Kupokea Faksi

Sababu zifuatazo zinaweza kuzingatiwa.

### KujisaKKujisajili kwenye huduma ya usambazaji wa simu.

**Suluhisho**

Ikiwa umejisajili kwa huduma ya kusambaza simu, huenda printa isiweze kupokea faksi. Wasiliana na mtoa huduma.

### Hii Hali ya Kupokea inawekwa kwa Mwenyewe wakati kifaa cha nje cha simu kimeunganishwa kwenye kichapishi.

**Suluhisho**

Iwapo kifaa cha simu cha nje kimeunganishwa kwenye kichapishi na kinashiriki laini ya simu na kichapishi, teua **Mipangilio** > **Mipangilio ya Jumla** > **Mipangilio ya Faksi** > **Mipangilio Msingi**, na kisha uweke **Hali ya Kupokea** iwe **Otomatiki**.

### Kumbukumbu inayopatikana ya kikasha pokezi haitoshi.

**Suluhisho**

Nyaraka 100 zilizopokewa zimehifadhiwa kwenye kisanduku pokezi kwa ujumla. Futa nyaraka zisizofaa.

### Kompyuta itaKompyuta itakayohifadhi faksi zilizopokewa haijawashwa.

**Suluhisho**

Wakati umeunda mipangilio ya kuhifadhi faksi zilizopokewa kwenye kompyuta, washa kompyuta. Faksi iliyopokewa itafutwa pindi tu imehifadhiwa kwenye kompyuta.

### Nambari ya faksi ya mtumaji imesajiliwa kwenye Orodha ya Nambari Zilizozuiwa.

**Suluhisho**

Hakikisha kuwa nambari ya mtyumaji inaweza kufutwa kutoka kwenye **Orodha ya Nambari Zilizozuiwa** kabla ya kuifuta. Ifute kutoka kwenye **Mipangilio** > **Mipangilio ya Jumla** > **Mipangilio ya Faksi** > **Mipangilio Msingi** > **Faksi ya Kukataliwa** > **Hariri Orodha ya Nambari Zilizozuiwa**. Au lemaza **Orodha ya Nambari Zilizozuiwa** kwenye **Mipangilio** > **Mipangilio ya Jumla** > **Mipangilio ya Faksi** > **Mipangilio Msingi** > **Faksi ya Kukataliwa** > **Faksi ya Kukataliwa**. Faksi zilizotumwa kutoka kwenye nambari ambazo hazijasajiliwa kwenye orodha hii zimezuiwa wakati mpangilio huu umewezeshwa.

### Nambari ya faksi ya mtumaji haijasajiliwa kwenye orodha ya waasiliani.

**Suluhisho**

Sajili nambari ya faksi ya mtumaji kwenye orodha ya mwasiliani. Au kulemaza **Waasiliani Wasiosajiliwa** kwenye **Mipangilio** > **Mipangilio ya Jumla** > **Mipangilio ya Faksi** > **Mipangilio Msingi** > **Faksi ya Kukataliwa** > **Faksi ya Kukataliwa**. Faksi zilizotumwa kutoka kwenye nambari ambazo hazijasajiliwa kwenye orodha hii zimezuiwa.

### Mtumaji ametuma faksi bila maelezo ya kijajuu.

**Suluhisho**

Uliza mtumaji iwapo maelezo yamesanidiwa kwenye mashine yake ya faksi. Au, kulemaza **Kijajuu cha Faksi kiko Tupu** kwenye **Mipangilio** > **Mipangilio ya Jumla** > **Mipangilio ya Faksi** > **Mipangilio Msingi** > **Faksi ya Kukataliwa** > **Faksi ya Kukataliwa**. Faksi ambazo hazijumuishi maelezo ya kijajuu zimezuiwa wakati mpangilio huu umewezeshwa.

## Haiwezi Kutuma Faksi kwa Mpokeaji Fulani

### Mpangilio wa Kasi ya Faksi uliosajiliwa kwenye orodha ya waasiliani sio sahihi.

**Suluhisho**

Teua mpokeaji kutoka kwenye orodha, na kisha uteue **Hariri** > **Kasi ya Faksi** > **Polepole(9,600bps)**.

## Haiwezi Kutuma Faksi Wakati Uliotajwa

### Tarehe na saa ya kichapishi sio sahihi.

**Suluhisho**

Teua **Mipangilio** > **Mipangilio ya Jumla** > **Mipangilio Msingi** > **Mipangilio ya Tarehe/Saa**, na kisha uweke tarehe na saa sahihi.

## Faksi Zinatumwa kwa Ukubwa Usio Sahihi

Sababu zifuatazo zinaweza kuzingatiwa.

### Nakala za kwanza hazijawekwa ipasavyo.

**Suluhisho**

- Hakikisha nakala ya kwanza imewekwa sahihi dhidi ya alama za upangiliaji.
- Ikiwa kingo za taswira iliyotambazwa zimepogolewa, sogeza nakala ya kwanza mbali kidogo na kona ya kioo cha kitambazaji. Unaweza kuchanganua eneo ndani ya takriban 1.5 mm (0.06 in.) kutoka kwenye ukingo wa glasi ya kichanganuzi.

➡ "Kuweka Nakala Asili" kwenye ukurasa wa 34

### Kuna vumbi au uchafu kwenye nakala asili au glasi ya kichanganuzi.

**Suluhisho**

Ondoa vumbi au uchafu wowote ambao unashika nakala asili kisha usafishe glasi ya kichanganuzi.

➡ "Kusafisha Glasi ya Kichanganuzi" kwenye ukurasa wa 120

## Faksi Iliyopokewa Haijachapishwa

Sababu zifuatazo zinaweza kuzingatiwa.

### Kosa limetokea kwenye kichapishi kama vile kukwama kwa karatasi.

**Suluhisho**

Futa kosa la kichapishi, na kisha umuulize mtumaji atume upya faksi.

### KucKuchapisha faksi zilizopokewa kumelemazwa chini ya mipangilio ya sasa.

**Suluhisho**

Iwapo **Hifadhi kwenye Kompyuta** imewekwa kwa **Ndiyo**, badilisha mpangilio huu kwenye **Ndiyo na Uchapishe**. Au, lemaza **Hifadhi kwenye Kikasha** na **Hifadhi kwenye Kompyuta** huruhusu uchapishaji kutekelezwa.

Unaweza kutafuta **Hifadhi kwenye Kikasha** na **Hifadhi kwenye Kompyuta** kwenye **Mipangilio** > **Mipangilio ya Jumla** > **Mipangilio ya Faksi** > **Mipangilio ya Kupokea** > **Faksi Towe**.

## Haiwezi Kutuma Au Kupokea Faksi (Windows)

Hakikisha kwamba kompyuta na kichapishi vimeunganishwa ipasavyo. Sababu na suluhu la tatizo hutofautiana kwa kutegemea iwapo vimeunganishwa au la.

### *Kuangalia Hali Ya Muunganisho*

Tumia Epson Printer Connection Checker kuangalia hali ya muunganisho ya kompyuta na kichapishi. Unaweza kutatua tatizo kwa kutegemea matokeo ya uangaliaji.

1. Donoa aikoni ya **Epson Printer Connection Checker** mara mbili kwenye eneo-kazi.

   Epson Printer Connection Checker huanza.

   Iwapo hakuna aikoni kwenye eneo-kazi, fuata mbinu zilizo hapa chini ili kuwasha Epson Printer Connection Checker.

   - Windows 10

     Bofya kitufe cha kuwasha, na kisha uteue **Epson Software** > **Epson Printer Connection Checker**.

   - Windows 8.1/Windows 8

     Andika jina la programu katika sehemu ya utafutaji, na kisha uchague ikoni inayoonekana.

   - Windows 7

     Bofya kitufe cha kuwasha kisha uteue **Programu Zote** > **Epson Software** > **Epson Printer Connection Checker**.

2. Fuata maelekezo yaliyo kwenye skrini ili kuangalia.

   ***Kumbuka:***
   *Iwapo jina la kichapishi halionyeshwi, sakinisha kiendeshi halali cha kichapishi cha Epson.*

   *"Kuangalia ikiwa kiendeshi halali cha kichapishi cha Epson kimesakinishwa — Windows" kwenye ukurasa wa 129*

Ikiwa umetambua tatizo, fuata suluhu inayoonyeshwa kwenye skrini.

Ikiwa huwezi kutatua tatizo, angallia yafuatayo kulingana na hali yako.

- Kichapishi hakijatambulika kupitia muunganisho wa mtandao

  "Haiwezi kuunganishwa kwenye Mtandao" kwenye ukurasa wa 145

- Kichapishi hakijatambulika kwa kutumia muunganisho wa USB
  "Kichapishi Hakiwezi Kuunganishwa kupitia USB (Windows)" kwenye ukurasa wa 148
- Kichapishi kimetambulika lakini hakiwezi kuchapisha.
  "Hakiwezi Kuchapisha Ingawa Muunganisho Umewekwa (Windows)" kwenye ukurasa wa 148

## Haiwezi kuunganishwa kwenye Mtandao

Huenda tatizo likawa mojawapo ya yafuatayo.

### Tatizo fulani limetokea kwenye kifaa cha mtandao kwa muunganisho wa Wi-Fi.

**Suluhisho**

Zima vifaa unavyotaka kuunganisha kwenye mtandao. Subiri karibu sekunde 10, na kisha uwashe vifaa katika mpangilio ufuatao; kipanga njia pasiwaya, kompyuta au kifaa maizi, na kisha kichapishi. Sogeza kichapishi na kompyuta au kifaa mahiri karibu na kipanga njia pasiwaya ili kusaidia na mawasiliano ya mawimbi ya redio, na kisha jaribu kutengeneza mipangilio ya mtandao tena.



### Vifaa haviwezi kupokea mawimbi kutoka kwenye kipanga njia pasiwaya kwa sababu vimetenganishwa kwa mbali sana.

**Suluhisho**

Baada ya kusogeza kompyuta au kifaa maizi na kichapishi karibu na kipanga njia pasiwaya, zima kipanga njia pasiwaya kisha ukiwashe tena.

### Unapobadilisha kipanga njia pasiwaya, mipangilio hailingani na kipanga njia kipya.

**Suluhisho**

Weka mipangilio ya muunganisho tena ili ilingane na kipanga njia pasiwaya kipya.

➡ "Unapobadilisha Kipanga Njia Pasiwaya" kwenye ukurasa wa 230

### SSID zilizounganishwa kutoka kompyuta au kifaa maizi na komyuta ni tofauti.

**Suluhisho**

Unapotumia vipanga njia pasiwaya vingi kwa wakati mmoja au kipanga njia pasiwaya kina SSID nyingi na vifaa vimeunganishwa kwenye SSID tofauti, huwezi kuunganisha kipanga njia pasiwaya.

Unganisha kompyuta au kifaa maizi kwenye SSID moja kama kichapishi.

- Mfano wa kuunganisha SSID tofauti




- Mfano wa kuunganisha SSID zenye safu tofauti za wawimbi




## Kitenganishi cha faragha kwenye kipanga njia pasiwaya kinapatikana.

### Suluhisho

Vipanga njia vingi pasiwaya bvina kitendaji cha kitenganishi kinachozuia mawasiliano kati ya vifaa ndani ya SSID sawa. Iwapo huwezi kuwasiliana kati ya kichapishi na kompyuta au kifaa maizi hata iwapo vimeunganishwa kwenye mtandao mmoja, lemaza kitendaji cha kitenganishi kwenye kipanga njia pasiwaya. Tazama mwongozo uliotolewa ulio na kipanga njia pasiwaya kwa maelezo.

## Anwani ya IP haijapangiwa ipasavyo.

### Suluhisho

Iwapo anwani ya IP iliyopangiwa kichapishi ni 169.254.XXX.XXX, na barakoa ndogo ni 255.255.0.0, huenda anwani ya IP isipangiwe kwa usahihi.

Teua **Mipangilio** > **Mipangilio ya Jumla** > **Mipangilio ya Mtandao** > **Mahiri** kwenye paneli dhibiti ya kichapishi, kisha uangalie anwani ya IP na barakoa ndogo iliyopangiwa kichapishi.

Washa upya kipanga njia chako pasiwaya au weka upya mipangilio ya mtandao kwa kichapishi.

## Kuna tatizo na mipangilio ya mtandao kwenye kompyuta hii.

**Suluhisho**

Jaribu kufikia tovuti yoyote kutoka kwenye kompyuta yako ili kuhakikisha kuwa mipangilio ya mtandao wa kompyuta yako ni sahihi. Iwapo huwezi kufikia tovuti yoyote, kuna tatizo kwenye kompyuta.

Angalia muunganisho wa mtandao wa kompyuta. Tazama hati iliyotolewa yenye kompyuta kwa maelezo.

## Kichapishi kimeunganishwa kwa Ethaneti kwa kutumia vifaa vinavyotumia IEEE 802.3az (Ethaneti Inayotunza Nishati).

**Suluhisho**

Unapounganisha kichapishi kwa Ethaneti ukitumia kifaa kinachotumia IEEE 802.3az (Energy Efficient Ethernet), matatizo yafuatayo yanaweza kutokea kwa kutegemea kitovu au kipanga njia unachotumia.

- Muunganisho unakuwa dhaifu, kichapishi kimeunganishwa na kutenganishwa tena na tena.
- Haiwezi kuunganisha kwenye kichapishi.
- Kasi ya mawasiliano inajikokota.

Fuata maelekezo hapa chini ili kulemaza IEEE 802.3az kwa kichapishi kisha uunganishe.

1. Ondoa kebo ya Ethaneti iliyounganishwa kwenye kompyuta na kichapishi.
2. Ikiwa IEEE 802.3az ya kompyuta imewezeshwa, ilemaze.

   Tazama hati iliyotolewa yenye kompyuta kwa maelezo.
3. Unganisha kompyuta na kichapishi ukitumia kebo ya Ethaneti moja kwa moja.
4. Kwenye kichapishi, chapisha ripoti ya muunganisho wa mtandao.

   "Kuchapisha Ripoti ya Muunganisho wa Mtandao" kwenye ukurasa wa 241
5. Angalia anwani ya IP ya kichapishi kwenye ripoti ya muunganisho wa mtandao.
6. Kwenye kompyuta, fikia Web Config.

   Zindua kivinjari Wavuti, na kisha uingize anwani ya IP ya kichapishi.

   "Kuendesha Web Config Kwenye Kivinjari Wavuti" kwenye ukurasa wa 261
7. Teua **Advanced Settings** kutoka kwenye orodha upande wa juu kulia wa dirisha.
8. Teua **Network Settings** > **Wired LAN**.
9. Teua **OFF** kwa **IEEE 802.3az**.
10. Bofya **Next**.
11. Bofya **OK**.
12. Ondoa kebo ya Ethaneti iliyounganishwa kwenye kompyuta na kichapishi.
13. Ikiwa ulilemaza IEEE 802.3az ya kompyuta katika hatua ya 2, iwezeshe.
14. Unganisha kebo za Ethaneti ulizoondoa kwenye hatua ya 1 kwenye kompyuta na kichapishi.

Iwapo bado tatizo linatokea, vifaa kando na kichapishi vinaweza kuwa vinatumia tatizo.

## Kichapishi Hakiwezi Kuunganishwa kupitia USB (Windows)

Sababu zifuatazo zinaweza kuzingatiwa.

### Kebo ya USB haijachomekwa kwenye njia ya umeme ipasavyo.

**Suluhisho**

Unganisha kebo ya USB vizuri kwenye kichapishi na kompyuta.

### Kuna tatizo na kitovu cha USB.

**Suluhisho**

Ikiwa unatumia kitovu cha USB, jaribu kuunganisha kichapishi moja kwa moja kwenye kompyuta.

### Kuna tatizo na kebo ya USB au upenyo wa kuingiza USB.

**Suluhisho**

Iwapo kebo ya USB haiwezi kutambuliwa, badilisha kiweko, au badilisha kebo ya USB.

## Haiwezi Kutuma au Kupokea Faksi Hata Ingawa Muunganisho Umewekwa Ipasavyo (Windows)

Sababu zifuatazo zinaweza kuzingatiwa.

### prPProgramu haijasakinishwa.

**Suluhisho**

Hakikisha kwamba kiendeshi cha PC-FAX kimesakinishwa kwenye kompyuta. Kiendeshi cha PC-FAX kimesakinishwa pamoja na FAX Utility. Fuata hatua za hapa chini ili kuangalia jiwapo kimesakinishwa.

Hakikisha kichapishi (faksi) kinaonekana katika **Vifaa na Vichapishi**, **Kichapishi**, au **Kichapishi na Maunzi Mengine**. Printa (faksi) inaonekana kama “EPSON XXXXX (FAX)”. Ikiwa kichapishi (faksi) hakionekani, sakinusha FAX Utility na kisha uisakinishe upya. Angalia yafuatayo ili ufikie **Vifaa na Vichapishi**, **Kichapishi**, au **Vichapishi na Maunzi Mengine**.

- Windows 10

  Bofya kitufe cha kuwasha kisha uchague **Mifumo ya Windows** > **Paneli Dhibiti** > **Tazama vifaa na vichapishi** katika **Maunzi na Sauti**.

- Windows 8.1/Windows 8

  Teua **Eneo-kazi** > **Mipangilio** > **Paneli Dhibiti** > **Tazama vifaa na vichapishi** katika **Maunzi na Sauti** au **Maunzi**.

- Windows 7

  Bofya kitufe cha kuanza, na uchague **Paneli Dhibiti** > **Tazama vifaa na vichapishi** katika **Maunzi na Sauti** au **Maunzi**.

- Windows Vista

  Bofya kitufe cha kuwasha, na uteue **Paneli Dhibiti** > **Kichapishi** katika **Maunzi na Sauti**.

- Windows XP

  Bofya kitufe cha kuanza, na uchague **Mipangilio** > **Paneli Dhibiti** > **Printa na Maunzi Mengine** > **Printa na Faksi**.

### Uhalalishaji wa mtumiaji umeshindikana wakati faksi imetumwa kutoka kwenye kompyuta.

**Suluhisho**

Weka jina la mtumiaji na nenosiri kwenye kiendeshi cha kichapishi. Unapotuma faksi kutoka kwenye kompyuta wakati kitendaji cha usalama kinachowazuia watumiaji dhidi ya kutumia kitendaji cha faksi ya kichapishi kiwekwa, uhalalishaji wa mtumiaji unatekelezwa kwa jina la mtumiaji na nenosiri kama imewekwa kwenye kiendeshi cha kichapishi.

### Kuna baadhi ya matatizo kwa muunganisho wa faksi na mipangilio ya faksi.

**Suluhisho**

Jaribu suluhisho za muunganisho wa faksi na mipangilio ya faksi.

## Haiwezi Kutuma Au Kupokea Faksi (Mac OS)

Hakikisha kwamba kompyuta na kichapishi vimeunganishwa ipasavyo. Sababu na suluhu la tatizo hutofautiana kwa kutegemea iwapo vimeunganishwa au la.

### *Kuangalia Hali Ya Muunganisho*

Tumia EPSON Status Monitor kuangalia hali ya muunganisho ya kompyuta na kichapishi.

1. Teua **Mapendeleo ya Mfumo** kwenye menyu ya Apple > **Vichapishaji na Vitambazaji** (au **Chapisha na Utambaze**, **Chapisha na Utume Faksi**), na kisha uteue kichapishi.

2. Bofya **Chaguo na Vifaa** > **Huduma** > **Fungua Huduma ya Printa**.

3. Bofya **EPSON Status Monitor**.

Viwango vya wino unaosalia vikionyeshwa, muunganisho umefaulu kuwekwa kati ya kompyuta na kichapishi.

Angalia yafuatayo ikiwa muunganisho haujawekwa.

❏ Kichapishi hakijatambulika kupitia muunganisho wa mtandao

"Haiwezi kuunganishwa kwenye Mtandao" kwenye ukurasa wa 152

❏ Kichapishi hakijatambulika kwa kutumia muunganisho wa USB

"Kichapishi Hakiwezi Kuunganishwa kupitia USB (Mac OS)" kwenye ukurasa wa 155

Angalia yafuatayo ikiwa muunganisho umewekwa.

❏ Kichapishi kimetambulika lakini hakiwezi kuchapisha.

"Hakiwezi Kuchapisha Ingawa Muunganisho Umewekwa (Mac OS)" kwenye ukurasa wa 156

## Haiwezi kuunganishwa kwenye Mtandao

Huenda tatizo likawa mojawapo ya yafuatayo.

### Tatizo fulani limetokea kwenye kifaa cha mtandao kwa muunganisho wa Wi-Fi.

**Suluhisho**

Zima vifaa unavyotaka kuunganisha kwenye mtandao. Subiri karibu sekunde 10, na kisha uwashe vifaa katika mpangilio ufuatao; kipanga njia pasiwaya, kompyuta au kifaa maizi, na kisha kichapishi. Sogeza

kichapishi na kompyuta au kifaa mahiri karibu na kipanga njia pasiwaya ili kusaidia na mawasiliano ya mawimbi ya redio, na kisha jaribu kutengeneza mipangilio ya mtandao tena.



## Vifaa haviwezi kupokea mawimbi kutoka kwenye kipanga njia pasiwaya kwa sababu vimetenganishwa kwa mbali sana.

### Suluhisho

Baada ya kusogeza kompyuta au kifaa maizi na kichapishi karibu na kipanga njia pasiwaya, zima kipanga njia pasiwaya kisha ukiwashe tena.

## Unapobadilisha kipanga njia pasiwaya, mipangilio hailingani na kipanga njia kipya.

### Suluhisho

Weka mipangilio ya muunganisho tena ili ilingane na kipanga njia pasiwaya kipya.

➡ "Unapobadilisha Kipanga Njia Pasiwaya" kwenye ukurasa wa 230

## SSID zilizounganishwa kutoka kompyuta au kifaa maizi na komyuta ni tofauti.

### Suluhisho

Unapotumia vipanga njia pasiwaya vingi kwa wakati mmoja au kipanga njia pasiwaya kina SSID nyingi na vifaa vimeunganishwa kwenye SSID tofauti, huwezi kuunganisha kipanga njia pasiwaya.

Unganisha kompyuta au kifaa maizi kwenye SSID moja kama kichapishi.

- ❏ Mfano wa kuunganisha SSID tofauti



❏ Mfano wa kuunganisha SSID zenye safu tofauti za wawimbi




## Kitenganishi cha faragha kwenye kipanga njia pasiwaya kinapatikana.

**Suluhisho**

Vipanga njia vingi pasiwaya bvina kitendaji cha kitenganishi kinachozuia mawasiliano kati ya vifaa ndani ya SSID sawa. Iwapo huwezi kuwasiliana kati ya kichapishi na kompyuta au kifaa maizi hata iwapo vimeunganishwa kwenye mtandao mmoja, lemaza kitendaji cha kitenganishi kwenye kipanga njia pasiwaya. Tazama mwongozo uliotolewa ulio na kipanga njia pasiwaya kwa maelezo.

## Anwani ya IP haijapangiwa ipasavyo.

**Suluhisho**

Iwapo anwani ya IP iliyopangiwa kichapishi ni 169.254.XXX.XXX, na barakoa ndogo ni 255.255.0.0, huenda anwani ya IP isipangiwe kwa usahihi.

Teua **Mipangilio** > **Mipangilio ya Jumla** > **Mipangilio ya Mtandao** > **Mahiri** kwenye paneli dhibiti ya kichapishi, kisha uangalie anwani ya IP na barakoa ndogo iliyopangiwa kichapishi.

Washa upya kipanga njia chako pasiwaya au weka upya mipangilio ya mtandao kwa kichapishi.

## Kuna tatizo na mipangilio ya mtandao kwenye kompyuta hii.

**Suluhisho**

Jaribu kufikia tovuti yoyote kutoka kwenye kompyuta yako ili kuhakikisha kuwa mipangilio ya mtandao wa kompyuta yako ni sahihi. Iwapo huwezi kufikia tovuti yoyote, kuna tatizo kwenye kompyuta.

Angalia muunganisho wa mtandao wa kompyuta. Tazama hati iliyotolewa yenye kompyuta kwa maelezo.

## Kifaa kilichounganishwa kwenye kituo cha USB 3.0 kinasababisha mtafaruku wa mawimbi.

**Suluhisho**

Unapounganisha kifaa kwenye kituo tayarishi cha USB 3.0 kwenye Mac, ukatizaji wa mawimbi ya redio unaweza kutokea. Jaribu yafuatayo iwapo huwezi kunganisha kwenye LAN pasiwaya (Wi-Fi) au iwapo operesheni hazitakuwa thabiti.

❏ Weka kifaa kilichounganishwa kwenye kituo tayarishi cha USB 3.0 mbali na kompyuta.

### Kichapishi kimeunganishwa kwa Ethaneti kwa kutumia vifaa vinavyotumia IEEE 802.3az (Ethaneti Inayotunza Nishati).

#### Suluhisho

Unapounganisha kichapishi kwa Ethaneti ukitumia kifaa kinachotumia IEEE 802.3az (Energy Efficient Ethernet), matatizo yafuatayo yanaweza kutokea kwa kutegemea kitovu au kipanga njia unachotumia.

- Muunganisho unakuwa dhaifu, kichapishi kimeunganishwa na kutenganishwa tena na tena.
- Haiwezi kuunganisha kwenye kichapishi.
- Kasi ya mawasiliano inajikokota.

Fuata maelekezo hapa chini ili kulemaza IEEE 802.3az kwa kichapishi kisha uunganishe.

1. Ondoa kebo ya Ethaneti iliyounganishwa kwenye kompyuta na kichapishi.
2. Ikiwa IEEE 802.3az ya kompyuta imewezeshwa, ilemaze.

   Tazama hati iliyotolewa yenye kompyuta kwa maelezo.
3. Unganisha kompyuta na kichapishi ukitumia kebo ya Ethaneti moja kwa moja.
4. Kwenye kichapishi, chapisha ripoti ya muunganisho wa mtandao.

   “Kuchapisha Ripoti ya Muunganisho wa Mtandao” kwenye ukurasa wa 241
5. Angalia anwani ya IP ya kichapishi kwenye ripoti ya muunganisho wa mtandao.
6. Kwenye kompyuta, fikia Web Config.

   Zindua kivinjari Wavuti, na kisha uingize anwani ya IP ya kichapishi.

   “Kuendesha Web Config Kwenye Kivinjari Wavuti” kwenye ukurasa wa 261
7. Teua **Advanced Settings** kutoka kwenye orodha upande wa juu kulia wa dirisha.
8. Teua **Network Settings** > **Wired LAN**.
9. Teua **OFF** kwa **IEEE 802.3az**.
10. Bofya **Next**.
11. Bofya **OK**.
12. Ondoa kebo ya Ethaneti iliyounganishwa kwenye kompyuta na kichapishi.
13. Ikiwa ulilemaza IEEE 802.3az ya kompyuta katika hatua ya 2, iwezeshe.
14. Unganisha kebo za Ethaneti ulizoondoa kwenye hatua ya 1 kwenye kompyuta na kichapishi.

Iwapo bado tatizo linatokea, vifaa kando na kichapishi vinaweza kuwa vinatumia tatizo.

## Kichapishi Hakiwezi Kuunganishwa kupitia USB (Mac OS)

Sababu zifuatazo zinaweza kuzingatiwa.

#### Kebo ya USB haijachomekwa kwenye njia ya umeme ipasavyo.

**Suluhisho**

Unganisha kebo ya USB vizuri kwenye kichapishi na kompyuta.

#### Kuna tatizo na kitovu cha USB.

**Suluhisho**

Ikiwa unatumia kitovu cha USB, jaribu kuunganisha kichapishi moja kwa moja kwenye kompyuta.

#### Kuna tatizo na kebo ya USB au upenyo wa kuingiza USB.

**Suluhisho**

Iwapo kebo ya USB haiwezi kutambuliwa, badilisha kiweko, au badilisha kebo ya USB.

### Haiwezi Kutuma au Kupokea Hata Ingawa Muunganisho Umewekwa Ipasavyo (Mac OS)

Sababu zifuatazo zinaweza kuzingatiwa.

#### Programu haijasakinishwa.

**Suluhisho**

Hakikisha kwamba kiendeshi cha PC-FAX kimesakinishwa kwenye kompyuta. Kiendeshi cha PC-FAX kimesakinishwa pamoja na FAX Utility. Fuata hatua za hapa chini ili kuangalia jiwapo kimesakinishwa.

Teua **Mapendeleo ya Mfumo** kutoka kwenye menyu ya Apple > **Vichapishi na Vitambazaji** (au **Chapisho na Tambazo**, **Kuchapisha na Faksi**), na kisha uhakikishe kichapishi (faksi) kimeonyeshwa. Kichapishi (faksi) kinaonekana kama “FAX XXXX (USB)” au “FAX XXXX (IP)”. Ikiwa kichapishi (faksi) hakionekani, bofya [+] na kisha usajili printa (faksi) hiyo.

#### Kiendeshi cha PC-FAX kimesitishwa.

**Suluhisho**

Teua **Mapendeleo ya Mfumo** kutoka kwenye menyu ya Apple > **Vichapishi na Vitambazaji** (au **Chapisho na Tambazo**, **Chapisho na Faksi**), na kisha ubofye mara mbili kichapishi (faksi). Ikiwa kichapishi kimesitishwa, bofya **Endelea** (au **Endelea Kutumia Kichapishi**).

#### Uhalalishaji wa mtumiaji umeshindikana wakati faksi imetumwa kutoka kwenye kompyuta.

**Suluhisho**

Weka jina la mtumiaji na nenosiri kwenye kiendeshi cha kichapishi. Unapotuma faksi kutoka kwenye kompyuta wakati kitendaji cha usalama kinachowazuia watumiaji dhidi ya kutumia kitendaji cha faksi ya kichapishi kiwekwa, uhalalishaji wa mtumiaji unatekelezwa kwa jina la mtumiaji na nenosiri kama imewekwa kwenye kiendeshi cha kichapishi.

#### Kuna baadhi ya matatizo kwa muunganisho wa faksi na mipangilio ya faksi.

**Suluhisho**

Jaribu suluhisho za muunganisho wa faksi na mipangilio ya faksi.

# Haiwezi Kuendesha Kichapishi Inavyotarajiwa

## Operesheni ziko Polepole

### Inachapisha Polepole Sana

Sababu zifuatazo zinaweza kuzingatiwa.

#### Programu zisizo muhimu zinaendeshwa.

**Suluhisho**

Funga programu zozote zisizo muhimu kwenye kompyuta au kifaa chako maizi.

#### Ubora wa chapisho umewekwa kuwa juu.

**Suluhisho**

Punguza mpangilio wa ubora.

#### Uchapishaji wa pande mbili umelemazwa.

**Suluhisho**

Wezesha mipangilio ya pande mbili (au kasi ya juu). Wakati mpangilio huu umewezeshwa, kichwa cha kichapisha huchapisha kikisogea pande zote mbili, na kasi ya uchapishaji huongezeka.

- Windows

  Teua **Uchapishaji katika mielekeo miwili** kwenye kichupo cha **Chaguo Zaidi** cha kiendeshi cha kichapishi.

- Mac OS

  Teua **Mapendeleo ya Mfumo** kwenye menyu ya Apple > **Vichapishaji na Vitambazaji** (au **Chapisha na Utambaze**, **Chapisha na Utume Faksi**), kisha uteue kichapishaji. Bofya **Chaguo na Vifaa** > **Chaguo** (au **Kiendeshi**). Teua On kama mpangilio wa **Uchapishaji katika mielekeo miwili**.

#### Modi Tulivu imelemazwa.

**Suluhisho**

Lemaza **Modi Tulivu**. Kasi ya kuchapisha hupungua wakati kichapishi kikiendeshwa katika **Modi Tulivu**.

- Paneli Dhibiti

  Teua  kwenye skrini ya nyumbani kisha uteue **Zima**.

- Windows

  Teua **Zima** kama mpangilio wa **Modi Tulivu** kwenye kichupo cha **Kuu** kiendeshi cha kichapishi.

- Mac OS

  Teua **Mapendeleo ya Mfumo** kwenye menyu ya Apple > **Vichapishaji na Vitambazaji** (au **Chapisha na Utambaze**, **Chapisha na Utume Faksi**), kisha uteue kichapishaji. Bofya **Chaguo na Vifaa** > **Chaguo** (au **Kiendeshi**). Teua Off kama mpangilio wa **Modi Tulivu**.

## Kasi ya Uchapishaji Inapungua Haraka Wakati wa Uchapishaji Endelevu

### Kitendaji kinachozuia uendeshaji wa kichapishi dhidi ya kupata joto jingi na kuharibika kinaendesha operesheni.

**Suluhisho**

Unaweza kuendelea kuchapisha. Ili urudi kwa kasi ya kawaida ya uchapishaji, wacha kichapishi kitulie kwa angalau dakika 30. Kasi ya uchapishaji hairudi kwa kwasi ya kawaida ikiwa imezimwa.

## Kasi ya Utambazaji Iko Chini

### Kutambaza kwa ubainifu wa juu.

**Suluhisho**

Jaribu kutambaza kwa ubainifu wa chini.

## Skrini ya LCD Inakuwa Nyeusi

### Printa iko katika modi ya kulala.

**Suluhisho**

Donoa mahali popote kwenye skrini ya LCD ili kuirejesha kwa hali yake ya awali.

## Sauti za Operesheni ziko Juu

### Modi Tulivu imelemazwa.

**Suluhisho**

Ikiwa sauti za operesheni iko juu sana, wezesha **Modi Tulivu**. Kuwezesha kipengele hiki kunaweza kupunguza kasi ya uchapishaji.

- ❏ Paneli Dhibiti

  Teua  kwenye skrini ya nyumbani, na kisha uwezeshe **Hali Tulivu**.

- ❏ Kiendeshi cha printa cha Windows

  Wezesha **Modi Tulivu** kwenye kichupo cha **Kuu**.

- ❏ Kiendeshi cha printa cha Mac OS

  Teua **Mapendeleo ya Mfumo** kwenye menyu ya Apple > **Vichapishaji na Vitambazaji** (au **Chapisha na Utambaze**, **Chapisha na Utume Faksi**), na kisha uteue kichapishaji. Bofya **Chaguo na Vifaa** > **Chaguo** (au **Kiendeshi**). Teua **On** kama mpangilio wa **Modi Tulivu**.

## Tarehe na Saa Sio Sahihi

### KosaKosa lilitokea kwenye usambazaji wa nishati.

**Suluhisho**

Baada ya kupotea kwa stima kunakosababishwa na radi au ikiwa kifaa kimezimwa kwa muda mrefu saa inaweza kuonyesha wakati usio sahihi. Weka tarehe na saa kwa usahihi kwenye **Mipangilio** > **Mipangilio ya Jumla** > **Mipangilio Msingi** > **Mipangilio ya Tarehe/Saa** kwenye paneli dhibiti.

## Cheti Kuu Kinahitaji Kusasishwa

### Muda wa cheti kikuu umekwisha.

**Suluhisho**

Endesha Web Config, na kisha usasishe cheti cha shina.

## Haiwezi Kukatisha Kuchapisha kutoka kwenye Kompyuta Inayoendesha Mac OS X v10.6.8

### Kuna tatizo kwa usanidi wako wa AirPrint.

**Suluhisho**

Endesha Web Config, kisha uchague **Port9100** kama mipangilio ya **Itifaki Kipaumbele** katika **AirPrint Setup**. Teua **Mapendeleo ya Mfumo** kwenye menyu ya Apple > **Vichapishaji na Vitambazaji** (au **Chapisha na Utambaze**, **Chapisha na Utume Faksi**), ondoa kichapishi kisha ukirejeshe tena.

➡ “Programu ya Kusawazisha Utendakazi wa Kichapishi (Web Config)” kwenye ukurasa wa 260

## Ujumbe Unaokukumbusha Kuweka Upya Kiwango cha Wino Unaonyeshwa Hata Baada ya Kujaza upya Wino

### Kiwango cha wino hakikuwekwa upya.

**Suluhisho**

Baada ya kujaza upya wino, fuata maelekezo yaliyo kwenye skrini ili kuweka upya kiwango cha wino.

➡ “Vidokezo vya Kuweka upya Kiwango cha Wino” kwenye ukurasa wa 203

## Onyesho la Kiwango cha Wino Halibadiliki Hata Baada ya Kujaza upya Wino

### Kiwango cha wino hakikuwekwa upya.

**Suluhisho**

Baada ya kujaza upya wino, fuata maelekezo yaliyo kwenye skrini ili kuweka upya kiwango cha wino.

➡ “Vidokezo vya Kuweka upya Kiwango cha Wino” kwenye ukurasa wa 203

### Nambari ya Faksi ya Mtumaiji Haikuonyeshwa

#### Nambari ya faski ya mtumaiji haijawekwa kwenye mashine ya mtumaji.

**Suluhisho**

Huenda mtumaji hajaweka nambari ya faksi. Wasiliana na mtumaji.

### Nambari ya Faksi ya Mtumaji Inayoonyeshwa Kwenye Faksi Zilizopokewa Sio Sahihi

#### nambari ya faski ya mtyumNambari ya faski ya mtumaiji iliyowekwa kwenye mashine ya mtumaji sio sahihi.

**Suluhisho**

Huenda mtumaji ameweka nambari ya faksi visivyo. Wasiliana na mtumaji.

### Haiwezi Kupiga Simu kwenye Simu Iliyounganishwa

#### Kebo ya simu haijaunganishwa ipasavyo.

**Suluhisho**

Unganisha simu kwenye lango la EXT. kwenye printa, na uchukue mkono wa simu. Usiposikia toni ya kudayo kupitia mkono wa simu, unganisha kebo ya simu ipasavyo.

### Mashine ya Kujibu Haiwezi Kujibu Simu za Sauti

#### Mpangilio wa kichapishi wa Hutoa mlio ili Kujibu umewekwa kwa chini ya idadi ya milio kwa mashine yako ya kujibu.

**Suluhisho**

Teua **Mipangilio** > **Mipangilio ya Jumla** > **Mipangilio ya Faksi** > **Mipangilio Msingi** > **Hutoa mlio ili Kujibu**, na kisha uweke idadi ya juu zaidi kuliko idadi ya milio kwa mashine yako ya kujibu.

### FaksiFaksi Nyingi Taka Zimepokelewa

#### KipKipengele cha kichapishi cha kuzuia faksi taka hakijasanidiwa.

**Suluhisho**

Weka mipangilio ya **Faksi ya Kukataliwa** kwenye **Mipangilio** > **Mipangilio ya Jumla** > **Mipangilio ya Faksi** > **Mipangilio Msingi**.

"Kuunda Mipangilio ya Kuzuia Faksi Taka" kwenye ukurasa wa 305

## Ujumbe unaonyeshwa kwenye Skrini ya LCD

Ikiwa ujumbe wa hitilafu unaonekana kwenye skrini ya LCD, fuata maelekezo yaliyo kwenye skrini au usuluhishaji ulio hapa chini kutatua tatizo hilo.

| Ujumbe wa Hitilafu | Suluhisho |
|---|---|
| Hitilafu ya Printa<br>Washa printa tena. Angalia nyaraka zako kwa maelezo zaidi. | Ondoa karatasi yoyote au nyenzo yoyote ya kukinga katika printa. Iwapo bado ujumbe wa kosa unaonyeshwa, wasiliana na auni ya Epson. |
| Karatasi zinazotoka kwenye XX. | Pakia karatasi, na kisha uchomeke mkanda wa karatasi kila wakati. |
| Pedi ya wino ya machapisho yasiyo na mipaka ya printa inakaribia mwisho wa matumizi yake. Sio sehemu inayoweza kubadilishwa. Tafadhali wasiliana na auni ya Epson. | Wasiliana na Epson au mtoa huduma aliyeidhinishwa na Epson ili abadilishe padi ya wino ya uchapishaji usio na mipaka*. Sio sehemu ya kukarabatiwa na mtumiaji.<br>Donoa **OK** ili kuendelea na uchapishaji. |
| Pedi ya wino ya machapisho yasiyo na mipaka ya printa imefikisha mwisho wa matumizi yake. Sio sehemu inayoweza kubadilishwa. Tafadhali wasiliana na auni ya Epson. | Wasiliana na Epson au mtoa huduma aliyeidhinishwa na Epson ili abadilishe padi ya wino ya uchapishaji usio na mipaka*. Sio sehemu ya kukarabatiwa na mtumiaji.<br>Hata hivyo, unaweza kutenda shughuli zisizotumia wino kama vile utambazaji. |
| Onyesho Otom. Usanidi wa Karatasi Imezimwa. Baadhi ya vipengele vinaweza kokosekana. Kwa maelezo, angalia nyaraka. | Ikiwa **Onyesho Otom. Usanidi wa Karatasi** imelemazwa, huwezi kutumia AirPrint. |
| Hakuna mlio wa simu uliotambuliwa. | Tatizo hili linaweza kutatuliwa kwa kuteua **Mipangilio** > **Mipangilio ya Jumla** > **Mipangilio ya Faksi** > **Mipangilio Msingi** > **Aina ya Laini** na kisha kuteua **PBX**. Ikiwa mfumo wa simu yako unahitaji msimbo wa ufikiaji wa nje ili umapte mstari wa nje, wake msimbo wa ufikiaji baada ya kuchagua **PBX**. Tumia # (hashi) badala ya msimbo halisi wa ufikiaji unapoingiza nambari ya faksi ya nje. Hii hufanya muunganisho kuwa salama zaidi.<br>Ikiwa ujumbe wa hitilafu bado unaonekana, weka mipangilio ya kuwa **Ugunduaji Mlio wa kupiga Simu** imelemazwa. Hata hivyo, kulemaza kipengele hiki kunaweza kufuta tarakimu ya kwanza ya nambari ya faksi na itume faksi kwa nambari isiyo sahihi. |
| Mchanganyiko wa anwani ya IP na Barakoa ya Subnet si sahihi. Angalia nyaraka zako kwa maelezo zaidi. | Ingiza anwani sahihi ya IP au kichanganishi chaguo-msingi. Wasiliana na mtu aliyesanidi mtandao kwa usaidizi. |
| Sasisha cheti shina ili utumie huduma za wingu. | Endesha Web Config, na kisha usasishe cheti cha shina. |
| Angalia kuwa kiendeshi cha printa imesakinishwa kwenye kompyuta na kuwa mipangilio ya kituo ya printa ni sahihi. | Bofya **Foleni ya U'haji** kwenye kichupo cha kienfdeshi cha kichapishi cha **Utunzaji**. Hakikisha kuwa tundu la kichapishi limeteuliwa vizuri katika **Sifa** > **Tundu** kutoka kwenye menyu ya **Kichapishi** kama ifuatavyo.<br>Teua “**USBXXX**” kwa muunganisho wa USB, au “**EpsonNet Print Port**” kwa muunganisho wa mtandao. |
| Angalia kuwa kiendeshi cha printa imesakinishwa kwenye kompyuta na kuwa mipangilio ya kituo cha USB cha printa ni sahihi. | |
| Recovery Mode<br>Update Firmware | Kichapishi kimeanza katika modi ya kurejesha kwa sababu sasisho la programu msingi halijafaulu. Fuata hatua zilizo hapa chini ujaribu kusasisha ngome tena.<br>1. Unganisha kompyuta na kichapishi ukitumia kebo ya USB. (Wakati wa modi ya kurejesha, huwezi kusasisha programu msingi kupitia muunganisho wa mtandao.)<br>2. Tembelea tovuti yako ya Epson kwa maelekezo zaidi. |

* Katika baadhi ya mizunguko ya uchapishaji kiasi kidogo sana cha wino wa ziada kinaweza kukusanywa katika padi ya wino ya uchapishaji usiokuwa na mpaka. Ili kuzuia uvujaji wa wino kutoka kwenye padi, bidhaa hii

imeundwa kusimamisha uchapishaji usiokuwa na mpaka wakati padi imefikisha kikomo chake. Kuhitajika kwake na mara inayohitajika kutatofautiana kulingana na idadi ya kurasa unazochapisha ukitumia chaguo la kuchapisha bila kingo. Kuhitajika kwa ubadilishaji wa padi hakumaanishi kwamba printa yako imewacha kufanya kazi kulingana na sifa zake. Printa itakuarifu wakati padi inahitajika kubadilishwa na jambo linaweza tu kufanywa na Mtoa huduma aliyeidhinishwa na Epson. Udhamini wa Epson hausimamii gharama ya ubadilishaji huu.

# Karatasi Zinakwama

Angalia hitilafu inayoonyeshwa kwenye paneli dhibiti na ufuate maelekezo ili uondoe karatasi iliyokwama ikiwa ni pamoja na vipande vilivyoraruka. Bkisha, futa hitilafu.

***Muhimu:***

- *Ondoa karatasi iliyokwama kwa uangalifu. Kuondoa karatasi kwa nguvu kunaweza kusababisha uharibifu wa printa.*
- *Wakati unaondoa karatasi iliyokewama, epuka kuinamisha kichapishi, usikiweke wima, au kuigeuza upande wa chini kuangalia juu; la sivyo wino utavuja.*

## Kuondoa Karatasi Iliyokwama

***Tahadhari:***

- *Chunga mkono au vidole vyako visikwame wakati unafungua au kufunga kitengo cha kitambazaji. La sivyo unaweza kujeruhiwa.*
- *Usiwahi kugusa vitufe vilivyo kwenye paneli dhibiti wakati mkono wako uko ndani ya kichapishi. Ikiwa kichapishi kitaanza kufanya kazi, inaweza kusababisha majeraha. Kuwa makini usiguse sehemu zinazojitokeza ili uzuie majeraha.*

1. Ondoa kifuniko cha nyuma.



2. Ondoa karatasi iliyokwama.



3. Ondoa Karatasi Iliyokwama kutoka kwa kifuniko cha nyuma.



4. Ingiza kifuniko cha nyuma kwenye printa.

5. Funga kifuniko cha waraka iwako kiko wazi.

6. Fungua kitengo cha kitambazaji kwa mikono miwili hadi kijifunge.



7. Ondoa karatasi iliyokwama.



> **Muhimu:**
>
> *Usiguze kebo nyeupe bapa, sehemu angavu, na tyubu za wino zilizo ndani ya kichapishi. Ukifanya hivyo unaweza kusababisha hitalifu.*
>
> 

8. Funga kitengo cha kitambazaji.



> ***Kumbuka:***
> *Kitengo cha kitambazaji kimeundwa ili kufunga taratibu na kukataa kidogo kama kuzuia vidole vyako kukamatwa. Endelea kufunga hata ikiwa unahisi inakataa kidogo.*

## Kuondoa Karatasi Iliyokwama kutoka kwa ADF

1. Fungua kifuniko cha ADF.



2. Ondoa karatasi iliyokwama.



3. Inua trei ya ingizo ya ADF.

> ***Muhimu:***
>
> *Hakikisha umefungua kifuniko cha ADF kabla ya kuinua trei ya ingizo ya ADF. Vinginevyo, huenda ADF ikaharibika.*



4. Ondoa karatasi iliyokwama.



5. Shusha trei ya ingizo ya ADF.



6. Fungua kifuniko cha ADF hadi kitoe mbofyo.



## Kuzuia Karatasi Kukwama

Angalia yafuatayo ikiwa karatasi zinakwama mara kwa mara.

❏ Weka printa kwenye eneo tambarare na uitumie katika hali ya mazingira iliyopendekezwa.
  "Sifa za Kimazingira" kwenye ukurasa wa 285

❏ Tumia karatasi inayotumika katika kichapishi hiki.
  "Karatasi Inayopatikana na Uwezo" kwenye ukurasa wa 250

❏ Fuata maagizo ya kushughilikia karatasi.
  "Tahadhari za Kushughulikia Karatasi" kwenye ukurasa wa 30

❏ Weka karatasi ikiwa inaangalia upande unaofaa, na telezesha mwongozo wa kingo kando ya kingo ya karatasi.
  "Kuweka Karatasi" kwenye ukurasa wa 32

❏ Usipakie laha zaidi ya idadi ya juu zaidi iliyobainishwa kwa karatasi.

❏ Weka karatasi moja ya karatasi kwa wakati mmoja unapopakia karatasi nyingi.

❏ Hakikisha mipangilio ya ukubwa wa karatasi na aina ya karatasi inalingana na ukubwa halisi wa karatasi na aina ya karatasi iliyopakiwa kwenye kichapishi.
  "Orodha ya Aina za Karatasi" kwenye ukurasa wa 31

❏ Safisha kibiringizaji ndani ya kichapishi.
  "Kusafisha Kijia cha Karatasi kwa Matatizo ya Kuingiza Karatasi" kwenye ukurasa wa 112

# Ni Wakati wa Kujaza tena Wino

## Tahadhari za Kushughulikia Chupa ya Wino

Soma maelekezo yafuatayo kabla ya kujaza wino upya.

### Kuhifadhi tahadhari kwa wino

❏ Weka chupa za wino nje ya mwale wa jua wa moja kwa moja.

❏ Usihifadhi chupa za wino katika halijoto za juu au zinazoganda.

❏ Epson inapendekeza utumie chupa ya wino kabla ya tarehe iliyochapishwa kwenye pakiti.

- Wakati wa kuhifadhi au kusafirisha chupa ya wino, usiinamishe chupa na usiigongeshe au kuiweka mahali penye mabadiliko ya hali joto.La sivyo, wino unaweza kuvuja hata kama kifuniko kilicho kwenye chupa ya wino kimekazwa vizuri.Hakikisha umeweka chupa ya wino ikiwa imesimama wakati unakaza kifuniko, na utahadhari ili uzuie wino usivuje wakati unasafirisha chupa, kwa mfano, kuweka chupa kwenye mkoba.
- Baada ya kuleta chupa ya wino ndani kutoka eneo baridi la uhifadhi, iwache ipate joto katika halijoto ya chumba kwa angalau saa tatu kabla ya kuitumia.
- Usifungue pakiti ya chupa ya wino hadi uwe tayari kujaza tangi la wino.Chupa ya wino hupakiwa bila hewa ili kudumisha utumikaji wake.Ukiwacha chupa ya wino bila kuipakia kwa muda mrefu kabla ya kuitumia, uchapishaji wa kawaida huenda usiwezekane.
- Pindi unapofungua chupa ya wino, tunapendekeza uitumie haraka iwezekanavyo.

#### Kushughulikia tahadhari kwa kujaza wino

- Ili uhakikishe unapokea ubora wa juu wa uchapishaji na kusaidia kulinda kichwa chako ya kuchapisha, akiba tofauti ya usalama ya wino hubakia katika tangi wakati printa yako inakuonyesha unafaa ujaze wino upya.Viwango vilivyoandikwa havijumuishi akiba hii.
- Kwa matokeo bora ya kuchapisha usitumie viwango vya wino vilivyo chini kwa vipindi virefu vya muda.
- tumia chupa za wino zilizo na msimbo sahihi wa sehemu ya printa hii.
- Wino wa kichapishi hiki unafaa kushughulikiwa kwa uangalifu. Wino unaweza kumwagika wakati matanki ya wino yamejazwa au kujazwa upya na wino. Ikiwa wino utamwagikia nguo au vitu vyako, huenda usitoke.
- Usitingishe haraka zaidi au kufinyaza chupa za wino.
- Kuendelea kutumia printa kwa muda mrefu wakati kiwango cha wino kiko chini ya laini ya chini kunaweza kuharibu printa. Jaza tanki la wino hadi mstari wa juu wakati kichapishi hakifanyi operesheni. Ili kuonyesha makadirio sahihi ya kiwango cha wino, weka upya kiwango cha wino baada ya kujza tanki.
- Ili upate matokeo mazuri ya uchapishaji, jaza upya matangi ya wino hadi mstari wa juu angalau mara moja kwa mwaka.

#### Matumizi ya wino

- Ili kudumisha utendaji mzuri wa kichwa cha kuchapisha, kiasi fulani cha wino hutumiwa kutoka kwenye tanki zote wakati wa operesheni za matengenezo kama vile usafishaji wa kichwa cha kuchapisha. Huenda pia wino ukatumika unapowasha kichapishi.
- Wakati unachapisha rangi moja au kijivujivu, wino wa rangu badala ya wino mweusi unaweza kutumiwa kulingana na aina ya karatasi au mipangilio ya ubora wa uchapishaji. Hii ni kwa sababu mchanganyiko wa wino wa rangu unatumiwa kutengeneza rangi nyeusi.
- Kiasi fulani cha wino ulio ndani ya chupa za wino ulikuja na printa yako hutumiwa wakati wa usanidi wa mwanzo.Ili uchapishe nakala za hali ya juu, kichwa cha kuchapisha kilicho katika printa yako kitajazwa wino.Mchakato huu wa mara moja hutumia kiasi cha wino na basi chupa hizi zinaweza kuchapisha kurasa chache kulingana na chupa za wino zitakazofuata.
- Viwango viliandikwa vinaweza kuwa tofauti kulingana na picha unazochapisha, aina ya karatasi unayotumia, marudio ya uchapishaji na hali ya mazingisa kama vile halijoto.
- Angalia kwa macho viwango vya wino katika matangi halisi ya wino. Kuendelea kutumia kichapishi wakati wino umetumika kunaweza kuharibu kichapishi. Epson inapendekea ujaze tangi la wino hadi mstari wa juu wakati printa haitumiki ili uweke kiwango cha wino upya.

## Kujaza Matangi ya Wino Upya

1. Funga kifuniko cha waraka iwako kiko wazi.

2. Fungua kitengo cha kitambazaji kwa mikono miwili hadi kijifunge.



3. Fungua kifuniko cha tanki la wino.



Soma tahadhari za matumizi za kujaza wino kwenye skrini, na kisha uende kwenye skrini inayofuata.

4. Funga kifuniko kilicho kwenye tanki la wino.



> **Muhimu:**
>
> *Hakikisha kwamba rangi ya tangi la wino inalingana na rangi ya wino unayotaka kujaza upya.*

5. Unaposhikilia chupa ya wino wima, geuza kifuniko polepole ili kukiondoa.



> **Muhimu:**
>
> - *Epson inapendekeza utumie chupa halali za wino za Epson.*
> - *Chunga usimwage wino wowote.*

6. Angalia mstari wa juu (a) kwenye tanki la wino.




7. Pangilia upande wa juu wa chupa ya wino kwa kituo cha kujaza, na kisha uichomeke wima kwenye kituo cha kujaza wino hadi usitishe kiotomatiki kwenye mstari wa juu.

   Unapochomeka chupa ya wino kwenye kituo cha kujaza kwa rangi sahihi, wino huanza kumwagika na mtiririko husitishwa kiotomatiki wakati wino hufikia mstari wa juu.

Iwapo wino hautaanza kutiririka kwenye tanki, ondoa chupa ya wino na ujaribu kuichomeka tena. Hata hivyo, usichomeke upya chupa ya wino wakati wino umefikia mstari wa juu zaidi; vinginevyo wino unaweza kuvuja.



8. Unapokamilisha kujaza wino, ondoa chupa ya wino.

> **Muhimu:**
>
> *Usiache chupa ya wino kama imechomekwa; vinginevyo huenda chupa ikaharibika au wino unaweza kumwagika.*

***Kumbuka:***
*Iwapo wino wowote utasalia kwenye chupa ya wino, kaza kifuniko na uhifadhi cvhupa ikisimama kwa matumizi ya baadaye.*



9. Funga kifuniko cha tanki la wino kwa usalama.




10. Funga kifuniko cha tanki la wino kabisa.



11. Funga kitengo cha kitambazaji.



*Kumbuka:*
*Kitengo cha kitambazaji kimeundwa ili kufunga taratibu na kukataa kidogo kama kuzuia vidole vyako kukamatwa. Endelea kufunga hata ikiwa unahisi inakataa kidogo.*

12. Fuata maagizo ya kwenye skrini ili kuweka kiwango cha wino kwa rangi ya wino uliojazwa upya.

> *Muhimu:*
> *Hata kama hutajaza wino hadi mstari wa juu wa tanki la wino, unaweza kuendelea kutumia kichapishi. Ili kufanya kichapishi chako kiendelee kufanya kazi kwa hali nzuri, hata hivyo, jaza upya tanki la wino hadi mstari wa juu na kisha uweke upya viwango vya wino mara moja.*

**Maelezo Husika**

➡ “Misimbo ya Chupa ya Wino” kwenye ukurasa wa 253
➡ “Tahadhari za Kushughulikia Chupa ya Wino” kwenye ukurasa wa 197
➡ “Kusafisha Wino Uliomwagika” kwenye ukurasa wa 127

## Vidokezo vya Kuweka upya Kiwango cha Wino

Hakikisha umeweka upya kiwango cha wino baada ya kujaza upya wino.

Ikiwa ulijaza upya rangi mbili au zaidi, unahitaji kuchagua rangi zote ambazo ulijaza upya na uweke upya kiwango cha wino.

Isipokuwa uweke upya kiwango cha wino, kiwango cha wino kilichoonyeshwa hakibadiliki hata baada ya kujaza upya wino.

**Maelezo Husika**

➡ “Kuangalia Hali ya Vitumika” kwenye ukurasa wa 112

# Ni wakati wa Kubadilisha Kikasha cha Matengenezo

## Tahadhari za Kushughulikia Kisanduku cha Ukarabati

Soma maagizo yafuatayo kabla ya kubadilisha kisanduku cha ukarabati.

- Usiguse chipu ya kijani iliyo upande wa kando wa kisanduku cha ukarabati. Kufanya hivyo kunaweza kuzuia utendaji na uchapishaji wa kawaida.
- Usiangushe kisanduku cha ukarabati au ukiweke kwenye mishtuko ya ajabu.
- Usibadilishe kisanduku cha ukarabati wakati wa uchapishaji; la sivyo, wino unaweza kuvuja.
- Usiondoe kisanduku cha ukarabati na kifuniko chake isipokuwa unapobadilisha kisanduku cha ukarabati; la sivyo wino unaweza kuvuja.
- Wakati kifuniko hakiwezi kuaambatishwa tena, huenda kikasha cha matengenezo kisisakinishwe vilivyo. Ondoa kikasha cha matengenezo, na ukisakinishe upya.
- Usiinamishe kisanduku cha ukarabati kilichotumiwa hadi kifungiwe ndani ya mfuko wa plastiki; la sivyo wino unaweza kuvuja.
- Usiguse sehemu zilizo wazi kwenye kikasha cha matengenezo kwa kuwa unaweza kujipaka wino.
- Usitumie upya kisanduku cha ukarabati ambacho kimeondokewa na kutotumiwa kwa muda mrefu. Wino ndani ya kisanduku hicho umekauka na hakuna wino zaidi unaweza kunyonywa.
- Weka kisanduku cha ukarabati mbali na mwale wa jua wa moja kwa moja.
- Usihifadhi kisanduku cha ukarabati katika halijoto za juu au zinazoganda.

## Kubadilisha Kisanduku cha Ukarabati

Katika mizunguko fulani ya uchapishaji viango vidogo vya wino wa ziada vinaweza kukusanywa katika kisanduku cha ukarabati. Ili uzuie uvujaji wa wino kutoka kwa kisanduku cha ukarabati, printa imeundwa kusimamisha uchapishaji wakati uwezo wa kunyonya wa kisanduku cha ukarabati imefikisha kikomo chake. Kuhitajika kwake na mara inayohitajika kutatofautiana kulingana na idadi ya kurasa unazochapisha, aina ya nyenzo unayochapisha na idadi ya mizunguko ya usafisha ambayo printa inafanya.

Wakati ujumbe unaonyeshwa ukikuomba kubadilisha kisanduku cha ukarabati, rejelea uhuishaji unaonyeshwa kwenye paneli ya udhibiti. Kuhitajika kwa ubadilishaji wa kisanduku hakumaanishi kwamba printa yako imewacha kufanya kazi kulingana na sifa zake. Udhamini wa Epson hausimamii gharama ya ubadilishaji huu. Ni sehemu inayokarabatiwa na mtumiaji.



***Kumbuka:***
- *Wakati kikasha cha matengenezo kimejaa, huwezi kuchapisha au kusafisha kichwa cha kuchapisha hadi kibadilishwe ili kuzuia umwagikaji wa wino. Hata hivyo, unaweza kutenda shughuli zisizotumia wino kama vile utambazaji.*
- *Wakati skrini inayofuata imeonyeshwa, sehemu haiwezi kubadilishwa na watumiaji. Wasiliana na usaidizi wa Epson.*




**Maelezo Husika**

➡ "Msimbo wa Kisanduku cha Ukarabati" kwenye ukurasa wa 254
➡ "Tahadhari za Kushughulikia Kisanduku cha Ukarabati" kwenye ukurasa wa 204

# Ubora wa Kuchapisha, Kunakili na Kutambaza ni Duni

## Ubora wa Uchapishaji Uko Chini

### Rangi Haipo, Uungnishaji au Rangi Zisizotarajiwa Zinaonekana kwenye Chapisho




#### Huenda nozeli za kichwa cha kuchapisha zimeziba.

**Suluhisho**

- Fanya ukaguzi wa nozeli ili kuona ikiwa nozeli za kichwa cha kuchapisha zimeziba. Fanya ukaguzi wa nozeli, na kisha usafishe kichwa cha kuchapisha ikiwa nozeli zozote za kichwa cha kichapisha zitaziba. Ikiwa hujatumia kichapishi chako kwa muda mrefu, nozeli za kichwa cha kichapishi zinaweza kuziba na huenda matone ya wino yakatoka.
- Iwapo ulichapisha wakati kiwango cha wino kilikuwa chini zaidi kuonekana kwenye madirisha ya tangi la wino, jaza upya tangi za wino hadi kwenye mistari ya juu na kisha utumie huduma ya **Usafishaji wa Nishati** ili kubadilisha wino ndani ya tyubu za wino. Baada ya kutumia huduma hiyo, fanya ukaguzi wa nozeli ili kuona iwapo ubora wa chapisho umeimarika.

➡ "Kukagua na Kusafisha Kichwa cha Kuchapisha" kwenye ukurasa wa 115

➡ “Kuendesha Usafishaji wa Nishati” kwenye ukurasa wa 117

## Ubora wa Uchapishaji ni Duni kwa Wino Nyeusi




### Huenda nozeli za kichwa cha kuchapisha zimeziba.

**Suluhisho**

- Fanya ukaguzi wa nozeli ili kuona ikiwa nozeli za kichwa cha kuchapisha zimeziba. Fanya ukaguzi wa nozeli, na kisha usafishe kichwa cha kuchapisha ikiwa nozeli zozote za kichwa cha kichapisha zitaziba. Ikiwa hujatumia kichapishi chako kwa muda mrefu, nozeli za kichwa cha kuchapishai zinaweza kuziba na huenda matone ya wino yakatoka.

  “Kukagua na Kusafisha Kichwa cha Kuchapisha” kwenye ukurasa wa 115

- Iwapo huwezi kutatua tatizo kwa kutumia usafishaji wa kichwa, unaweza kuchapisha mara moja kwa mchanganyiko wa rangi ya wino ili kuunda nyeusi kwa kubadilisha mipangilio ifuatayo katika Windows.

  Bofya **Mipangilio Iliyorefushwa** kwenye kichupo cha kienfdeshi cha kichapishi cha **Utunzaji**. Iwapo utateua **Use a Mixture of Color Inks to Create Black**, unaweza kuchapisha katika ubora **Wastani** wa kuchapisha wakati **Aina ya Krtasi** ni **Karatasi tupu**, **Letterhead**, au **Bahasha**.

  Kumbuka kwamba kipengele hiki hakiwezi kutatua kufungana kwa tundu. Ili kutatua kufungana kwa tundu, tunapendekeza kuwasiliana na msaada wa Epson kwa ukarabati.

## Mistari wa Rangi Hutokea kati ya Umbali wa Takriban 3.3 cm



Sababu zifuatazo zinaweza kuzingatiwa.

### Mipangilio ya aina ya karatasi hailingani na karatasi iliyopakiwa.

**Suluhisho**

Teua mpangilio unaofaa wa aina ya karatasi kwa aina ya karatasi iliyopakiwa katika kichapishi.

➡ “Orodha ya Aina za Karatasi” kwenye ukurasa wa 31

### Ubora wa chapisho umewekwa kuwa chini.

**Suluhisho**

Unapochapisha kwenye karatasi tupu, chapisha kwa kutumia mpangilio wa ubora wa juu.

- Windows

  Teua **Juu** kutoka **Ubora** kwenye kichapishi cha kichupo cha **Kuu**.

- Mac OS

  Teua **Nzuri** kama **Print Quality** kutoka kwenye menyu ya kidirisha cha **Mipangilio ya Kuchapisha**.

### Mkao wa Kichwa cha kuchapisha haujaoana.

**Suluhisho**

Teua menyu ya **Matengenezo** > **Ulainishaji Kichwa** > **Upangiliaji Kimlalo** kwenye paneli dhibiti ili kuoanisha kichwa cha kuchapisha.

## Machapisho Yasiyoonekana Vizuri, Mstari Wima, au Ulinganishaji visivyo





Sababu zifuatazo zinaweza kuzingatiwa.

### Mkao wa kichwa cha kuchapisha haujaoana.

**Suluhisho**

Teua menyu ya **Matengenezo** > **Ulainishaji Kichwa** > **Ulainishaji Wima** kwenye paneli dhibiti ili kuoanisha kichwa cha kuchapisha.

### Mpangilo wa uchapishaji wa pande mbili umelemazwa.

**Suluhisho**

Ikiwa ubora wa chapisho hautaimarika hata baada ya kulinganisha kichwa, lemaza mpangilio wa uchapishaji wa pande mbili.

Wakati wa uchapishaji wa pande mbili (au kasi ya juu), kichwa cha kuchapisha huchapisha kikisogea pande zote mbili, na mistari wima huenda ikakosa kulingana. Kulemaza mipangilio huenda kukapunguza kasi ya uchapishaji lakini kukaimarisha ubora wa chapisho.

- Windows

  Futa **Uchapishaji katika mielekeo miwili** iliyo kwenye kichupo cha kiendesha kichapishi cha **Chaguo Zaidi**.

- Mac OS

  Teua **Mapendeleo ya Mfumo** kwenye menyu ya Apple > **Vichapishaji na Vitambazaji** (au **Chapisha na Utambaze**, **Chapisha na Utume Faksi**), na kisha uteue kichapishaji. Bofya **Chaguo na Vifaa** > **Chaguo** (au **Kiendeshi**). Teua **Off** kama mpangilio wa **Uchapishaji katika mielekeo miwili**.

## Chapa Inatoka Kama Karatasi Tupu



### Huenda nozeli za kichwa cha kuchapisha zimeziba.

**Suluhisho**

Fanya ukaguzi wa nozeli na kisha ujaribu Usafishaji wa Nishati ili kuona ikiwa nozeli za kichwa cha kuchapisha zimeziba.

➡ "Kukagua na Kusafisha Kichwa cha Kuchapisha" kwenye ukurasa wa 115
➡ "Kuendesha Usafishaji wa Nishati" kwenye ukurasa wa 117

### Mipangilio ya uchapishaji na ukubwa wa karatasi iliyopakiwa kwenye kichapishi ni tofauti.

**Suluhisho**

Badilisha mipangilio ya kichapishi kulingana na ukubwa wa karatasi iliyopakiwa kwenye kichapishi. Pakia karatasi kwenye kichapishi inayolingana na mipangilio ya uchapishaji.

### Laha nyingi za karatasi zimelishwa kwenye kichapishi kwa wakati mmoja.

**Suluhisho**

Angalia yafuatayo ili kuzuia laha nyingi za karatasi kulishwa kwenye kichapishi kwa wakati mmoja.

➡ "Karatasi Kadhaa Kuwekwa Moja baada ya Nyingine" kwenye ukurasa wa 142

## Karatasi Imechafuka au Imechakaa



Sababu zifuatazo zinaweza kuzingatiwa.

### Karatasi haijapakiwa ipasavyo.

**Suluhisho**

Uunganishaji mlalo (mtagusano wa pembe 90 kwa mwelekeo wa uchapishaji) unapoonekana, au shemu ya juu au ya chini imepakwa, pakia karatasi kwenye mwelekeo ufaao na utelezeshe miongozo ya kingo hadi kwenye kingo za karatasi.

➡ "Kuweka Karatasi" kwenye ukurasa wa 32

### Njia ya karatasi imepakwa.

**Suluhisho**

Uunganishaji wima (mlalo kwa mwelekeo wa uchapishaji) ukionekana, au karatasi ikipakwa, safisha njia ya karatasi.

➡ “Kusafisha Kijia cha Karatasi na Umwagikaji wa Wino” kwenye ukurasa wa 119

### Karatasi imekunja.

**Suluhisho**

Weka karatasi katika eneo laini ili kuangalia iwapo imejikunja. Iwapo ndivyo, ilainishe.

### Kichwa cha kuchapisha kinasugua eneo la karatasi.

**Suluhisho**

Wakati unachapisha katika karatasi nono, kichwa cha chapisho kiko karibu na eneo la uchapishaji na karatasi inaweza kuchafuliwa. Katika hali hii, wezeshga mpangilio wa kupunguza uchafu. Ukiwasha mpangilio huu, ubora wa uchapishaji unaweza kupungua au uchapishaji unaweza kuwa na kasi ya chini.

Windows

Bofya **Mipangilio Iliyorefushwa** kwenye kichupo cha kiendeshi cha kichapishi **Utunzaji**, na kisha uteue **Karatasi ya Punje Fupi**.

### Sehemu ya nyuma ya karatasi ilichapishwa kabla ya upande ambao tayari ulikuwa umechapishwa kukauka.

**Suluhisho**

Unapofanya uchapishaji wa pande 2 mwenyewe, hakikisha kwamba wino umekauka kabisa kabla ya kupakia karatasi upya.

### Ukichapisha kwa kutumia uchapishaji wa pande 2 otomatiki, uzito wa chapisho ni wa juu zaidi na wakati wa kukauka ni mfupi mno.

**Suluhisho**

Wakati unatumia kipengele cha uchapishaji wa pande 2 na kuchapisha data ya uzito wa juu kama vile picha na grafu, weka uzito wa uchapishai kwa chini na muda wa kukauka kwa refu.

➡ “Kuchapisha Pande 2” kwenye ukurasa wa 39
➡ “Kuchapisha Pande 2” kwenye ukurasa wa 58

## Picha Zilizochapishwa Zinanata



### Chapisho lilifanywa kwenye upande mbaya wa karatasi ya picha.

**Suluhisho**

Hakikisha kuwa unachapisha kwenye upande unaochapishika. Unapochapisha kwenye upande usiofaa wa karatasi ya picha, unahitaji kusafisha njia ya karatasi.

➡ "Kusafisha Kijia cha Karatasi na Umwagikaji wa Wino" kwenye ukurasa wa 119

## Picha Zinachapishwa katika Rangi Zisizotarajiwa



Sababu zifuatazo zinaweza kuzingatiwa.

### Huenda nozeli za kichwa cha kuchapisha zimeziba.

**Suluhisho**

Fanya ukaguzi wa nozeli ili kuona ikiwa nozeli za kichwa cha kuchapisha zimeziba. Fanya ukaguzi wa nozeli, na kisha usafishe kichwa cha kuchapisha ikiwa nozeli zozote za kichwa cha kichapisha zitaziba. Ikiwa hujatumia kichapishi chako kwa muda mrefu, nozeli za kichwa cha kichapishi zinaweza kuziba na huenda matone ya wino yakatoka.

### Marekebisho ya Rangi yamewekwa.

**Suluhisho**

Unapochapisha kutoka kwenye kiendeshi cha kichapishi cha Windows, mpangilio wa urekebishaji picha kiotomatiki wa Epson unatekelezwa kwa chaguo-msingi kulingana na aina ya karatasi. Jaribu kubadilisha mpangilio.

Kwenye kichupo cha **Chaguo Zaidi**, teua **Kaida** kwenye **Usahihishaji wa Rangi**, na kisha ubofye **Iliyoboreshwa**. Badilisha mpangilio wa **Usahihishaji wa Eneo** kutoka **Otomatiki** hadi chaguo jingine lolote. Iwapo kubadilisha mpangilio hakufanyi kazi, tumia mbinu yoyote ya marekebisho ya rangi kando na **Ubora Picha** kwenye **Usimamiaji wa Rangi**.

➡ "Kurekebisha Rangi ya Uchapishaji" kwenye ukurasa wa 54

## Haiwezi Kuchapisha Bila Pambizo



### Hujaweka mipangilio ya uchapishaji usio na mpaka.

**Suluhisho**

Weka mpangilio wa uchapishaji usio na mpaka katika mipangilio ya kichapishi. Ukiteua aina ya karatasi isiyotumia uchapishaji usio na mpakaы, huwezi kuteua **Isiyo na kingo**. Teua aina ya karatasi inayotumia uchapishaji usio na mpaka.

- Windows

  Teua **Isiyo na kingo** kwenye kichupo cha **Kuu** cha kiendeshi cha kichapishi.

- Mac OS

  Chagua ukubwa wa karatasi usio na mpaka kutoka **Ukbwa wa Krtasi**.

➡ "Karatasi la Kuchapishwa Bila Mipaka" kwenye ukurasa wa 251

## Kingo za Picha Zinakatwa Wakati wa Uchapishaji wa Bila Mpaka



### Kwa sababu taswira imepanuliwa kidogo, sehemu inayochomoza inapogolewa.

**Suluhisho**

Teua mpangilio mdogo wa upanuaji.

- Windows

  Bofya **Mipangilio** karibu na kisanduku tiki **Isiyo na kingo** kwenye kichupo cha kiendeshi cha kichapishi **Kuu**, kisha ubadilishe mipangilio.

- Mac OS

  Rekebisha mpangilio wa **Ukuzaji** kutoka kwenye menyu ya **Mipangilio ya Kuchapisha** ya mawasiliano ya uchapishaji.

## Mkao, Ukubwa, au Pambizo za Uchapishaji Sio Sahihi



Sababu zifuatazo zinaweza kuzingatiwa.

### Karatasi imepakiwa visivyo.

**Suluhisho**

Weka karatasi ikiwa inaangalia upande unaofaa, na telezesha mwongozo wa kingo kando ya kingo ya karatasi.

➡ "Kuweka Karatasi" kwenye ukurasa wa 32

### Ukubwa wa karatasi haujawekwa ipasavyo.

**Suluhisho**

Teua mpangilio wa ukubwa wa karatasi unaofaa.

### Mpangilio wa pambizo katika programu hauko katika sehemu ya uchapishaji.

**Suluhisho**

Rekebisha mpangilio wa pambizo katika programu ili iingie katika sehemu inayoweza kuchapishwa.

➡ "Eneo Linaloweza Kuchapishwa" kwenye ukurasa wa 278

## Herufi Zilizochapishwa Sio Sahihi au Zimechanganywa



Sababu zifuatazo zinaweza kuzingatiwa.

### Kebo ya USB haijaunganishwa ipasavyo.

**Suluhisho**

Unganisha kebo ya USB vizuri kwenye kichapishi na kompyuta.

### Kuna shughuli inayosuburi kuchapishwa.

**Suluhisho**

Katisha uchapishaji wowote uliositishwa.

### Kompyuta imewekwa kwa modi ya Sinzia au Lala huku ikichapisha.

**Suluhisho**

Usiweke kompyuta kwenye modi ya **Sinzia** au modi ya **Lala** mwenyewe wakati wa kuchapisha. Kurasa za maandishi yaliyochanganywa huenda yakachapishwa wakati ujao unapowasha kompyuta.

### Unatumia kiendeshi cha kichapishi kwa kichapishi tofauti.

**Suluhisho**

Hakikisha kiendeshi cha kichapishi unachotumia ni cha kichapishi hiki. Angalia jina la kichapishi upande wa juu wa dirisha la kiendeshi cha kichapishi.

## Picha Iliyochapishwa Imegeuzwa




### Picha imewekwa ili kupinduka mlalo kwenye mipangilio ya chapisho.

**Suluhisho**

Futa mipangilio yoyote ya picha akisi katika kiendeshi cha printa au programu.

- Windows

  Futa **Taswira ya Kioo** iliyo kwenye kichupo cha kiendesha kichapishi cha **Chaguo Zaidi**.

- Mac OS

  Futa **Mirror Image** kutoka kwa menyu ya **Mipangilio ya Kuchapisha** ya mawasiliano ya uchapishaji.

## Ruwaza Zinazoonekana kama Micoro kwenye Machapisho



### Taswira au picha zenye ubainifu wa chini zilichapishwa.

**Suluhisho**

Wakati unachapisha taswira aui picha, chapisha ukitumia data yenye ubainifu wa juu. Taswira kwenye tovuti huwa na ubainifu wa chini ingawa zinaonekana vyema kidogo zikionyeshwa na kwa hivyo ubora wa uchapishaji unaweza kudorora.

# Ubora wa Nakala ni wa chini

## Rangi Haipo, Kufunga au Rangi Zisizotarajiwa Zinaonekana kwenye Nakala




### Huenda nozeli za kichwa cha kuchapisha zimeziba.

**Suluhisho**

- Fanya ukaguzi wa nozeli ili kuona ikiwa nozeli za kichwa cha kuchapisha zimeziba. Fanya ukaguzi wa nozeli, na kisha usafishe kichwa cha kuchapisha ikiwa nozeli zozote za kichwa cha kichapisha zitaziba. Ikiwa hujatumia kichapishi chako kwa muda mrefu, nozeli za kichwa cha kichapishi zinaweza kuziba na huenda matone ya wino yakatoka.
- Iwapo ulichapisha wakati kiwango cha wino kilikuwa chini zaidi kuonekana kwenye madirisha ya tangi la wino, jaza upya tangi za wino hadi kwenye mistari ya juu na kisha utumie huduma ya **Usafishaji wa Nishati** ili kubadilisha wino ndani ya tyubu za wino. Baada ya kutumia huduma hiyo, fanya ukaguzi wa nozeli ili kuona iwapo ubora wa chapisho umeimarika.

➡ "Kukagua na Kusafisha Kichwa cha Kuchapisha" kwenye ukurasa wa 115
➡ "Kuendesha Usafishaji wa Nishati" kwenye ukurasa wa 117

## Mistari wa Rangi Hutokea kati ya Umbali wa Takriban 3.3 cm



Sababu zifuatazo zinaweza kuzingatiwa.

### Mipangilio ya aina ya karatasi hailingani na karatasi iliyopakiwa.

**Suluhisho**

Teua mpangilio unaofaa wa aina ya karatasi kwa aina ya karatasi iliyopakiwa katika kichapishi.

➡ "Orodha ya Aina za Karatasi" kwenye ukurasa wa 31

### Ubora wa chapisho umewekwa kuwa chini.

**Suluhisho**

Unapochapisha kwenye karatasi tupu, chapisha kwa kutumia mpangilio wa ubora wa juu.

Teua **Juu** kwenye **Ubora**.

### Mkao wa Kichwa cha kuchapisha haujaoana.

**Suluhisho**

Teua menyu ya **Matengenezo** > **Ulainishaji Kichwa** > **Upangiliaji Kimlalo** kwenye paneli dhibiti ili kuoanisha kichwa cha kuchapisha.

## Nakala zisizoonekana, Mstari wima au Ulinganishaji visivyo



Sababu zifuatazo zinaweza kuzingatiwa.

### Mkao wa kichwa cha kuchapisha haujaoana.

**Suluhisho**

Teua menyu ya **Matengenezo** > **Ulainishaji Kichwa** > **Ulainishaji Wima** kwenye paneli dhibiti ili kuoanisha kichwa cha kuchapisha.

## Chapa Inatoka Kama Karatasi Tupu



### Huenda nozeli za kichwa cha kuchapisha zimeziba.

**Suluhisho**

Fanya ukaguzi wa nozeli na kisha ujaribu Usafishaji wa Nishati ili kuona ikiwa nozeli za kichwa cha kuchapisha zimeziba.

➡ "Kukagua na Kusafisha Kichwa cha Kuchapisha" kwenye ukurasa wa 115
➡ "Kuendesha Usafishaji wa Nishati" kwenye ukurasa wa 117

### Mipangilio ya uchapishaji na ukubwa wa karatasi iliyopakiwa kwenye kichapishi ni tofauti.

**Suluhisho**

Badilisha mipangilio ya kulingana na ukubwa wa karatasi iliyopakiwa kaenye kaseti ya karatasi. Pakia karatasi inayolingana na mipangilio ya uchapishaji kwenye kaseti ya karatasi.

### Laha nyingi za karatasi zimelishwa kwenye kichapishi kwa wakati mmoja.

**Suluhisho**

Angalia yafuatayo ili kuzuia laha nyingi za karatasi kulishwa kwenye kichapishi kwa wakati mmoja.

➡ "Karatasi Kadhaa Kuwekwa Moja baada ya Nyingine" kwenye ukurasa wa 142

## Karatasi Imechafuka au Imechakaa



Sababu zifuatazo zinaweza kuzingatiwa.

### Karatasi haijapakiwa ipasavyo.

**Suluhisho**

Uunganishaji mlalo (mtagusano wa pembe 90 kwa mwelekeo wa uchapishaji) unapoonekana, au shemu ya juu au ya chini imepakwa, pakia karatasi kwenye mwelekeo ufaao na utelezeshe miongozo ya kingo hadi kwenye kingo za karatasi.

➡ "Kuweka Karatasi" kwenye ukurasa wa 32

### Njia ya karatasi imepakwa.

**Suluhisho**

Uunganishaji wima (mlalo kwa mwelekeo wa uchapishaji) ukionekana, au karatasi ikipakwa, safisha njia ya karatasi.

➡ "Kusafisha Kijia cha Karatasi na Umwagikaji wa Wino" kwenye ukurasa wa 119

### Karatasi imekunja.

**Suluhisho**

Weka karatasi katika eneo laini ili kuangalia iwapo imejikunja. Iwapo ndivyo, ilainishe.

## Haiwezi Kunakili Bila Pambizo



### Hujaweka mipangilio ya uchapishaji usio na mpaka.

**Suluhisho**

Teua **Nakili** > **Mipangilio Mahiri** > **Nakala Isiyo na mipaka**, na kisha uwezeshe mpangilio. Iwapo umechagua karatasi ambayo haitumii uchapishaji usio na mpaka, huwezi kuwezesha mipangilio ya uchapishaji usio na mpaka. Teua aina ya karatasi inayotumia uchapishaji usio na mpaka.

➡ "Karatasi la Kuchapishwa Bila Mipaka" kwenye ukurasa wa 251

## Kingo za Taswira Zinapogolewa Wakati wa Kuchapisha Bila Mipaka



### Kwa sababu taswira imepanuliwa kidogo, sehemu inayochomoza inapogolewa.

**Suluhisho**

Teua mpangilio mdogo wa upanuaji.

Teua **Nakili** > **Mipangilio Mahiri** > **Nakala Isiyo na mipaka** > **Upanuzi** kwenye paneli dhibiti, na kisha ubadlishe mpangilio.

## Mkao, Ukubwa au Pambizo za Nakala si Sahihi



Sababu zifuatazo zinaweza kuzingatiwa.

### Karatasi imepakiwa visivyo.

**Suluhisho**

Weka karatasi ikiwa inaangalia upande unaofaa, na telezesha mwongozo wa kingo kando ya kingo ya karatasi.

➡ "Kuweka Karatasi" kwenye ukurasa wa 32

### Ukubwa wa karatasi haujawekwa ipasavyo.

**Suluhisho**

Teua mpangilio wa ukubwa wa karatasi unaofaa.

### Nakala za kwanza hazijawekwa ipasavyo.

**Suluhisho**

- Hakikisha nakala ya kwanza imewekwa sahihi dhidi ya alama za upangiliaji.
- Ikiwa kingo za taswira iliyotambazwa zimepogolewa, sogeza nakala ya kwanza mbali kidogo na kona ya kioo cha kitambazaji. Unaweza kuchanganua eneo ndani ya takriban 1.5 mm (0.06 in.) kutoka kwenye ukingo wa glasi ya kichanganuzi.

➡ "Kuweka Nakala Asili" kwenye ukurasa wa 34

### Kuna vumbi au uchafu kwenye glasi ya kichanganuzi.

**Suluhisho**

Unapoweka nakala asili kwenye glasi ya kitambazaji, ondoa vumbi lolote au uchafu ambao umekwama kwenye nakala asili, na usafishe glasi ya kitambazaji. Ikiwa kuna vumbi au uchafu kwenye glasi, sehemu ya kunakili inaweza kupanuka kujumuisha vumbi au uchafu huo, na kusababisha mkao mbaya wa kunakili au picha ndogo.

➡ "Kusafisha Glasi ya Kichanganuzi" kwenye ukurasa wa 120

## Rangi, Uchafu, Matone Yasiyo sawa, au Mistari Sambamba Itaonekana katika Picha Zilizonakiliwa



Sababu zifuatazo zinaweza kuzingatiwa.

### Njia ya karatasi ni chafu.

**Suluhisho**

Weka na utoe karatasi bila kuchapisha ili usafishe njia ya karatasi.

➡ "Kusafisha Kijia cha Karatasi na Umwagikaji wa Wino" kwenye ukurasa wa 119

### Kuna vumbi au uchafu kwenye nakala asili au glasi ya kichanganuzi.

**Suluhisho**

Ondoa vumbi au uchafu wowote ambao unashika nakala asili kisha usafishe glasi ya kichanganuzi.

➡ "Kusafisha Glasi ya Kichanganuzi" kwenye ukurasa wa 120

### Kuna vumbi au uchafu kwenye ADF au nakala asili.

**Suluhisho**

Safisha ADF, na uondoe vumbi au uchafu wowote unaoambatana na nakala asili.

➡ "Kusafisha ADF" kwenye ukurasa wa 120

### Nakala asili ilibonyezwa kwa nguvu kupita kiasi.

**Suluhisho**

Iwapo utabonyeza kwa nguvu zaidi, ukungu, waa, na madoa yanaweza kutokea.

Usibonyeze nakala asili au kifuniko cha hati kwa nguvu kupita kiasi.

➡ “Kuweka Nakala Asili” kwenye ukurasa wa 34

### Mpangilio wa uzito wa nakala iko juu sana.

**Suluhisho**

Punguza mpangilio ya uzito wa nakala.

➡ “Chaguo Msingi za Menyu kwa Kunakjili” kwenye ukurasa wa 73

## Ruwaza Zaidi (Mistari Sambamba Iliyopatana) Huonekana katika Taswira Iliyonakiliwa



### Ikiwa nakala asili ni hati iliyochapishwa kama vile gazeti au katalogi, ruwaza yenye madoa ya moire huonekana.

**Suluhisho**

Badilisha mipangilio ya kupunguza na kupanua. Ikiwa ruwaza ya moiré bado inaonekana, weka nakala asili kwa pembe tofauti kidogo.

➡ “Chaguo Mahiri za Menyu kwa Kunakili” kwenye ukurasa wa 74

## Picha ya Upande wa Nyuma wa Ya Asili Huonekana Katika Picha Iliyonakiliwa




Sababu zifuatazo zinaweza kuzingatiwa.

### Unapotambaza nakala asili nyembamba, taswira katika sehemu ya nyuma zinaweza kutambazwa wakati sawia.

**Suluhisho**

Weka nakala asili kwenye glasi ya kichanganuzi kisha uweke karatasi ndogo nyeusi juu yake.

➡ “Kuweka Nakala Asili” kwenye ukurasa wa 34

**Mpangilio wa uzito wa nakala iko juu sana.**

**Suluhisho**

Punguza mpangilio ya uzito wa nakala.

➡ "Chaguo Msingi za Menyu kwa Kunakjili" kwenye ukurasa wa 73

### Matini au taswira Iliyonakiliwa kutoka kwenye ADF Imefinywa au Kurefushwa




**Huenda baadhi ya nakala asili zisitambazwe vilivyo kutoka kwenye ADF.**

**Suluhisho**

Kuweka nakala asili kwenye glasi ya kitambazaji.

Teua ?, na kisha uteue **Jinsi ya** > **Weka nakala asili** > **Glasi ya kichanganuzi**. Teua **Maliza** ili kufunga skirini ya uhuishaji.

## Matatizo ya Picha Iliyotambazwa

### Rangi Zisizo sawa, Uchafu, Madoa na mengineyo Zinaonekana Unapotambaza kutoka kwenye Glasi ya Kitambazaji



**Kuna vumbi au uchafu kwenye nakala asili au glasi ya kichanganuzi.**

**Suluhisho**

Ondoa vumbi au uchafu wowote ambao unashika nakala asili kisha usafishe glasi ya kichanganuzi.

➡ "Kusafisha Glasi ya Kichanganuzi" kwenye ukurasa wa 120

**Nakala asili ilibonyezwa kwa nguvu kupita kiasi.**

**Suluhisho**

Iwapo utabonyeza kwa nguvu zaidi, ukungu, waa, na madoa yanaweza kutokea.

Usibonyeze nakala asili au kifuniko cha hati kwa nguvu kupita kiasi.

➡ "Kuweka Nakala Asili" kwenye ukurasa wa 34

## Mistari Sambamba Huonekana Unapotambaza kutoka kwenyeADF



### Kuna vumbi au uchafu kwenye ADF au nakala asili.

**Suluhisho**

Safisha ADF, na uondoe vumbi au uchafu wowote unaoambatana na nakala asili.

➡ "Kusafisha ADF" kwenye ukurasa wa 120

## Sehemu ya pembeni Huonekana katika Mandharinyuma ya Picha Zilizochanganuliwa




### Unapotambaza nakala asili nyembamba, taswira katika sehemu ya nyuma zinaweza kutambazwa wakati sawia.

**Suluhisho**

Unapochanganua kutoka kwenye glasi ya kichanganuzi, weka karatasi jeusi au pedi ya dawati juu ya nakala asili.

➡ "Kuweka Nakala Asili" kwenye ukurasa wa 34

## Haiwezi Kutambaza Eneo Sahihi kwenye Kioo cha Kitambazaji



### Nakala za kwanza hazijawekwa ipasavyo.

**Suluhisho**

- Hakikisha nakala ya kwanza imewekwa sahihi dhidi ya alama za upangiliaji.
- Ikiwa kingo za taswira iliyotambazwa zimepogolewa, sogeza nakala ya kwanza mbali kidogo na kona ya kioo cha kitambazaji. Unaweza kuchanganua eneo ndani ya takriban 1.5 mm (0.06 in.) kutoka kwenye ukingo wa glasi ya kichanganuzi.

➡ "Kuweka Nakala Asili" kwenye ukurasa wa 34

### Kuna vumbi au uchafu kwenye glasi ya kichanganuzi.

**Suluhisho**

Ondoa uchafu wowote kutoka kwa glasi ya kichanganuzi na jalada la waraka. Iwapo kuna takataka au uchafu wowote karibu na nakala asili, umbali wa utambazaji hupanuka ili kuujumuisha.

➡ "Kusafisha Glasi ya Kichanganuzi" kwenye ukurasa wa 120

### Unapochanganua nakala asilia nyingi ukitumia Epson ScanSmart, hakuna nafasi ya kutosha baina ya nakala asilia.

**Suluhisho**

Unapoweka nakala asili nyingi kwenye glasi ya kichanganuzi, hakikisha kuna nafasi ya angalau 20 mm (0.8 in.) kati ya nakala asili.

## Haiwezi Kutatua Matatizo kwenye Taswira Iliyotambazwa

Angalia yafuatayo ikiwa umejaribu suluhu zote na hujafanikiwa kutatua tatizo.

### Kuna tatizo na mipangilio ya programu ya utambazaji.

**Suluhisho**

Tumia Epson Scan 2 Utility ili kuanzisha mipangilio ya programu ya kitambazaji.

***Kumbuka:***
*Epson Scan 2 Utility ni programu inayokuja na zanamango ya kitambazaji.*

1. Anzisha Epson Scan 2 Utility.
   - Windows 10

     Bofya kitufe cha kuanza kisha uchague **EPSON** > **Epson Scan 2 Utility**.
   - Windows 8.1/Windows 8

     Andika jina la programu katika sehemu ya utafutaji, na kisha uchague ikoni inayoonekana.
   - Windows 7/Windows Vista/Windows XP

     Bofya kitufe cha kuanza kisha uteue **Programu Zote** au **Programu** > **EPSON** > **Epson Scan 2** > **Epson Scan 2 Utility**.
   - Mac OS

     Teua **Nenda** > **Programu** > **Epson Software** > **Epson Scan 2 Utility**.
2. Chagua kichupio cha **Nyingine**.
3. Bofya **Weka upya**.

Ikiwa uanzishaji hautatui tatizo hilo, sakinusha na usakinishe upya programu ya kitambazaji.

➡ “Kusakinisha au Kuondoa Programu Kando” kwenye ukurasa wa 128

### Matini au Taswira Iliyotambazwa kutoka kwenye ADF Imefinywa au Kurefushwa




#### Huenda baadhi ya nakala asili zisitambazwe vilivyo kutoka kwenye ADF.

**Suluhisho**

Kuweka nakala asili kwenye glasi ya kitambazaji.

Teua ⓘ, na kisha uteue **Jinsi ya** > **Weka nakala asili** > **Glasi ya kichanganuzi**. Teua **Maliza** ili kufunga skirini ya uhuishaji.

## Ubora wa Faksi Iliyotumwa ni Duni

### UbUbora wa Faksi Iliyotumwa ni Duni



Sababu zifuatazo zinaweza kuzingatiwa.

#### Kuna vumbi au uchafu kwenye nakala asili au glasi ya kichanganuzi.

**Suluhisho**

Ondoa vumbi au uchafu wowote ambao unashika nakala asili kisha usafishe glasi ya kichanganuzi.

➡ “Kusafisha Glasi ya Kichanganuzi” kwenye ukurasa wa 120

#### Nakala asili ilibonyezwa kwa nguvu kupita kiasi.

**Suluhisho**

Iwapo utabonyeza kwa nguvu zaidi, ukungu, waa, na madoa yanaweza kutokea.

Usibonyeze nakala asili au kifuniko cha hati kwa nguvu kupita kiasi.

➡ “Kuweka Nakala Asili” kwenye ukurasa wa 34

## Mistari Sambamba Huonekana Unapotuma Faksi kutoka ADF



### Kuna vumbi au uchafu kwenye ADF au nakala asili.

**Suluhisho**

Safisha ADF, na uondoe vumbi au uchafu wowote unaoambatana na nakala asili.

➡ "Kusafisha ADF" kwenye ukurasa wa 120

## Ubora wa Taswira ya Faksi Iliyotumwa ni Duni



Sababu zifuatazo zinaweza kuzingatiwa.

### Mwonekano umewekwa kuwa chini.

**Suluhisho**

Iwapo hufahamu utendaji wa mashine ya faksi ya mtumaji, weka yafuatayo kabla ya kutuma faksi.

- Teua **Faksi** > **Mipangilio ya Faksi** na kisha uweke mpangilio wa **Mwonekano** ili uweke taswira ya ubora wa juu zaidi.
- Teua **Faksi** > **Mipangilio ya Faksi** na kisha uwezeshe **Tuma Moja kwa Moja**.

  Kumbuka kuwa iwapo utaweka **Mwonekano** kwa **Picha** lakini utume faksi bila kuwezesha **Tuma Moja kwa Moja**, faksi inaweza kutumwa kwa mwonekano wa chini.

### MpaMpangilio wa ECM umelemazwa.

**Suluhisho**

Teua **Mipangilio** > **Mipangilio ya Jumla** > **Mipangilio ya Faksi** > **Mipangilio Msingi** na uwezeshe mpangilio wa **ECM** kwenye paneli dhibiti. Huenda hii ikaondoa kosa linatokea kwa sababu ya matatizo ya muunganisho. Kumbuka kuwa kasi ya kutuma na kupokea faksi inaweza kupungua kuliko wakati ECM imelemazwa.

### Taswira ya Upande wa Nyuma wa Nakala Asili Inaonekana katika Taswira Iliyotambazwa



Sababu zifuatazo zinaweza kuzingatiwa.

#### Unapotambaza nakala asili nyembamba, taswira katika sehemu ya nyuma zinaweza kutambazwa wakati sawia.

**Suluhisho**

Weka nakala asili kwenye glasi ya kichanganuzi kisha uweke karatasi ndogo nyeusi juu yake.

➡ "Kuweka Nakala Asili" kwenye ukurasa wa 34

#### Mpangilio wa Mpangilio wa uzito uko juu wakati wa kutuma faksi.

**Suluhisho**

Teua **Faksi** > **Mipangilio ya Faksi** > **Mipangilio ya Utambazaji** > **Uzito**, na kisha uwezeshe mpangilio.

## Ubora wa Faksi Iliyopokwa ni Duni

### UboraUbora wa Taswira ya Faksi Zilizopokewa ni Duni



Sababu zifuatazo zinaweza kuzingatiwa.

#### MpaMpangilio wa ECM umelemazwa.

**Suluhisho**

Teua **Mipangilio** > **Mipangilio ya Jumla** > **Mipangilio ya Faksi** > **Mipangilio Msingi** na uwezeshe mpangilio wa **ECM** kwenye paneli dhibiti. Huenda hii ikaondoa kosa linatokea kwa sababu ya matatizo ya muunganisho. Kumbuka kuwa kasi ya kutuma na kupokea faksi inaweza kupungua kuliko wakati ECM imelemazwa.

#### MpaMpangilio wa ubora wa taswira ipo chini kwenye mashine ya faksi ya mtumaji.

**Suluhisho**

Muulize mtumaji atume faksi katika ubora wa juu zaidi.

# Haiwezi Kutatua Tatizo

Ikiwa huwezi kutatua tatizo baada ya kujaribu suluhu zote, wasiliana na timu ya usaidizi ya Epson.

Ikiwa huwezi kutatua matatizo ya uchapishaji au kunakili, angalia maelezo yafuatayo yanayohusiana.

**Maelezo Husika**

➡ "Haiwezi Kutatua Matatizo ya Uchapishaji na Kunakili" kwenye ukurasa wa 226

## Haiwezi Kutatua Matatizo ya Uchapishaji na Kunakili

Jaribu matatizo yafuatayo ili kuanza mwanzo hadi utatue tatizo.

❏ Hakikisha kwamba umelinganisha aina ya karatasi iliyopakiwa kwenye kichapishi na aina ya karatasi iliyowekwa kwenye kichapishi na mipangilio ya aina ya karatasi kwenye kiendesha kichapishi.

  "Mipangilio ya Ukubwa na Aina ya Karatasi" kwenye ukurasa wa 30

❏ Tumia mipangilio ya ubora wa juu kwenye paneli dhibiti au kiendesha kichapishi.

❏ Linganisha kichwa cha kuchapisha.

  "Kulinganisha Kichwa cha Kuchapisha" kwenye ukurasa wa 118

❏ Angalia nozeli ili uone ikiwa nozeli za kichwa cha kuchapisha zimeziba.

  Ikiwa kuna sehemu ambazo hazipo kwenye ruwaza za kuangalia nozeli, huenda nozeli zimeziba. Rudia kusafisha kichwa na kuangalia nozeli kwa kupishana mara 3 na uangalie ikiwa kuziba huko kumeondolewa.

  Kumbuka kwamba usafishaji wa kichwa cha kuchapisha hutumia wino.

  "Kukagua na Kusafisha Kichwa cha Kuchapisha" kwenye ukurasa wa 115

❏ Zima kichapishi na usubiri kwa angalau saa 12 na uangalie ikiwa imeacha kuziba.

  Iwapo tatizo ni kuziba, kuacha kichapishi kwa muda bila kuchapisha kunaweza kutatua tatizo hilo.

  Unaweza kuangalia vipengee vifafuatavyo wakati kichapishi kimezima.

❏ Angalia kwamba unatumia chupa za wino halali za Epson.

  Jaribu kutumia chupa za wino halali wa Epson. Matumizi ya chupa za wino usio halali yanaweza kusababisha upungufu wa ubora wa uchapishaji.

❏ Angalia iwapo utepe nzito imechafuka.

  Ikiwa kuna uchafu uliopaka utepe nzito, pangusa uchafu huo kwa makini.

  "Kusafisha Filamu Angavu" kwenye ukurasa wa 123

❏ Hakikisha kwamba hakuna vipande vya karatasi vinavyosalia kwenye kichapishi.

  Unapoondoa karatasi, Usiguse utepe nzito kwa mikono yako ua karatasi.

❏ Angalia karatasi.

  Angalia ikiwa karatasi imejikunja au imepakiwa huku upande unaochapishika ukielekea juu.

  "Tahadhari za Kushughulikia Karatasi" kwenye ukurasa wa 30

  "Karatasi Inayopatikana na Uwezo" kwenye ukurasa wa 250

  "Aina Zisizopatikana za Karatasi" kwenye ukurasa wa 253

❏ Ukizima kichapishi na kusubiri kwa angalau saa 12 na ubora wa chapisho bado haujaimarisha, endesha Usafishaji wa Nishati.

  "Kuendesha Usafishaji wa Nishati" kwenye ukurasa wa 117

Ikiwa huwezi kutatua taizo kwa kuangalia suluhu zilizo hapa juu, unaweza kuhitaji kuomba ukarabati. Wasiliana na usaidizi wa Epson.

**Maelezo Husika**

➡ "Kabla ya Kuwasiliana na Epson" kwenye ukurasa wa 309
➡ "Kuwasiliana na Usaidizi wa Epson" kwenye ukurasa wa 309

# Kuongeza au Kubadilisha Kompyuta au Vifaa

Kuunganisha Kichapishi ambacho Kimeunganishwa kwenye Mtandao. . . . . . . . . . . .229

Kuwuka upya Muunganisho wa Mtandao. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .230

Kuunganisha Kifaa Maizi na Kichapishi Moja kwa Moja (Wi-Fi Direct). . . . . . . . . . . 236

Kuangalia Hali ya Muunganisho ya Mtandao. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 240

# Kuunganisha Kichapishi ambacho Kimeunganishwa kwenye Mtandao

Ikiwa kichapishi tayari kimeunganishwa kwenye mtandao, unaweza kuunganisha kompyuta au kifaa maizi kwenye kichapishi kupitia mtandao.

## Kutumia Kichapishaji cha Mtandao kutoka Kompyuta ya Pili

Tunapendekeza kutumia kisakinishaji ili kuunganisha kichapishi kwenye kompyuta. Unaweza kuendesha kisakinishaji kwa kutumia mbinu zifuatazo.

❏ Kusanidi kutoka kwenye tovuti

Fikia tovuti ifuatayo, kisha uingize jina la bidhaa. Nenda kwenye **Mpangilio**, na kisha uanze kusanidi.

https://epson.sn

❏ Sanidi kwa kutumia diski ya programu (kwenye modeli zinazokuja na diski ya programu na watumiaji walio na kompyuta za Windows zilizo na viendeshi vya diski pekee).

Chomeka diski ya programu kwenye kompyuta, kisha ufuate maagizo ya kwenye skrini.

### Teua Kichapishi

Fuata maagizo yaliyo kwenye skrini hadi skrini ifuatayo ionyeshwe, teua jina la kichapishi unachotaka kuunganishwa, na kisha ubofye **Ifuatayo**.




Fuata maagizo ya kwenye skrini.

## Kutumia Kichapishi cha Mtandao kutoka Kifaa Maizi

Unaweza kuunganisha kifaa maizi kwenye kichapishi ukitumia moja kati ya mbinu zifuatazo.

**Kuunganisha kupitia kipanga njia pasiwaya**

Unganisha kifaa maizi kwenye mtandao ule ule wa Wi-Fi (SSID) kama kichapishi.

Angalia yafuatayo kwa maelezo zaidi.

"Kuweka Mipangilio ya Kuunganishwa kwenye Kifaa Maizi" kwenye ukurasa wa 230

**Inaunganisha kupitia Wi-Fi Direct**

Unganisha kifaa maizi kwenye kichapishi moja kwa moja bila kipanga njia pasiwaya.

Angalia yafuatayo kwa maelezo zaidi.

"Kuunganisha Kifaa Maizi na Kichapishi Moja kwa Moja (Wi-Fi Direct)" kwenye ukurasa wa 236

# Kuwuka upya Muunganisho wa Mtandao

Sehemu hii hufafanua jinsi ya kuweka mipangilio ya muunganisho wa mtandao na kubadlisha mbinu ya muunganisho unapobadilisha kipanga njia pasiwaya au kompyuta.

## Unapobadilisha Kipanga Njia Pasiwaya

Unapobadilisha kipanga njia pasiwaya, weka mipangilio ya muunganisho kati ya kompyuta au kifaa maizi na kichapishi.

Unahitaji kuunda mipangilio hii iwapo utabadilisha mtoa huduma wako wa Intaneti nakadhalika.

### Kuweka Mipangilio ya Kuunganisha Kompyuta

Tunapendekeza kutumia kisakinishaji ili kuunganisha kichapishi kwenye kompyuta. Unaweza kuendesha kisakinishaji kwa kutumia mbinu zifuatazo.

- Kusanidi kutoka kwenye tovuti

  Fikia tovuti ifuatayo, kisha uingize jina la bidhaa. Nenda kwenye **Mpangilio**, na kisha uanze kusanidi.

  https://epson.sn

- Sanidi kwa kutumia diski ya programu (kwenye modeli zinazokuja na diski ya programu na watumiaji walio na kompyuta za Windows zilizo na viendeshi vya diski pekee).

  Chomeka diski ya programu kwenye kompyuta, kisha ufuate maagizo ya kwenye skrini.

### Kuweka Mipangilio ya Kuunganishwa kwenye Kifaa Maizi

Unaweza kutumia kichapishi kutoka kwenye kifaa maizi unapounganisha kichapishi katika mitandao sawa ya Wi-Fi (SSID) kama kifaa maizi. Ili kutumia kichapihsi kutoka kwenye kifaa maizi, sanidi kutoka kwenye tovuti ifuatayo. Fikia tovuti kutoka kwenye kifaa maizi unachotaka kuunganisha kwenye kichapishi.

http://epson.sn > **Mpangilio**

# Unapobadilisha Kompyuta

Unapobadilisha kompyuta, weka mipangilio kati ya kompyuta na kichapishi.

## Kuweka Mipangilio ya Kuunganisha Kompyuta

Tunapendekeza kutumia kisakinishaji ili kuunganisha kichapishi kwenye kompyuta. Unaweza kuendesha kisakinishaji kwa kutumia mbinu zifuatazo.

- Kusanidi kutoka kwenye tovuti

  Fikia tovuti ifuatayo, kisha uingize jina la bidhaa. Nenda kwenye **Mpangilio**, na kisha uanze kusanidi.

  https://epson.sn
- Sanidi kwa kutumia diski ya programu (kwenye modeli zinazokuja na diski ya programu na watumiaji walio na kompyuta za Windows zilizo na viendeshi vya diski pekee).

  Chomeka diski ya programu kwenye kompyuta, kisha ufuate maagizo ya kwenye skrini.

Fuata maagizo ya kwenye skrini.

# Kubadilisha Mbinu ya Muunganisho hadi kwa Kompyuta

Sehemu hii inafafanua jinsi ya kubadilisha mbinu ya uunganishaji wakati kompyuta na kichapishi vimeunganishwa.

## Kubadilisha Muunganisho wa Mtandao kutoka Ethaneti hadi Wi-Fi

Badilisha muunganisho wa Ethaneti hadi kwa Wi-Fi kutoka katika paneli dhibiti ya kichapishaji. Mbinu ya kubadilisha muunganisho kimsingi ni sawa na mipangilio ya muunganisho wa Wi-Fi.

**Maelezo Husika**

➡ "Kufanya Mipangilio ya Wi-Fi kutoka kwenye Paneli ya Kudhibiti" kwenye ukurasa wa 232

## Kubadilisha Muunganisho wa Mtandao kutoka Wi-Fi hadi Ethaneti

Fuata hatua zilizo hapa chini ili kubadilisha muunganisho kutoka Wi-Fi hadi muunganisho wa Ethaneti.

1. Teua **Mipangilio** kwenye skrini ya nyumbani.

2. Teua **Mipangilio ya Jumla** > **Mipangilio ya Mtandao** > **Usanidi wa Lana ya Waya**.

3. Fuata maagizo ya kwenye skrini.

## Kubadilisha kutoka muunganisho wa USB hadi Mtandao

Kutumia kisakinishaji na uwekaji upya katika mbinu tofauti ya muunganisho.

- Kusanidi kutoka kwenye tovuti

  Fikia tovuti ifuatayo, kisha uingize jina la bidhaa. Nenda kwenye **Mpangilio**, na kisha uanze kusanidi.

  https://epson.sn

- Sanidi kwa kutumia diski ya programu (kwenye modeli zinazokuja na diski ya programu na watumiaji walio na kompyuta za Windows zilizo na viendeshi vya diski pekee).

  Chomeka diski ya programu kwenye kompyuta, kisha ufuate maagizo ya kwenye skrini.

#### Uteuaji wa Kubadilisha Mbinu za Muunganisho

Fuata maagizo ya kwenye skrini hadi skrini ya ifuatayo ionyeshwe.

Teua muunganisho wa mtandao unaotaka kutumia, **Unganisha kupitia mtandao pasi waya (Wi-Fi)** au **Unganisha kupitia LAN ya waya (Ithaneti)**, na kisha ubofye **Ifuatayo**.




*Kumbuka:*
*Mbinu ya muunganisho iliyoonyeshwa inatofautiana kulingana na modeli.*

Fuata maagizo ya kwenye skrini.

## Kufanya Mipangilio ya Wi-Fi kutoka kwenye Paneli ya Kudhibiti

Unaweza kutengeneza mipangilio ya mtandao kutoka kwenye paneli dhibiti ya kichapishaji katika njia mbalimbali. Chagua njia ya muunganisho ambayo inalingana na mazingira na masharti unayotumia.

Iwapo unajua maelezo ya kipanga njia pasiwaya kama vile SSID na nenosiri, unaweza kuunda mipangilio kikuli.

Iwapo kipanga njia pasiewaya kinaauni WPS, unaweza kuunda mipangilio kwa kutumia usanidi wa kitufe cha kusukuma.

Baada ya kuunganisha kichapishi kwenye mtandao, unganisha kwenye kichapishaji kutoka kwenye kifaa ambacho unataka kutumia (kompyuta, kifaa maizi, kompyuta ndogo, na zaidi.).

### Maelezo Husika

➡ "Kuunda Mipangilio ya Wi-Fi kwa Kuingiza SSID na Nenosiri" kwenye ukurasa wa 233

➡ "Kuunda Mipangilio ya Wi-Fi kwa Usanidi wa Kitufe cha Kusukuma (WPS)" kwenye ukurasa wa 234

➡ "Kufanya Mipangilio kwa Msimbo wa PIN Sanidi (WPS)" kwenye ukurasa wa 235

## Kuunda Mipangilio ya Wi-Fi kwa Kuingiza SSID na Nenosiri

Unaweza kusanidi mtandao wa Wi-Fi kwa kuingiza maelezo muhimu ya kuunganisha kwenye kipanga njia pasiwaya kutoka kwenye paneli dhibiti ya kichapishi. Ili kusanidi kwa kutumia mbinu hii, unahitaji SSID na nenosiri kwa kipanga njia pasiwaya.

***Kumbuka:***
*Iwapo unatumia eneo la kipanga njia pasiwaya kwa mipangilio yake chaguo-msingi, SSID na nywila ziko kwenye lebo. Iwapo hufahamu SSID na nywila, tazama nyaraka zilizotolewa na kipanga njia pasiwaya.*




1. Donoa [icon] kwenye skrini ya nyumbani.

2. Teua **Wi-Fi (Inapendekezwa)**.

   Iwapo tayari kichapishi kimeunganishwa na Ethaneti, teua **Kipangishi njia**.

3. Donoa **Anza Kusanidi**.

   Iwapo tayari muunganisho wa mtandao umesanidiwa, maelezo ya muunganisho yanaonyeshwa. Donoa **Badilisha Mipangilio** ili kubadilisha mipangilio.

   Iwapo kichapishi tauari kimeunganishwa kwa Ethaneti, donoa **Badilisha kwa muunganisho wa Wi-Fi.**, na kisha uteue **Ndiyo** baada ya kuangalia ujumbe.

4. Teua **Sogora ya Kusanidi Wi-Fi**.

5. Teua SSID kwa kipanga njia pasiwaya.

   ***Kumbuka:***
   - *Iwapo SSID unayotaka kuunganisha kwayo haionyeshwi kwenye paneli dhibiti ya kichapishi, donoa **Tafuta Tena** ili kusasisha orodha. Iwapo bado haitaonyeshwa, donoa **Ingiza Kikuli**, na kisha uingize SSID moja kwa moja.*
   - *Iwapo hujui jina la mtandao (SSID) angalia iwapo maelezo yameandikwa kwenye lebo ya kipanga njia pasiwaya. Iwapo unatumia kipanga njia pasiwaya kwa mipangilio yake chaguo-msingi, tumia SSID kwenye lebo. Iwapo huwezi kutafuta maelezo yoyote, tazama nyaraka zilizotolewa pamoja na kipanga njia pasiwaya.*

6. Donoa **Ingiza Nywila**, na kisha uingize nenosiri.

   ***Kumbuka:***
   - *Nenosiri linaathiriwa na herufi kubwa au ndogo.*
   - *Iwapo hujui nenosiri, angalia iwapo maelezo yameandikwa kwenye lebo ya kipanga njia pasiwaya. Kwenye lebo, nenosiri linaweza kuandikwa "Network Key", "Wireless Password", na kadhalika. Ikiwa unatumia kipanga njia pasiwaya na mipangilio yake chaguomsingi, tumia nenosiri lilioandikwa kwenye lebo.*

7. Unapokamilisha, donoa **OK**.

8. Angalia mipangilio, na kisha udonoe **Anza Kusanidi**.

9. Funga skrini.

   Skrini hufunga kiotomatiki baada ya kipindi maalum cha muda.

   ***Kumbuka:***
   *Ukishindwa kuunganisha, pakia karatasi tupu la ukubwa wa A4, na kisha uteue **Chapisha Ripoti ya Ukaguzi** ili kuchapisha ripoti ya muunganisho.*

10. Funga skrini ya **Mipangilio ya Muunganis. Mtandao**.

**Maelezo Husika**

➡ "Kuingiza Vibambo" kwenye ukurasa wa 27

➡ "Kuangalia Hali ya Muunganisho ya Mtandao" kwenye ukurasa wa 240

## Kuunda Mipangilio ya Wi-Fi kwa Usanidi wa Kitufe cha Kusukuma (WPS)

Unaweza kusanidi mtandao wa Wi-Fi kiotomatiki kwa kubonyeza kitufe kwenye kipanga njia pasiwaya. Ikiwa masharti yafuatayo yatatimizwa, unaweza kusanidi kwa kutumia mbinu hii.

- Kipanga njia pasiwaya kinatangamana na WPS (Usanidi wa Wi-Fi Uliolindwa).
- Muunganisho wa sasa wa Wi-Fi ulitambuliwa kwa kubonyeza kitufe kwenye kipanga njia pasiwaya.

1. Donoa  kwenye skrini ya nyumbani.

2. Teua **Wi-Fi (Inapendekezwa)**.

   Iwapo tayari kichapishi kimeunganishwa na Ethaneti, teua **Kipangishi njia**.

3. Donoa **Anza Kusanidi**.

   Iwapo tayari muunganisho wa mtandao umesanidiwa, maelezo ya muunganisho yanaonyeshwa. Donoa **Badilisha Mipangilio** ili kubadilisha mipangilio.

   Iwapo kichapishi tauari kimeunganishwa kwa Ethaneti, donoa **Badilisha kwa muunganisho wa Wi-Fi.**, na kisha uteue **Ndiyo** baada ya kuangalia ujumbe.

4. Teua **Sukuma Kitufe cha Usanidi (WPS)**.

5. Shikilia chini kitufe cha [WPS] kwenye kipanga njia pasiwaya hadi taa ya usalama imweke.




Ikiwa hujui kilipo kitufe cha [WPS], au hakuna vitufe kwenye kipanga njia pasiwaya, tazama hati iliyotolewa yenye kipamnga njia pasiwaya kwa maelezo.

6. Donoa **Anza Kusanidi** kwenye kichapishi.

7. Funga skrini.

   Skrini hufunga kiotomatiki baada ya kipindi maalum cha muda.

   ***Kumbuka:***
   *Iwapo muunganisho utashindikana, washa upya kipanmga njia pasiwaya, kisogeze karibu na kichapishi, na ujaribu tena. Iwapo haitafanya kazi, chapisha ripoti ya muunganisho wa mtandao na uangalie suluhisho.*

8. Funga skrini ya **Mipangilio ya Muunganis. Mtandao**.

**Maelezo Husika**

➡ "Kuangalia Hali ya Muunganisho ya Mtandao" kwenye ukurasa wa 240

## Kufanya Mipangilio kwa Msimbo wa PIN Sanidi (WPS)

Unaweza kuunganisha kiotomatiki kwenye kipanga njia pasiwaya kwa kutumia msimbo wa PIN. Unaweza kutumia mbinu hii kuweka ikiwa kipanga njia pasiwaya kina uwezo wa WPS (Usanidi wa Wi-Fi Uliolindwa). Tumia kompyuta kuingiza msimbo wa PIN katika kipanga njia pasiwaya.

1. Donoa  kwenye skrini ya nyumbani.

2. Teua **Wi-Fi (Inapendekezwa)**.

   Iwapo tayari kichapishi kimeunganishwa na Ethaneti, teua **Kipangishi njia**.

3. Donoa **Anza Kusanidi**.

   Iwapo tayari muunganisho wa mtandao umesanidiwa, maelezo ya muunganisho yanaonyeshwa. Donoa **Badilisha Mipangilio** ili kubadilisha mipangilio.

   Iwapo kichapishi tauari kimeunganishwa kwa Ethaneti, donoa **Badilisha kwa muunganisho wa Wi-Fi.**, na kisha uteue **Ndiyo** baada ya kuangalia ujumbe.

4. Chagua **Nyingine** > **Usanidi Msimbo PIN (WPS)**.

5. Tumia kompyuta yako kuingiza msimbo wa PIN (nambari ya herufi nane) inayoonyeshwa kwenye paneli dhibiti ya kichapishi hadi kwenye kipanga njia pasiwaya ndani ya dakika mbili.

   ***Kumbuka:***
   *Tazama waraka uliotolewa kwa kipanga njia pasiwaya chako kwa maelezo kuhusu kuweka msimbo wa PIN.*

6. Donoa **Anza Kusanidi** kwenye paneli dhibiti ya kichapishi.

7. Funga skrini.

   Skrini hufunga kiotomatiki baada ya kipindi maalum cha muda.

   ***Kumbuka:***
   *Iwapo muunganisho utashindikana, washa upya kipanga njia pasiwaya, lisogeze karibu na kichapishi, na ujaribu tena. Iwapo haitafanya kazi, chapisha ripoti ya muunganisho na uangalie suluhisho.*

8. Funga skrini ya **Mipangilio ya Muunganis. Mtandao**.

**Maelezo Husika**

➡ "Kuangalia Hali ya Muunganisho ya Mtandao" kwenye ukurasa wa 240

# Kuunganisha Kifaa Maizi na Kichapishi Moja kwa Moja (Wi-Fi Direct)

Wi-Fi Direct (AP Rahisi) hukuruhusu kuunganisha mifaa maizi moja kwa moja kwenye kichapishi bila kipanga njia pasiwaya na kuchapisha kutoka kifaa maizi.

## Kuhusu Wi-Fi Direct

Tumia mbinu hii ya muunganisho wakati hutumii Wi-Fi nyumbani au afisini au wakati unataka kuunganisha kichapishi na kompyuta au kifaa maizi moja kwa moja. Katika modi hii, kichapishi hutumika kama kipanga njia pasiwaya na unaweza kuunganisha vifaa kwenye kichapishi bila kutumia kipanga njia pasiwaya wastani. Hata hivyo, vifaa vilivyounganishwa moja kwa moja kwenye kichapishi haviwezi kuwasiliana na vingine kupitia kichapishi.



Kichapishi kinaweza kuunganishwa na Wi-Fi au Etheneti, na muunganisho wa Wi-Fi Direct (AP Rahisi) kwa wakati mmoja. Hata hivyo, ukiwasha muunganisho wa mtandao kwenye muunganisho wa Wi-Fi Direct (AP Rahisi) wakati kichapishi kimeunganishwa kwa Wi-Fi, Wi-Fi inakatwa muunganisho kwa muda.

## Kunganisha kwenye Vifaa kwa kutumia Wi-Fi Direct

Mbinu hii hukuruhusu kuunganisha kichapishi moja kwa moja kwenye vifaa bila eneo la kipanga njia pasiwaya.

***Kumbuka:***
*Kwa watumiaji wa iOS au Android, ni rahisi kusanidi kutoka kwenye Epson Smart Panel.*

*Unahitaji kuunda mipangilio hii kwa kichapishi na kifaa unachotaka kuunganisha mara moja. Isipokuwa ulemaze Wi-Fi Direct au kurejesha mipangilio ya mtandao kwa chaguo-msingi yake, huhitaji kuunda mipangilio hii tena.*

1. Donoa kwenye skrini ya nyumbani.

2. Donoa **Wi-Fi Direct**.

3. Donoa **Anza Kusanidi**.

4. Teua **Mbinu Nyingine**.

5. Teua **Vifaa Vingine vya OS**.

6. Kwenye skrini ya Wi-Fi ya kifaa, teua SSID iliyoonyeshwa kwenye paneli dhibiti, na kisha uingize nenosiri.




7. Kwenye skrini ya programu ya kuchapisha kwa kifaa, teua kichapishi unachotaka kuunganishwa.

8. Kwenye paneli dhibiti ya kichapishi, teua **Imekamilika**.

Kwa vifaa ambavyo vimeunganishwa kwenye kichapishi mbeleni, teua jina la mtandao (SSID) kwenye skrini ya Wi-Fi ya kifaa maizi ili kuviunganisha tena.

***Kumbuka:***
*Iwapo unatumia kifaa cha iOS, pia unaweza kuunganisha kwa kutumia msimbo wa QR kwa kamera wastani ya iOS. Tazama kiungo cha hapa chini http://epson.sn.*

## Kukatisha Muunganisho wa Wi-Fi Direct (AP Rahisi)

***Kumbuka:***
*Wakati muunganisho wa Wi-Fi Direct wa (AP Rahisi) unalemazwa, kompyuta zote na vifaa maizi vilivyounganishwa kwenye kichapishi katika muunganisho wa Wi-Fi Direct (AP Rahisi) vinatenganishwa. Iwapo unataka kukata muunganisho wa kifaa maalum, kata muunganisho kutoka kwenye kifaa badala ya kichapishi.*

1. Donoa kwenye skrini ya nyumbani.
2. Teua **Wi-Fi Direct**.

   Maelezo ya Wi-Fi Direct yanaonyeshwa.
3. Donoa **Anza Kusanidi**.
4. Donoa .
5. Teua **Lemaza Wi-Fi Direct**.
6. Donoa **Lemaza mipangilio**.
7. Wakati ujumbe wa ukamilisho umeonyeshwa, funga skrini.

   Skrini hufunga kiotomatiki baada ya kipindi maalum cha muda.
8. Funga skrini ya **Mipangilio ya Muunganis. Mtandao**.

## Kubadilisha Mipangilio ya Wi-Fi Direct (AP Rahisi) kama vile SSID

Wakati muunganisho wa Wi-Fi Direct (AP Rahisi) umewezeshwa, unaweza kubadilisha mipangilio kutoka > **Wi-Fi Direct** > **Anza Kusanidi** > , na kisha vipengee vifuatavyo vya menyu vimeonyesha.

### Badilisha Jina la Mtandao

Badilisha jina la mtandao (SSID) la Wi-Fi Direct (AP Rahisi) linalotumika kwa kuunganisha kichapishi kwenye jina lako lisilo na mantiki. Unaweza kuweka jina la mtandao (SSID) kwenye vibambo vya ASCII vinavyoonyeshwa kwenye kibodi ya programu kwenye paneli dhibiti. Unaweza kuingiza hadi vibambo 22.

Unapobadilisha jina la mtandao (SSID), vifaa vyote vilivyounganishwa vinakatwa muunganisho. Tumia jina jipya la mtandao (SSID) iwapo unataka kuunganisha upya kifaa.

### Badilisha Nywila

Badilisha nenosiri la Wi-Fi Direct (AP Rahisi) linalotumika kwa kuunganisha kichapishi kwenye jina lako lisilo na mantiki. Unaweza kuweka nenosiri kwenye vibambo vya ASCII vinavyoonyeshwa kwenye kibodi ya programu kwenye paneli dhibiti. Unaweza kuingiza vibambo kati ya 8 hadi 22.

Unapobadilisha nenosiri, vifaa vyote vilivyounganishwa vinakatwa muunganisho. Tumia nenosiri jipya iwapo unataka kuunganisha upya kifaa.

### Lemaza Wi-Fi Direct

Lemaza mipangilio ya Wi-Fi Direct (AP Rahisi) ya kichapishi. Unapoilemaza, vifaa vyote vilivyounganishwa kwenye kichapishi katika muunganisho wa Wi-Fi Direct (AP Rahisi) vinakatwa muunganisho.

### Rejeza Mipangilio Chaguo-msingi

Rejesha mipangilio yote ya Wi-Fi Direct (AP Rahisi) kwenye chaguo-msingi yake.

Maelezo ya muunganisho wa Wi-Fi Direct (AP Rahisi) ya kifaa maizi yaliyohifadhiwa kwenye kichapishi yamefutwa.

# Kuangalia Hali ya Muunganisho ya Mtandao

Unaweza kuangalia hali ya muunganisho wa mtandao katika njia ifuatayo.

**Maelezo Husika**

➡ "Kukagua Hali ya Muunganisho wa Mtandao kutoka Paneli Dhibiti" kwenye ukurasa wa 240

➡ "Kuchapisha Ripoti ya Muunganisho wa Mtandao" kwenye ukurasa wa 241

## Kukagua Hali ya Muunganisho wa Mtandao kutoka Paneli Dhibiti

Unaweza kuangalia hali ya muunganisho ukitumia aikoni ya mtandao au taarifa ya mtandao kwenye paneli dhibiti ya kichapishi.

### Kuangalia Hali ya Muunganisho wa Mtandao kwa Kutumia Aikoni ya Mtandao

Unaweza kuangalia hali ya muunganisho wa mtandao na nguvu ya mawimbi ya redio kwa kutumia ikoni ya mtandao kwenye skrini ya nyumbani ya kichapishi.




### Kuonyesha Maelezo ya Kina ya Mtandao kwenye Paneli Dhibiti

Wakati kichapishi chako kimeunganishwa kwenye mtandao, pia unaweza kutazama maelezo mengine yanayohusiana na mtandao kwa kuteua menyu unazotaka kuangalia.

1. Teua **Mipangilio** kwenye skrini ya nyumbani.

2. Teua **Mipangilio ya Jumla** > **Mipangilio ya Mtandao** > **Hali ya Mtandao**.

3. Ili kuangalia maelezo, teua menyu unazotaka kuangalia.

   ❏ Hali ya LAN ya waya/Wi-Fi

   Huonyesha maelezo ya mtandao (jina la kifaa, muunganisho, nguvu ya ishara, na zaidi) kwa miunganisho ya Ethaneti au Wi-Fi.

   ❏ Hali ya Wi-Fi Direct

   Huonyesha iwapo Wi-Fi Direct imewezeshwa au kulemazwa, na SSID, nywila zaidi kwa miunganisho ya Wi-Fi Direct.

- ❏ Chapisha Karatasi ya Hali
  Huchapisha laha la hali ya mtandao. Maelezo ya Ethaneti, Wi-Fi, Wi-Fi Direct, na kadhalika yaliyochapishwa kwenye kurasa mbili au zaidi.

## Kuchapisha Ripoti ya Muunganisho wa Mtandao

Unaweza kuchapisha ripoti ya muunganisho wa mtandao ili kuangalia hali kati ya kichapishi na kipanga njia pasiwaya.

1. Teua **Mipangilio** kwenye skrini ya nyumbani.
2. Teua **Mipangilio ya Jumla** > **Mipangilio ya Mtandao** > **Ukaguzi wa Muunganisho**.

   Ukaguzi wa muunganisho unaanza.
3. Teua **Chapisha Ripoti ya Ukaguzi**.
4. Chapisha ripoti ya muunganisho wa mtandao.

   Iwapo kosa limetokea, angalia ripoti ya muunganisho, na kisha ufuate suluhisho zilizochapishwa.

### Ujumbe na Suluhisho kwenye Ripoti ya Muunganisho wa Mtandao

Angalia ujumbe na misimbo ya kosa katika ripoti ya muunganisho wa mtandao, na kisha ufuate suluhisho.



Check Network Connection

| | |
|---|---|
| Check Result | FAIL |
| Error code | (E-2) |

See the Network Status and check if the Network Name (SSID) is the SSID you want to connect.
If the SSID is correct, make sure to enter the correct password and try again.

If your problems persist, see your documentation for help and networking tips.

Checked Items

| | |
|---|---|
| Wireless Network Name (SSID) Check | FAIL |
| Communication Mode Check | Unchecked |
| Security Mode Check | Unchecked |
| MAC Address Filtering Check | Unchecked |
| Security Key/Password Check | Unchecked |
| IP Address Check | Unchecked |
| Detailed IP Setup Check | Unchecked |

Network Status

| | |
|---|---|
| Printer Name | EPSON XXXXXX |
| Printer Model | XX-XXX Series |
| IP Address | 169.254.137.8 |
| Subnet Mask | 255.255.0.0 |
| Default Gateway | |
| Network Name (SSID) | EpsonNet |
| Security | None |
| Signal Strength | Poor |
| MAC Address | F8:D0:27:40:C0:AC |

a. Msimbo wa kosa

b. Ujumbe kwenye Mazingira ya Mtandao

**Maelezo Husika**

➡ "E-1" kwenye ukurasa wa 242
➡ "E-2, E-3, E-7" kwenye ukurasa wa 242
➡ "E-5" kwenye ukurasa wa 243
➡ "E-6" kwenye ukurasa wa 243
➡ "E-8" kwenye ukurasa wa 244
➡ "E-9" kwenye ukurasa wa 244
➡ "E-10" kwenye ukurasa wa 244
➡ "E-11" kwenye ukurasa wa 245
➡ "E-12" kwenye ukurasa wa 245
➡ "E-13" kwenye ukurasa wa 246
➡ "Ujumbe kwenye Mazingira ya Mtandao" kwenye ukurasa wa 246

## E-1

**Suluhisho:**

- Hakikisha kuwa kebo yako ya Ethaneti imeunganishwa salama kwenye kichapishi chako na kitovu chako au kifaa kingine cha mtandao.
- Hakikisha kuwa kitovu au kifaa chako kingine cha mtandao vimewashwa.
- Iwapo unataka kuunganisha kichapishi kwa Wi-Fi, unda mipangilio ya Wi-Fi kwa kichapishi kwa sababu imelemazwa.

## E-2, E-3, E-7

**Suluhisho:**

- Hakikisha kipanga njia chako cha pasi waya kimewashwa.
- Thibitisha kwamba kompyuta au kifaa chako kimeunganishwa vizuri kwenye kipanga njia cha pasi waya.
- Zima kipanga njia cha pasi waya. Subiri takriban sekunde 10, na kisha ukiwashe.
- Weka printa karibu na kipanga njia chako cha pasi waya na uondoe vitu vyovyote kati yake.
- Ikiwa umeingiza SSID kwa mikono, ikague ikiwa na sahihi. Angalia SSID kutoka kwenye sehemu ya **Network Status** kwenye ripoti ya muunganisho wa mtandao.
- Ikiwa kipanga njia cha pasi waya kina SSID kadhaa, chagua SSID ambayo imeonyeshwa. Wakati SSID inatumia masafa yasiyotangamana, printa haizionyeshi.
- Ikiwa unatumia usanidi wa kitufe cha msukumo kuanzisha muunganisho wa mtandao, hakikisha kipanga njia chako cha pasi waya kinakubali WPS. Huwezi kutumia usanidi wa kitufe cha msukumo ikiwa kipanga njia chako cha pasi waya hakikubali WPS.
- Hakikisha SSID yako hutumia vibambo vya ASCII pekee (vibambo vya herufi na nambari na alama). Printa haiwezi kuonyesha SSID ambayo ina vibambo visivyokuwa vya ASCII.

- Hakikisha unajua SSID na nenosiri lako kabla ya kuunganisha kwenye kipanga njia cha pasi waya. Ikiwa unatumia kipanga njia cha pasi waya na mipangilio yake msingi, SSID na nenosiri ziko kwenye lebo kwenye kipanga njia cha pasi waya. Ikiwa hujui SSID na nenosiri lako, wasiliana na mtu aliyekuwekea kipanga njia cha pasi waya, au ungalie hati zilizokuja pamoja na kipanga njia cha pasi waya.
- Ikiwa unaunganisha kwenye SSID iliyotengenezwa kwa kutumia kipengele cha ufungaji cha kifaa maizi, kagua SSID na nenosiri kwenye hati zilizokuja pamoja na kifaa maizi.
- Ikiwa muunganisho wako wa Wi-Fi utatenganishwa kwa ghafla, kagua hali zifuatazo. Ikiwa hali zozote kati ya hizi zinatumika, weka mipangilio ya mtandao wako upya kwa kupakua na kuendesha programu kutoka kwenye tovuti ifuatayo.

  http://epson.sn > **Mpangilio**

  - Kifaa kingine mahiri kiliongezwa kwenye mtandao kwa kutumia usanidi wa kitufe cha uwasilishi.
  - Mtandao wa Wi-Fi ulisanidiwa kwa kutumia mbinu yoyote mbali na usanidi wa kitufe cha uwasilishi.

**Maelezo Husika**

➡ "Kuweka Mipangilio ya Kuunganisha Kompyuta" kwenye ukurasa wa 231

➡ "Kufanya Mipangilio ya Wi-Fi kutoka kwenye Paneli ya Kudhibiti" kwenye ukurasa wa 232

## E-5

**Suluhisho:**

Hakikisha aina ya usalama wa kipanga njia pasiwaya imewekwa kwa mojawapo ya yafuatayo. Iwapo sio hivyo, badilisha aina ya usalama katika kipanga njia pasiwaya, na kisha uweke upya mipangilio ya mtandao wa kichapishaji.

- WEP- biti 64 (biti 40)
- WEP- biti 128 (biti 104)
- WPA PSK (TKIP/AES)*
- WPA2 PSK (TKIP/AES)*
- WPA (TKIP/AES)
- WPA2 (TKIP/AES)
- WPA3-SAE (AES)

* WPA PSK pia inajulikana kama WPA ya Kibinafsi. WPA2 PSK pia inajulikana kama WPA2 ya Kibinafsi.

## E-6

**Suluhisho:**

- Kagua kama anwani ya uchujaji ya MAC imelemazwa. Ikiwa imewezesha, sajili anwani ya MAC ya printa ili isichujwe. Angali waraka uliotolewa pamoja na kipanga njia cha pasi waya kwa maelezo. Unaweza kukagua anwani ya printa ya MAC kutoka sehemu ya **Network Status** kuhusu ripoti ya muunganisho wa mtandao.
- Ikiwa kipanga njia chako cha pasi waya kinashiriki uhalalishaji wa kushiriki na usalama wa WEP, hakikisha ufunguo na kiolezo cha uhalalishaji ni sahihi.

- Ikiwa idadi ya vifaa vilivyounganishwa kwenye kipanga njia cha pasi waya ni chini ya idadi ya vifaa vya mtandao ambavyo unataka kuunganisha, fanya mipangilio kwenye kipanga njia cha pasi waya iongeze idadi ya vifaa vinavyoweza kuunganishwa. Angali waraka uliotolewa pamoja na kipanga njia cha pasi waya ili kufanya mipangilio.

**Maelezo Husika**

➡ "Kuweka Mipangilio ya Kuunganisha Kompyuta" kwenye ukurasa wa 231

## E-8

**Utatuzi:**

- Wezesha DHCP kwenye kipanga njia pasiwaya ikiwa mipangilio ya kichapishi ya Pata Anwani ya IP imewekwa kuwa Otomatiki.
- Iwapo mpangilio wa Kupata kichapishi IP umewekwa Kikuli, anwani IP unayoweka kikuli ni batili kutokana na kuwa nje ya masafa (kwa mfano: 0.0.0.0). Weka anwani halali ya IP kutoka katika paneli dhibiti ya kichapishi.

**Maelezo Husika**

➡ "Mipangilio ya Mtandao" kwenye ukurasa wa 267

## E-9

**Suluhisho:**

Kagua zifuatazo.

- Vifaa vimewashwa.
- Unaweza kufikia Intaneti na kompyuta nyingine au vifaa vya mtandao kwenye mtandao sawa kutoka kwa vifaa unavyotaka kuunganisha kwenye printa.

Ikiwa bado haiunganishi printa yako na vifaa vya mtandao baada ya kuthibitisha yaliyo hapa juu, zima kipanga njia cha pasi waya. Subiri takriban sekunde 10, na kisha ukiwashe. Weka upya mipangilio ya mtandao wako kwa kupakua na kuendesha kisakinishaji kutoka kwenye tovuti ifuatayo.

http://epson.sn > **Mpangilio**

**Maelezo Husika**

➡ "Kuweka Mipangilio ya Kuunganisha Kompyuta" kwenye ukurasa wa 231

## E-10

**Suluhisho:**

Angalia yafuatayo.

- Vifaa vingine kwenye mtandao vimewashwa.
- Anwani za mtandao (IP anwani, barakoa ya mtandao mdogo, na kichanganishi chaguomsingi) ni sahihi ikiwa umeweka kipengele cha kichapishaji cha Pata Anwani ya IP kuwa Mwenyewe.

Weka upya anwani ya mtandao iwapo hizi sio sahihi. Unaweza kuangalia anwani, barakoa ya mtandao mdogo, na kichanganishi cha IP kutoka kwenye sehemu ya **Network Status** kwenye ripoti ya muunganisho wa mtandao.

Iwapo DHCP imewashwa, badilisha mpangilio wa kichapishaji wa Pata Anwani ya IP kuwa Otomatiki. Ikiwa unataka kuweka anwani ya IP kuwa mwenyewe, angalia anwani ya IP ya kichapishi kutoka katika sehemu ya **Network Status** katika ripoti ya muunganisho wa mtandao, kisha chagua Mwenyewe kwenye skrini ya mipangilio ya mtandao. Weka barakoa ya mtandao mdogo kwa [255.255.255.0].

Ikiwa hii bado haitaunganisha kichapishi chako na vifaa vya mtandao, zima kipanga njia pasiwaya. Subiri kwa karibu sekunde 10, na kisha uiwashe.

#### Maelezo Husika

➡ “Mipangilio ya Mtandao” kwenye ukurasa wa 267

## E-11

#### Suluhisho:

Kagua zifuatazo.

❏ Anwani ya njia msingi ni sahihi ukiweka Usanidi wa TCP/IP wa Printa kwa Kufanya Mwenyewe.

❏ Kifaa ambacho kimewekwa kama njia msingi kimewashwa.

Weka anwani sahihi ya njia msingi. Unaweza kukagua anwani msingi kutoka kwenye sehemu ya **Network Status** kuhusu ripoti ya muunganisho wa mtandao.

#### Maelezo Husika

➡ “Mipangilio ya Mtandao” kwenye ukurasa wa 267

## E-12

#### Suluhisho:

Kagua zifuatazo.

❏ Vifaa vingine kwenye mtandao vimewashwa.

❏ Anwani za mtandao (anwani ya IP, anwani fiche, na njia msingi) ni sahihi ikiwa unaziingiza kwa mkono.

❏ Anwani za mtandao za vifaa vingine (anwani fiche na njia msingi) ni sawa.

❏ Anwani ya IP haigongani na vifaa vingine.

Ikiwa bado haiunganishi printa yako na vifaa vya mtandao baada ya kuthibitisha yaliyo hapa juu, jaribu zifuatazo.

❏ Zima kipanga njia cha pasi waya. Subiri takriban sekunde 10, na kisha ukiwashe.

❏ Weka mipangilio ya mtandao tena kwa kutumia kisakinishaji. Unaweza kuiendesha kutoka kwenye tovuti ifuatayo.

  http://epson.sn > **Mpangilio**

❏ Unaweza kusajili manenosiri kadhaa kwenye kipanga njia cha pasi waya ambacho hutumia usalama wa aina ya WEP. Ikiwa manenosiri kadhaa yamesajiliwa, kagua kwanza kama nenosiri lililosajiliwa limewekwa kwenye printa.

**Maelezo Husika**

➡ "Mipangilio ya Mtandao" kwenye ukurasa wa 267
➡ "Kuweka Mipangilio ya Kuunganisha Kompyuta" kwenye ukurasa wa 231

## E-13

**Suluhisho:**

Kagua zifuatazo.

- Vifaa vya mtandao kama vile kipanga njia cha pasi waya, kitovu, na kipanga njia zimewashwa.
- Usanidi wa TCP/IP wa vifaa vya mtandao haujasanidiwa kwa mkono. (Ikiwa usanidi wa TCP/IP umewekwa kiotomatiki wakati wa usanidi wa TCP/IP wa vifaa vingine vya mtandao vimewekwa kwa mikono, huenda mtandao wa printa ukatofautiana na mtandao wa vifaa vingine.)

Ikiwa bado inazozana baada ya kuangalia hii, jaribu ifuatayo.

- Zima kipanga njia cha pasi waya. Subiri takriban sekunde 10, na kisha ukiwashe.
- Weka mipangilio ya mtandao kwenye kompyuta ambayo iko kwenye mtandao sawa na printa kwa kutumia kisakinishaji. Unaweza kuiendesha kutoka kwenye tovuti ifuatayo.

  http://epson.sn > **Mpangilio**
- Unaweza kusajili manenosiri kadhaa kwenye kipanga njia cha pasi waya ambacho hutumia usalama wa aina ya WEP. Ikiwa manenosiri kadhaa yamesajiliwa, kagua kwanza kama nenosiri lililosajiliwa limewekwa kwenye printa.

## Ujumbe kwenye Mazingira ya Mtandao

| Ujumbe | Suluhisho |
|---|---|
| The Wi-Fi environment needs to be improved. Turn the wireless router off and then turn it on. If the connection does not improve, see the documentation for the wireless router. | Baada ya kusogeza kichapishi karibu na kipanga njia pasiwaya na kuondoa vizuizi vyovyote kati yake, zima kipanga njia pasiwaya. Subiri kwa karibu sekunde 10, na kisha uiwashe. Endapo bado haitaunganishwa, angalia waraka ulioletwa pamoja na kipanga njia pasiwaya. |
| *No more devices can be connected. Disconnect one of the connected devices if you want to add another one. | Kompyuta na vifaa maizi vinavyoweza kuunganishwa kwa wakati mmoja vimeunganishwa kwenye muunganisho kamili wa Wi-Fi Direct (AP Rahisi). Ili kuongeza kompyuta nyingine au kifaa maizi, kata muunganisho wa mojawapo ya vifaa vilivyounganishwa au kiunganishe kwenye mtandao mwingine kwanza.<br><br>Unaweza kuthibitisha idadi ya vifaa pasiwaya vinavyoweza kuunganishwa kwa wakati mmmoja na idadi ya vifaa vilivyounganishwa kwa kuangalia laha la hali ya mtandao au paneli dhibiti ya kichapishi. |
| The same SSID as Wi-Fi Direct exists in the environment. Change the Wi-Fi Direct SSID if you cannot connect a smart device to the printer. | Kwenye paneli dhibiti ya kichapishi, nenda kwenye skrini ya Usanidi wa Wi-Fi Direct na uteue menyu ili kubadilisha mpangilio. Unaweza kubadilisha jina la mtandao linalofuata baada ya DIRECT-XX-. Ingiza ndani ya vibambo 22. |

## Kuchapisha Laha la Hali ya Mtandao

Unaweza kukagua maelezo ya kina ya mtandao kwa kuyachapisha.

1. Teua **Mipangilio** kwenye skrini ya nyumbani.

2. Teua **Mipangilio ya Jumla** > **Mipangilio ya Mtandao** > **Hali ya Mtandao**.

3. Teua **Chapisha Karatasi ya Hali**.

4. Angalia ujumbe, na kisha uchapishe karatasi ya hali ya mtandao.

## Kuangalia Mtandao wa Kompyuta (Windows pekee)

Kwa kutumia kisituo cha amri, angalia hali ya muunganisho wa kompyuta na njia ya muunganisho kwenye kichapishi. Hilo litakusaidia kutatua matatizo.

❏ amri ya ipconfig

Onyesha hali ya muunganisho wa kiolersura cha mtandao ambao unatumika kwa sasa kwa kompyuta.

Kwa kulinganisha maelezo ya mpangilio na mawasiliano halisi, unaweza kuangalia iwapo muunganisho ni sahihi. Endapo kuna seva anuwai za DHCP kwenye mtandao sawa, unaweza kutafuta anwani halisi iliyopangiwa kompyuta, seva inayorejelewa ya DNS, nk.

❏ Umbizo: ipconfig /all

❏ Mifano:



- amri ya pathping

  Unaweza kuthibitisha orodha ya vipanga njia vinavyopitia mafikio ya mpangishaji na uelekezaji wa mawasiliano.

  - Umbizo: pathping xxx.xxx.xxx.xxx
  - Mifano: pathping 192.0.2.222



# Maelezo ya Bidhaa


Maelezo ya Karatasi . . . . . . . . . . 250

Taarifa ya Bidhaa Tumika . . . . . . . . . . 253

Maelezo ya Programu . . . . . . . . . . 254

Orodha ya Menyu ya Mipangilio . . . . . . . . . . 263

Ufafanuzi wa Bidhaa . . . . . . . . . . 278

Taarifa ya Udhibiti . . . . . . . . . . 286

# Maelezo ya Karatasi

## Karatasi Inayopatikana na Uwezo

### Karatasi Halali ya Epson

Epson inapendekeza utumie karatasi halali ya Epson ili kuhakikisha uchapishaji wa hali ya juu.

***Kumbuka:***
- *Upatikanaji wa karatasi unategemea eneo. Kwa maekezo mapya kuhusu karatasi inayopatikana katika eneo lako, wasiliana na usaidizi wa Epson.*
- *Angalia yafuatayo kwa maelezo kuhusu aina za karatasi zinazopatikana kwa uchapishaji usio na mipaka na wa pande 2.*

  *"Karatasi la Kuchapishwa Bila Mipaka" kwenye ukurasa wa 251*

  *"Karatasi la Kuchapishwa Upande 2" kwenye ukurasa wa 252*
- *Wakati unachapisha kwenye karatasi halisi ya Epson kwa ukubwa uliowekwa na mtumiaji, mipangilio ya ubora wa chapa wa **Wastani** au **Normal** ndio hupatikana tu. Ijapokuwa baadhi ya viendeshi vya printa hukuruhusu uchague ubora wa juu wa chapa, chapa huchapishwa kwa kutumia **Wastani** au **Normal**.*

#### Karatasi inayofaa kwa kuchapisha nyaraka

| Jina la Midia | Ukubwa | Uwezo wa Kupakia (Laha) |
|---|---|---|
| Epson Bright White Ink Jet Paper | A4 | 200 |

#### Karatasi inayofaa kwa kuchapisha nyaraka na picha

| Jina la Midia | Ukubwa | Uwezo wa Kupakia (Laha) |
|---|---|---|
| Epson Photo Quality Ink Jet Paper | A4 | 100 |
| Epson Double-sided Photo Quality Ink Jet Paper | A4 | 80 |
| Epson Matte Paper-Heavyweight | A4 | 20 |
| Epson Double-Sided Matte Paper | A4 | 1 |

#### Karatasi linalofaa kwa kuchapisha picha

| Jina la Midia | Ukubwa | Uwezo wa Kupakia (Laha) |
|---|---|---|
| Epson Ultra Glossy Photo Paper | A4, 13×18 cm (5×7 in.), 10×15 cm (4×6 in.) | 20 |
| Epson Premium Glossy Photo Paper | A4, 13x18 cm (5x7 in.), 16:9 upana wa ukubwa (102x181 mm), 10x15 cm (4x6 in.) | 20 |
| Epson Premium Semigloss Photo Paper | A4, 13×18 cm (5×7 in.), 10×15 cm (4×6 in.) | 20 |

| Jina la Midia | Ukubwa | Uwezo wa Kupakia (Laha) |
|---|---|---|
| Epson Photo Paper Glossy | A4, 13×18 cm (5×7 in.), 10×15 cm (4×6 in.) | 20 |

#### Aina nyingine mbalimbali za karatasi

| Jina la Midia | Ukubwa | Uwezo wa Kupakia (Laha) |
|---|---|---|
| Epson Photo Quality Self Adhesive Sheets | A4 | 1 |

## Karatasi Inayopatikana ya Kununua

***Kumbuka:***
*Angalia yafuatayo kwa maelezo kuhusu aina za karatasi zinazopatikana kwa uchapishaji usio na mipaka na wa pande 2.*

*"Karatasi la Kuchapishwa Bila Mipaka" kwenye ukurasa wa 251*

*"Karatasi la Kuchapishwa Upande 2" kwenye ukurasa wa 252*

#### Karatasi tupu

Karatasi tupu inajumuisha karatasi ya nakala na kichwa cha barua[*1].

| Ukubwa | Uwezo wa Kupakia (Laha) |
|---|---|
| Herufi, A4, B5, A5, A6, B6, 16K (195×270 mm) | 250 |
| Inayoruhusiwa, Indian-Inayoruhususiwa, 8.5×13 in. | 50 |
| Iliyobainishwa na Mtumiaji[*2] (mm)<br>89×127 hadi 215.9×1200 | 1 |

*1 Karatasi ambayo maelezo kama vile jina la mtumaji au jina la shirika yanachapishwa awali kwenye kijajuu. Lazima kuwe na pambizo ya 3 mm au zaidi katika upande wa juu wa karatasi. Uchapishaji wa pande 2 na uchapishaji usio na kingo haupatikani kwa karatasi yenye mwambaa kichwa.

*2 Ni uchapishaji wa kompyuta unaopatikana peke yake.

#### Bahasha

| Ukubwa | Uwezo wa Kupakia (Bahasha) |
|---|---|
| Bahasha #10, Bahasha DL, Bahasha C6 | 10 |

## Karatasi la Kuchapishwa Bila Mipaka

### *Karatasi Halali ya Epson*

- Epson Bright White Ink Jet Paper
- Epson Photo Quality Ink Jet Paper

- Epson Double-sided Photo Quality Ink Jet Paper
- Epson Matte Paper-Heavyweight
- Epson Double-Sided Matte Paper
- Epson Ultra Glossy Photo Paper
- Epson Premium Glossy Photo Paper
- Epson Premium Semigloss Photo Paper
- Epson Photo Paper Glossy

**Maelezo Husika**

➡ "Karatasi Inayopatikana na Uwezo" kwenye ukurasa wa 250

### *Karatasi Inayopatikana ya Kununua*

Karatasi tupu, Karatasi la nakala, (Barua, A4)

**Maelezo Husika**

➡ "Karatasi Inayopatikana na Uwezo" kwenye ukurasa wa 250

## Karatasi la Kuchapishwa Upande 2

### *Karatasi Halali ya Epson*

- Epson Bright White Ink Jet Paper
- Epson Double-sided Photo Quality Ink Jet Paper (Uchapishaji mwenyewe wa pande 2.)
- Epson Double-Sided Matte Paper (Uchapishaji mwenyewe wa pande 2.)

**Maelezo Husika**

➡ "Karatasi Inayopatikana na Uwezo" kwenye ukurasa wa 250

### *Karatasi Inayopatikana ya Kununua*

- Karatasi tupu, karatasi ya nakala *

* Herufi, A4, B5, 16K, na ukubwa uliofafanuliwa wa mtumiaji (182×257 hadi 215.9×297 mm) inaauniwa kwa uchapishaji otomatiki wa pande 2.

**Maelezo Husika**

➡ "Karatasi Inayopatikana na Uwezo" kwenye ukurasa wa 250

## Aina Zisizopatikana za Karatasi

Usitumie karatasi zifuatazo. Utumiaji wa aina hizi za karatasi husababisha ukwamaji wa karatasi na uchafu kwenye uchapishaji.

❏ Karatasi ambazo zimekunjama kama mawimbi

❏ Karatasi ambazo zimeraruka au kukatika

❏ Karatasi ambazo zimekunjwa

❏ Karatasi ambazo ni chafu

❏ Karatasi ambazo ni nene au nyembamba zana

❏ Karatasi zilizo na vibandiko

Usitumie bahasha zifuatazo. Kutumia aina hizi za bahasha husababisha kukwakma kwa karatasi na wino kumwagika kwenye chapisho.

❏ Bahasha ambazo zimekunjwa

❏ Bahasha ambazo sehemu zao za pigo zina gundi au bahasha dirisha

❏ Bahasha ambazo ni nyembamba sana
Zinaweza kukunjama wakati wa kuchapisha.

# Taarifa ya Bidhaa Tumika

## Misimbo ya Chupa ya Wino

Epson inapendekeza utumie chupa halali za wino za Epson.

Ifuatayo ndio misimbo ya chupa halisi za wino wa Epson.

***Muhimu:***

❏ *Waranti ya Epson haishughulikii uharibifu uliosababishwa na wino mwingine kando na ule uliobainishwa, pamoja na wino wowote halali wa Epson usioundiwa printa hii au wino wowote wa mhusika mwingine.*

❏ *Bidhaa zingine ambazo hazijatengenezwa na Epson zinaweza kusababisha uharibifu ambao haujasimamiwa na udhamini wa Epson, na wakati mwingine, zinaweza kusababisha mienendo ya uchapishaji isiyo ya kawaida.*

***Kumbuka:***

❏ *Misimbo ya chupa ya wino hutofautiana kulingana na eneo. Kwa misimbo sahihi katika eneo lako, wasiliana na usaidizi wa Epson.*

❏ *Ingawa chupa za wino zinaweza kuwa na nyenzo zilizorejelezwa, hii haiathiri ufanyaji kazi au utendaji wa printa.*

❏ *Sifa na sura ya chupa ya wino zinaweza kubadilishwa bila notisi ili kuoboresha.*

**Kwa matumizi ya Uropa**

| Bidhaa | BK: Black (Nyeusi) | C: Cyan (Siani) | M: Magenta (Majenta) | Y: Yellow (Manjano) |
|---|---|---|---|---|
| ET-4850/ET-4856 | 102 | 102 | 102 | 102 |

| Bidhaa | BK: Black (Nyeusi) | C: Cyan (Siani) | M: Magenta (Maje-nta) | Y: Yellow (Manjano) |
|---|---|---|---|---|
| L6290 Series | 101 | 101 | 101 | 101 |
| ET-4850U | 120 | 120 | 120 | 120 |

***Kumbuka:***
*Tembelea tovuti ifuatayo kwa maelezo kuhusu nyuga za chupa ya wino ya Epson.*

*http://www.epson.eu/pageyield*

### For Australia and New Zealand

| BK: Black (Nyeusi) | C: Cyan (Siani) | M: Magenta (Majenta) | Y: Yellow (Manjano) |
|---|---|---|---|
| 502 | 502 | 502 | 502 |

### Kwa matumizi ya Asia

| BK: Black (Nyeusi) | C: Cyan (Siani) | M: Magenta (Majenta) | Y: Yellow (Manjano) |
|---|---|---|---|
| 001 | 001 | 001 | 001 |

## Msimbo wa Kisanduku cha Ukarabati

Kikasha cha matengenezo kinaweza kununuliwa na kubadilishwa na mtumiaji.

Epson inapendekeza utumiaji wa kisanduku halali cha ukarabati cha Epson.

Ifuatayo ni msimbo wa kisanduku halisi cha ukarabati cha Epson.

T04D1

***Muhimu:***
*Pindi tu baada ya kusakinisha kisanduku cha ukarabati kwenye kichapishi maalum hakiwezi kutumika kwa vichapishi vingine.*

# Maelezo ya Programu

Sehemu hii hutambulisha huduma za mtandao na bidhaa za programu zinazopatikana kwa kichapishi chako kutoka kwenye tovuti ya Epson.

# Programu ya Kuchapisha

## Programu ya Kuchapisha kutoka katika Kompyuta (Kiendeshi cha Kichapishi cha Windows)

Kiendeshi cha kichapishi hudhibiti printa kulingana na amri za programu. Kuweka mipangilio kwenye kiendeshi cha kichapishi hutoa matokeo bora zaidi ya uchapishaji. Pia unaweza kuangalia hali ya kichapishi au kuiweka ikiwa katika hali nzuri kwa kutumia huduma ya kiendeshi cha kichapishi.

***Kumbuka:***
*Unaweza kubadilisha lugha ya kiendeshi cha kichapishi. Teua lugha unayotaka kutumia kutoka kwa mpangilio wa **Lugha** kwenye kichupo cha **Utunzaji**.*

### Kufikia kiendeshi cha kichapishaji kutoka programu

Ili uweke mipangilio inayotumika kwenye programu unayotumia peke yake, ifikie kutoka kwa programu hiyo.

Chagua **Chapisha** au **Usanidi wa Uchapishaji** katika menyu ya **Faili**. Chagua printa yako, na kisha ubofye **Mapendeleo** au **Sifa**.

***Kumbuka:***
*Utendaji hutofautiana kulingana na programu. Angalia msaada wa programu kwa maelezo.*

### Kufikia kiendeshi cha printa kutoka kwa paneli dhibiti

Kuweka mipangilio inayotumika kwenye programu zote, ifikie kutoka kwa paneli dhibiti.

❏ Windows 10/Windows Server 2019/Windows Server 2016

Bofya kitufe cha kuwasha kisha uchague **Mifumo ya Windows** > **Paneli Dhibiti** > **Tazama vifaa na vichapishi** katika **Maunzi na Sauti**. Bofya kulia kwenye kichapihsi chako, au bonyeza na uishikilie na kisha uteue **Mapendeleo ya uchapishaji**.

❏ Windows 8.1/Windows 8/Windows Server 2012 R2/Windows Server 2012

Teua **Eneo Kazi** > **Mipangilio** > **Paneli Dhibiti** > **Tazama vifaa na vichapishi** katika **Maunzi na Sauti**. Bofya kulia kwenye kichapihsi chako, au bonyeza na uishikilie na kisha uteue **Mapendeleo ya uchapishaji**.

❏ Windows 7/Windows Server 2008 R2

Bofya kitufe cha kuwasha, na uteue **Paneli Dhibiti** > **Tazama vifaa na vichapishi** katika **Maunzi na Sauti**. Bofya kulia kwenye kichapishi chako na uteue **Mapendeleo ya kichapishi**.

❏ Windows Vista/Windows Server 2008

Bofya kitufe cha kuwasha, na uteue **Paneli Dhibiti** > **Kichapishi** katika **Maunzi na Sauti**. Bofya kulia kwenye kichapishi chako na uteue **Mapendeleo ya kichapishi**.

❏ Windows XP/Windows Server 2003 R2/Windows Server 2003

Bofya kitufe cha kuwasha, na uteue **Paneli Dhibiti** > **Vichapishi na Maunzi Nyingine** > **Vichapishi na Faksi**. Bofya kulia kwenye kichapishi chako na uteue **Mapendeleo ya kichapishi**.

### Kufikia kiendeshi cha printa kutoka kwa ikoni ya printa kwenye mwambaa kazi

Ikoni ya printa iliyo kwenye mwambaa kazi wa eneo kazi ni ikoni ya mkato ya kukuwezesha ufikie kiendeshi cha printa kwa urahisi.

Ukibofya ikoni ya printa na uchague **Mipangilio ya Printa**, unaweza kufikia dirisha sawa la mipangilio ya printa na linaloonekana katika paneli dhibiti. Ukibofya ikoni hii mara mbili, unaweza kuona hali ya printa.

***Kumbuka:***
*Ikiwa ikoni ya printa haionekani kwenye mwabaa kazi, nenda kwa dirisha la kiendeshi cha printa, bofya **Inachunguza Mapendeleo** kwenye kichupo cha **Utunzaji**, na kisha uchague **Sajili ikoni ya njiamkato kwenye upau kazi**.*

#### Kuanzisha huduma

Nenda kwa dirisha la kiendeshi cha kichapishi. Bofya kichupo cha **Utunzaji**.

### *Kuweka Mipangilio ya Utendaji kwa Kiendeshi cha Printa cha Windows*

Unaweza kuweka mipangilio kama vile kuwezesha **EPSON Status Monitor 3**.

1. Nenda kwa dirisha la kiendeshi cha printa.

2. Bofya **Mipangilio Iliyorefushwa** kwenye kichupo cha **Utunzaji**.

3. Weka mipangilio inayofaa, na kisha ubofye **SAWA**.

   Angalia msaada wa mtandaoni kwa ufafanuzi wa vipengele vya mpangilio.

#### Maelezo Husika

➡ "Programu ya Kuchapisha kutoka katika Kompyuta (Kiendeshi cha Kichapishi cha Windows)" kwenye ukurasa wa 255

## Programu ya Kuchapisha kutoka katika Kompyuta (Kiendeshi cha Kichapishi cha Mac OS)

Kiendeshi cha kichapishi hudhibiti printa kulingana na amri za programu. Kuweka mipangilio kwenye kiendeshi cha kichapishi hutoa matokeo bora zaidi ya uchapishaji. Pia unaweza kuangalia hali ya kichapishi au kuiweka ikiwa katika hali nzuri kwa kutumia huduma ya kiendeshi cha kichapishi.

#### Kufikia kiendeshi cha kichapishaji kutoka programu

Bofya **Mpangilio wa Karatasi** au **Chapisha** kwenye menyu ya **Faili** ya programu yako. Inapohitajika, bofya **Onyesha Maelezo** (au ▼) ili uongeze dirisha la uchapishaji.

***Kumbuka:***
*Kwa kutegemea programu inayotumika, huenda **Usanidi wa Kurasa** usionyeshwe kwenye menyu ya **Faili**, na oparesheni ya kuonyesha skrini ya uchapishaji inaweza kuwa tofauti. Angalia usaidizi wa programu kwa maelezo.*

#### Kuanzisha huduma

Teua **Mapendeleo ya Mfumo** kwenye menyu ya Apple > **Vichapishaji na Vitambazaji** (au **Chapisha na Utambaze**, **Chapisha na Utume Faksi**), kisha uteue kichapishaji. Bofya **Chaguo na Vifaa** > **Huduma** > **Fungua Huduma ya Printa**.

#### *Mwongozo wa Mac OS Kiendeshi cha Printa*

**Epson Printer Utility**

Unaweza kufanya dhima ya ukarabati kama vile ukaguzi wa nozeli na usafishaji wa kichwa cha kichapisha, na kwa kuanzisha **EPSON Status Monitor**, unaweza kuangalia hali ya printa na maelezo ya hitilafu.




#### *Kufikia Dirisha la Mipangilio ya Operesheni la Kiendeshi cha Kichapishi cha Mac OS*

Teua **Mapendeleo ya Mfumo** kwenye menyu ya Apple > **Vichapishaji na Vitambazaji** (au **Chapisha na Utambaze**, **Chapisha na Utume Faksi**), kisha uteue kichapishaji. Bofya **Chaguo na Vifaa** > **Chaguo** (au **Kiendeshi**).

## Programu ya Uchapishaji Haraka na Furaha kutoka katika Kompyuta (Epson Photo+)

Epson Photo+ ni programu inayokuruhusu kuchapusha taswira kwa urahisi kwa mipangilio mbalimbali. Pia unaweza kufanya marekebisho ya taswira na kurekebisha mkao unapotazama uhakiki wa waraka wako. Pia unaweza kuongeza mwangaza kwenye taswira zako kwa kuongeza matini na mihuri unapopenda. Unapochapisha kwenye karatasi hjalali la picha la Epson, utendaji wa wino unetumika kwa upeo wa juu kuunda ukamilisho maridadi kwa rangi nzuri zaidi.

Angalia msaada wa programu kwa maelezo.

***Kumbuka:***

- *Programu endeshi za Windows Server hazikubaliwi.*
- *Ili utumie programu hii kiendeshji cha kichapishi kinahitaji kusakinishwa.*

**Kuanzia kwenye Windows**

- Windows 10

  Bofya kitufe cha kuwasha kisha uteue **Epson Software** > **Epson Photo+**.

- Windows 8.1/Windows 8

  Andika jina la programu katika sehemu ya utafutaji, na kisha uchague ikoni inayoonekana.

- Windows 7/Windows Vista/Windows XP

  Bofya kitufe cha kuwasha kisha uteue **Programu Zote** au **Programu** > **Epson Software** > **Epson Photo+**.

#### Kuanzia kwenye Mac OS

Teua **Nenda** > **Programu** > **Epson Software** > **Epson Photo+**.

#### Maelezo Husika

➡ “Kusakinisha Programu Kando” kwenye ukurasa wa 128

## Programu ya Kuendesha Kichapishi Rahisi kutoka kwenye Kifaa maizi (Epson Smart Panel)

Epson Smart Panel ni programu inayokuwezesha kutekeleza operesheni za kichapishi rahisi ikiwa ni pamoja na kuchapisha, kunakili au kutambaza kutoka kwa kifaa maizi kama vile smartphone na kompyuta kibao. Unaweza kuunganisha kichapishi na kifaa maizi kupitia mtandao pasiwaya, kuangalia viwango vya wino na hali ya kichapishi, na kuangalia suluhisho iwapo kosa litatokea. Pia unaweza kunakili rahisi kwa kusajili nakala ya kipendwa.

Tafuta na usakinishe Epson Smart Panel kutoka App Store au Google Play.

## Programu ya Kuchapisha kwa Urahisi kutoka katika Programu ya Android (Epson Print Enabler)

Epson Print Enabler ni programu ambayo hukuruhusu kuchapisha hati, barua pepe, picha na kurasa za wavuti pasiwaya moja kwa moja kutoka katika simu au kompyuta yako kibao (Toleo la Android v4.4 au jipya zaidi). Kwa kudonoa mara chache tu, kifaa chako cha Android kinaweza kugundua kichapishi cha Epson ambacho kimeunganishwa kwenye mtandao sawa pasiwaya.

Tafuta na usakinishe Epson Print Enabler kutoka Google Play.

# Programu ya Utambazaji

## Programu ya Kutambaza kutoka katika Kompyuta (Epson ScanSmart)

Programu hii inakuruhusu kutambaza nyaraka na picha kwa urahisi kisha kuhifadhi picha zilizotambazwa kwa njia rahisi.

Angalia msaada wa Epson ScanSmart kwa maelezo kuhusu kutumia vipengele hivi.

#### Kuanzia kwenye Windows

- Windows 10

  Bofya kitufe cha kuwasha, na kisha uteue **Epson Software** > **Epson ScanSmart**.
- Windows 8.1/Windows 8

  Andika jina la programu katika sehemu ya utafutaji, na kisha uchague ikoni inayoonekana.
- Windows 7

  Bofya kitufe cha kuwasha kisha uteue **Programu Zote** > **Epson Software** > **Epson ScanSmart**.

#### Kuanzia kwenye Mac OS

Teua **Nenda** > **Programu** > **Epson Software** > **Epson ScanSmart**.

## ProgramuProgramu ya Kutuma Faksi

### Programu-tumizi kwa Usanidi wa Operesheni za Faksi na Kutuma Faksi (FAX Utility)

FAX Utility ni programu inayokuruhusu kusanidi mipangilio mbalimbali ya kutuma faksi kutoka kwa kompyuta. Unaweza kuunda au kuhariri orodha ya waasiliani ya kutumiwa wakati wa kutuma faksi, usanidi ili uhifadhi faksi zilizopokewa katika famati ya PDF kwenye kompyuta, na zaidi. Angalia msaada wa programu kwa maelezo.

***Kumbuka:***
- *Programu endeshi za Windows Server hazikubaliwi.*
- *Hakikisha umesakinishwa kiendeshi cha printa kabla ya kusakinisha FAX Utility.*
- *Hakikisha FAX Utility imesakinishwa. tazama "Kuwasha Windows" au "Kuwasha Mac OS" hapa chini ili kuangalia iwapo programu imesakinishwa.*

#### Kuanzia kwenye Windows

- Windows 10

  Bofya kitufe cha kuwasha, na uteue **Epson Software** > **FAX Utility**.
- Windows 8.1/Windows 8

  Andika jina la programu katika sehemu ya utafutaji, na kisha uchague ikoni inayoonekana.
- Windows 7/Windows Vista/Windows XP

  Bofya kitufe cha kuanza, na uchague **Programu Zote** (au **Programu**) > **Epson Software** > **FAX Utility**.

#### Kuanzia kwenye Mac OS

Teua **Mapendeleo ya Mfumo** kutoka kwenye menyu ya Apple > **Vichapishi na Vitambazaji** (au **Chapisho & Tambazo**, **Chapisho na Faksi**), na kisha uchague kichapishi (FAKSI). Bofya **Chaguo na Vifaa** > **Huduma** > **Fungua Huduma ya Printa**.

#### Maelezo Husika

➡ "Kutuma Faksi Kutoka kwa Kompyuta" kwenye ukurasa wa 103

➡ "Kupokea Faksi kwenye Kompyuta" kwenye ukurasa wa 107

## Programu-tumizi ya Kutuma Faksi (Kiendeshi cha PC-FAX)

Kiendeshi cha PC-FAX ni programu inakuwezesha kutuma hati iliyoundwa kwenye programu tofauti kama faksi moja kwa moja kutoka kwa kompyuta. Kiendeshi cha PC-FAX husakinishwa wakati unasakinisha Huduma ya FAKSI. Angalia msaada wa programu kwa maelezo.

***Kumbuka:***
- *Programu endeshi za Windows Server hazikubaliwi.*
- *Angalia ikiwa kiendeshi cha PC-FAX kimesakinishwa. Angalia "Kufikia kutoka Windows" au "Kufikia kutoka Mac OS" hapa chini.*
- *Utendaji huwa tofauti kulingana na programu uliyotumia kuunda hati hiyo. Angalia msaada wa programu kwa maelezo.*

#### Kufikia kutoka kwa Windows

Katika programu, chagua **Chapisha** au **Usanidi wa Uchapishaji** katika menyu ya **Faili**. Chagua printa yako (FAKSI), na kisha ubofye **Mapendeleo** au **Sifa**.

#### Kufikia kutoka kwa Mac OS

Katika programu, chagua **Chapisha** kutoka kwa menyu ya **Faili**. Chagua printa yako (FAKSI) kama mpangilio wa **Printa**, na kisha uchague **Fax Settings** au **Recipient Settings** katika menyu ya kidukizo.

#### Maelezo Husika

➡ "Kutuma Faksi Kutoka kwa Kompyuta" kwenye ukurasa wa 103

# ProgramuProgramu ya Uundaji wa Kifurushi

## Application for Creating Driver Packages (EpsonNet SetupManager)

EpsonNet SetupManager ni programu ya kuunda kifurushi kwa usakinishaji rahisi wa kichapishi, kama vile kusakinisha kiendeshi cha kichapishi, kusakinisha EPSON Status Monitor na kuunda kituo cha kichapishi. Programu hii huruhusu msimamizi kuunda vifurushi vya kipekee na kuvisambaza kwenye vikundi.

Kwa maelezo zaidi, tembelea tovuti yako ya kimaeneo ya Epson.

http://www.epson.com

# Programu ya Kuweka Mipangilio

## Programu ya Kusawazisha Utendakazi wa Kichapishi (Web Config)

Web Config ni programu ambayo huendeshwa katika kivinjari cha wavuti, kama vile Microsoft Edge na Safari, kwenye kompyuta na kifaa mahiri. Unaweza kuthibitisha hali ya printa au kubadilisha huduma ya ntandao na mipangilio ya printa. Ili utumie Web Config, unganisha printa na kompyuta au kifaa kwenye mtandao mmoja.

Vivinjari vifuatavyo vinakubaliwa. Tumia toleo jipya.

Microsoft Edge, Internet Explorer, Firefox, Chrome, Safari

***Kumbuka:***
*Huenda ukaombwa kuingiza nenosiri la msimamizi unapoendesha Web Config. Tazama maelezo husika hapa chini kupata maelezo zaidi.*

**Maelezo Husika**

➡ "Thamani Chaguo-Msingi ya Nenosiri la Msimamizi" kwenye ukurasa wa 16

### *Kuendesha Web Config Kwenye Kivinjari Wavuti*

1. Angalia anwani ya IP ya kichapishi.

   Teua ikoni ya mtandao kwenye skrini ya nyumbani ya kichapishi, na kisha uteue mbinu ya muunganisho amilifu ili kuthibitisha anwani ya IP ya kichapishi.

   ***Kumbuka:***
   *Pia unaweza kuangalia anwani ya IP kwa kuchapisha ripoti ya muunganisho wa mtandao.*

2. Zindua kivinjari Wavuti kwenye kompyuta au kifaa mahiri, na kisha uingize anwani ya IP ya kichapishi.

   Umbizo:

   IPv4: http://anwani ya IP ya kichapishi/

   IPv6: http://[anwani ya IP ya kichapishi]/

   Mifano:

   IPv4: http://192.168.100.201/

   IPv6: http://[2001:db8::1000:1]/

   ***Kumbuka:***
   *Ukitumia kifaa mahiri, unaweza pia kuendesha Web Config kutoka katika skrini ya maelezo ya bidhaa ya Epson Smart Panel.*

   Kwa vile kichapishi kinatumia cheti cha kutiwa sahihi binafsi kufikia HTTPS, onyo huonyeshwa kwenye kivinjari unapoanza Web Config; hii haionyeshi kuwa kuna tatizo na unaweza kupuuza kwa usalama.

**Maelezo Husika**

➡ "Kuchapisha Ripoti ya Muunganisho wa Mtandao" kwenye ukurasa wa 241

### *Kuendesha Web Config kwenye Windows*

Unapounganisha kompyuta kwenye kichapishi kwa kutumia WSD, fuata hatua hapa chini ili kuendesha Web Config.

1. Fungua orodha ya vichapishi kwenye kompyuta.

   ❏ Windows 10

   Bofya kitufe cha kuwasha kisha uchague **Mifumo ya Windows** > **Paneli Dhibiti** > **Tazama vifaa na vichapishi** katika **Maunzi na Sauti**.

   ❏ Windows 8.1/Windows 8

   Teua **Eneo-kazi** > **Mipangilio** > **Paneli Dhibiti** > **Tazama vifaa na vichapishi** katika **Maunzi na Sauti** (au **Maunzi**).

- ❏ Windows 7

  Bofya kitufe cha kuwasha, na uteue **Paneli Dhibiti** > **Tazama vifaa na vichapishi** katika **Maunzi na Sauti**.

- ❏ Windows Vista

  Bofya kitufe cha kuwasha, na uteue **Paneli Dhibiti** > **Kichapishi** katika **Maunzi na Sauti**.

2. Bofya kulia kwenye kichapishi chako na uteue **Sifa**.

3. Teua kichupo cha **Huduma ya Wavuti** na ubofye URL.

   Kwa vile kichapishi kinatumia cheti cha kutiwa sahihi binafsi kufikia HTTPS, onyo huonyeshwa kwenye kivinjari unapoanza Web Config; hii haionyeshi kuwa kuna tatizo na unaweza kupuuza kwa usalama.

#### *Kuendesha Web Config kwenye Mac OS*

1. Teua **Mapendeleo ya Mfumo** kwenye menyu ya Apple > **Vichapishaji na Vitambazaji** (au **Chapisha na Utambaze**, **Chapisha na Utume Faksi**), kisha uteue kichapishaji.

2. Bofya **Chaguo na Usambazaji** > **Onyesha Tovuti ya Kichapishi**.

   Kwa vile kichapishi kinatumia cheti cha kutiwa sahihi binafsi kufikia HTTPS, onyo huonyeshwa kwenye kivinjari unapoanza Web Config; hii haionyeshi kuwa kuna tatizo na unaweza kupuuza kwa usalama.

## Programu ya Kusanidi Kifaa Kipya kwenye Mtandao (EpsonNet Config)

EpsonNet Config ni programu inayokuruhusu kuweka anwani na itifaku za kusano ya mtandao. Angalia mwongozo wa uendeshaji kwa EpsonNet Config au msaada wa programu-tumizi kwa maelezo zaidi.

### Kuanzia kwenye Windows

- ❏ Windows 10/Windows Server 2019/Windows Server 2016

  Bofya kitufe cha kuwasha, na kisha uteue **EpsonNet** > **EpsonNet Config**.

- ❏ Windows 8.1/Windows 8/Windows Server 2012 R2/Windows Server 2012

  Andika jina la programu katika sehemu ya utafutaji, na kisha uchague ikoni inayoonekana.

- ❏ Windows 7/Windows Vista/Windows XP/Windows Server 2008 R2/Windows Server 2008/Windows Server 2003 R2/Windows Server 2003

  Bofya kitufe cha kuanza, na uchague **Programu Zote** au **Programu** > **EpsonNet** > **EpsonNet Config SE** > **EpsonNet Config**.

### Kuanzia kwenye Mac OS

**Nenda** > **Programu** > **Epson Software** > **EpsonNet** > **EpsonNet Config SE** > **EpsonNet Config**.

### Maelezo Husika

➡ "Kusakinisha Programu Kando" kwenye ukurasa wa 128

## Programu ya Kusasisha

### Programu ya Kusasisha Programu na Vifaa Dhibiti (Epson Software Updater)

Epson Software Updater ni programu ambayo husakinisha programu mpya na kusasisha vifaa dhabiti na miongozo kupitia Mtandao. Iwapo unataka kuangalia taarifa ya visasisho mara kwa mara, unaweza kuweka kipindi cha kuangalia visasisho kwenye Mipangilio ya Epson Software Updater ya Sasisho Otomatiki.

***Kumbuka:***
*Programu endeshi za Windows Server hazikubaliwi.*

#### Kuanzia kwenye Windows

- Windows 10

  Bofya kitufe cha kuwasha, na kisha uteue **EPSON Software** > **Epson Software Updater**.

- Windows 8.1/Windows 8

  Andika jina la programu katika sehemu ya utafutaji, na kisha uchague ikoni inayoonekana.

- Windows 7/Windows Vista/Windows XP

  Bofya kitufe cha kuwasha, na kisha uteue **Programu Zote** (au **Programu**) > **EPSON Software** > **Epson Software Updater**.

***Kumbuka:***
*Kadhalika, unaweza kuwasha Epson Software Updater kwa kubofya ikoni ya kichapishi kwenye mwambaa kazi ulio kwenye eneo kazi, na kisha uteue **Kisasisho cha Programu**.*

#### Kuanzia kwenye Mac OS

Teua **Nenda** > **Programu** > **Epson Software** > **Epson Software Updater**.

#### Maelezo Husika

➡ "Kusakinisha Programu Kando" kwenye ukurasa wa 128

# Orodha ya Menyu ya Mipangilio

Teua **Mipangilio** kwenye skrini ya nyumbani ya kichapishi ili kufanya mipangilio mbalimbali.

## Mipangilio ya Jumla

Teua menyu kwenye paneli dhibiti kama ilivyofafanuliwa hapa chini.

**Mipangilio** > **Mipangilio ya Jumla**

### Mipangilio Msingi

Teua menyu kwenye paneli dhibiti kama ilivyofafanuliwa hapa chini.

**Mipangilio** > **Mipangilio ya Jumla** > **Mipangilio Msingi**

Mwangaza wa LCD:

Rekebisha mwangaza wa skrini ya LCD.

Sauti:

Rekebisha sauti.

- Nyamazisha

  Teua **On** ili kunyamazisha sauti kama zile zitolewazo na **Ubonyezaji Kitufe**.

- Hali ya Kawaida

  Teua sauti kama vile **Ubonyezaji Kitufe**.

- Hali Tulivu

  Teua sauti kama vile **Ubonyezaji Kitufe** kwenye **Hali Tulivu**.

Kipima saa cha Kulala:

Rekebisha kipindi cha muda cha kuingia kwenye modi ya kusinzia (modi ya kuhifadhi nishati) wakati kichapishi hakijatekeleza operesheni zozote. Skrini ya LCD inakuwa nyeusi wakati muda uliowekwa unapita.

Kipima Saa ya Kuzima:

Huenda bidhaa yako ina kipengele hiki au kipengele cha **Mip'ilio ya Kuzima** kulingana na eneo la ununuzi.

Teua mpangilio huu ili kuzima kichapishi kiotomatiki wakati hakijatumiwa kwa kipindi cha muda uliobainishwa. Unaweza kurekebisha muda kabla ya udhibiti wa nishati kutekelezwa. Uongezaji wowote utaathiri utumiaji wa nishati wa kifaa. Tafadhali zingatia mazingira kabla ya kufanya mabadiliko yoyote.

Mip'ilio ya Kuzima:

Huenda bidhaa yako ina kipengele hiki au kipengele cha **Kipima Saa ya Kuzima** kulingana na eneo la ununuzi.

- Zima Ikiwa Haitumiki

  Teua mpangilio huu ili kuzima kichapishi kiotomatiki iwapo hakijatumiwa kwa kipindi cha muda uliobainishwa. Uongezaji wowote utaathiri utumiaji wa nishati wa kifaa. Tafadhali zingatia mazingira kabla ya kufanya mabadiliko yoyote.

- Zima ikiwa Imetenganishwa

  Teua mpangilio huu ili kuzima printa baada ya muda maalum wakati vituo tarishi zote ikijumuisha kituo cha LINE kimetenganishwa. Kipengele hiki huenda kisipatiokane kulingana na eneo lako.

  Angalia tovuti ifuatayo kwa muda maalum.

  https://www.epson.eu/energy-consumption

Mipangilio ya Tarehe/Saa:

- Tarehe/Saa

  Ingiza tarehe na saa ya sasa.

- Saa za Mchana Mrefu

  Teua mpangilio wa wakati wa majira ya joto unaotumika katika eneo lako.

- Utofauti wa Saa

  Ingiza tofauti ya saa kati ya saa yako ya ndani na UTC (Saa Inayoratibiwa ya Kimataifa).

Nchi/Eneo:

Teua nchi au eneo ambalo unatumia kichapishi chako. Iwapo utabadilisha nchi au eneo, mipangilio yako ya faksi inarejea kwa chaguo-msingi na lazima uiteue tena.

Lugha/Language:

Teua lugha inayotumiwa kwenye skrini ya LCD.

Pazia:

Badilisha rangi ya mandharinyuma ya skrini ya nyumbani.

Muda wa Shughuli Umeisha:

Teua **On** ili kurejesha skrini ya kwanza wakati hakuna operesheni imetekelezwa kwa muda uliobainishwa.

Kibodi:

Badillisha muundo wa kibodi kwenye skrini ya LCD.

**Maelezo Husika**

➡ "Kuhifadhi Nishati" kwenye ukurasa wa 128

➡ "Kuingiza Vibambo" kwenye ukurasa wa 27

## Mipangilio ya Printa

Teua menyu kwenye paneli dhibiti kama ilivyofafanuliwa hapa chini.

**Mipangilio** > **Mipangilio ya Jumla** > **Mipangilio ya Printa**

Mipangilio Chanzo Karatasi:

Mipangilio ya Karatasi:

Chagua ukubwa wa karatasi na aina ya karatasi uliyopakia kwenye chanzo cha karatasi.Unaweza kufanya **Mip. ya Kar'si U'ipenda** kwenye ukubwa wa karatasi na aina ya karatasi.

A4/Letter Ubadilishaji Otomatiki:

Teua **On** Ili kuweka karatasi kutoka kwa chanzo cha karatasi kilichowekwa ukubwa wa A4 wakati hakuna chanzo cha karatasi kilichowekwa kama Letter, au huweka kutoka kwa chanzo cha karatasi kilichowekwa ukubwa wa Letter ambapo hakuna chanzo cha karatasi kilichowekwa A4.

Ilani ya Hitilafu:

Teua **On** ili kuonyesha ujumbe wa kosa wakati ukubwa wa karatasi ulioteuliwa haufanani na karatasi iliyopakiwa.

Onyesho Otom. Usanidi wa Karatasi:

Chagua **On** ili kuonyesha skrini ya **Mipangilio ya Karatasi** unapopakia kwenye kaseti ya karatasi. Ukilemaza kipengele hiki, huwezi kuchapisha kutoka kwenye iPhone, iPad au iPod touch ukitumia AirPrint.

### Mipangilio Uchapishaji Jumla:

Mipangilio hii ya chapisho inatumiwa wakati unachapisha kwa kutumia kifaa cha nje bila kutumia kiendeshi cha kichapishaji. Mipangilio hii ya chapisho inatumiwa wakati unachapisha kwa kutumia kiendeshi cha kichapishaji.

#### Fidia ya Juu:

Rekebisha pambizo ya juu ya karatasi.

#### Fidia ya Kushoto:

Rekebisha pambizo ya kushoto ya karatasi.

#### Mwendo wa Juu Upande wa Nyuma:

Rekebisha pambizo ya juu ya ukurasa wa nyuma wakati unatekeleza uchapishaji wa pande 2.

#### Mwendo Kushoto Upande wa Nyuma:

Rekebisha pambizo ya kushoto ya ukurasa wa nyuma wakati unatekeleza uchapishaji wa pande 2.

#### Kagua Upana wa Karatasi:

Teua **On** ili kuangalia upana wa karatasi kabla ya kuchapisha. Hii huzuia uchapishaji nje ya mipaka ya karatasi wakati mpangilio wa ukubwa wa karatasi sio sahihi, lakini hii inaweza kupunguza kasi ya uchapishaji.

#### Ruka Ukurasa Tupu:

Huruka kurasa tupu katika data ya uchapishaji kiotomatiki.

### Kitatatua Hitilafu Kiotomatiki:

Teua hatua ya kutekeleza wakati kosa la uchapishaji ya pande 2 linatokea au kosa la kujaa kwa kumbukumbu linapotokea.

- ❏ On

  Huonyesha tahadhari na vichapisho katika modi ya upande mmoja wakati kosa la uchapishaji wa pande 2 linatokea, au huchapisha kile kichapishi kinaweza kuchakata wakati kosa la kujaa kwa kumbukumbu linatokea.

- ❏ Zima

  Huonyesha ujumbe wa kosa na kukatisha uchapishaji.

### Hali Tulivu:

Teua **On** ili kupunguza kelele wakati wa kuchapisha, hata hivyo, hii inaweza kupunguza kasi ya uchapishaji. Kulingana na aina ya karatasi na mipangilio ya ubora wa kuchapisha uliyoteua, huenda kusiwe na tofauti katika kiwango cha kelele ya kichapishi.

### Muda wa Kukausha Wino:

Teua muda wa kukausha wino unaotaka kutumia unapotekeleza uchapishaji wa pande 2.Kichapishi huchapisha upande mwingine baada ya kuchapisha upande mmoja.Iwapo chapisho lako limepakwa wino, ongeza mpangilio wa muda.

Muungan. Kompyuta kupitia USB:

Teua **Wezesha** ili kuruhusu kompyuta kufikia kichapishi inapounganishwa kwenye USB. Wakati **Lemaza** imeteuliwa, uchapishaji na utambazaji ambao haujatumwa kupitia muunganisho wa mtandao unazuiwa.

**Maelezo Husika**

➡ "Kuweka Karatasi" kwenye ukurasa wa 32

## Mipangilio ya Mtandao

Teua menyu kwenye paneli dhibiti kama ilivyofafanuliwa hapa chini.

**Mipangilio** > **Mipangilio ya Jumla** > **Mipangilio ya Mtandao**

Usanidi wa Wi-Fi:

Sanidi au badilisha mipangilio ya mtandao wa pasi waya. Chagua mbinu ya muunganisho kutoka kwa zifuatazo na kisha ufuate maagizo kwenye paneli dhibiti.

Wi-Fi (Inapendekezwa):

- ❏ Sogora ya Kusanidi Wi-Fi
- ❏ Sukuma Kitufe cha Usanidi (WPS)
- ❏ Nyingine
  - ❏ Usanidi Msimbo PIN (WPS)
  - ❏ Unganisha Wi-Fi Kiotomatiki
  - ❏ Lemaza Wi-Fi

    Unaweza kutatua matatizo ya mtandao kwa kulemaza mipangilio ya Wi-Fi au kuweka mipangilio ya Wi-Fi tena. Teua  > **Wi-Fi (Inapendekezwa)** > **Badilisha Mipangilio** > **Nyingine** > **Lemaza Wi-Fi** > **Anza Kusanidi**.

Wi-Fi Direct:

- ❏ iOS
- ❏ Vifaa Vingine vya OS
- ❏ Menu
  - ❏ Badilisha Jina la Mtandao
  - ❏ Badilisha Nywila
  - ❏ Lemaza Wi-Fi Direct
  - ❏ Rejeza Mipangilio Chaguo-msingi

Usanidi wa Lana ya Waya:

Sanidi au badilisha muunganisho wa mtandao ambao hutumia kebo za LAN na kipanga njia. Wakati hii inatumika, miunganisho ya Wi-Fi inalemazwa.

Hali ya Mtandao:

Huonyesha au huchapisha mipangilio ya sasa ya mtandao.

- Hali ya LAN ya waya/Wi-Fi
- Hali ya Wi-Fi Direct
- Chapisha Karatasi ya Hali

Ukaguzi wa Muunganisho:

Huangalia muunganisho wa mtandao wa sasa na kuchapisha ripoti. Ikiwa kuna matatizo yoyote ya muunganisho, kagua ripoti ili utatue tatizo.

